**20 APRILI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 20 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, sasa aulize swali lake.

Na. 136

### Ujenzi wa barabara ya Kwamtoro – Sanzawa hadi Mpendo - Chemba

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga barabara ya Kwamtoro - Sanzawa hadi Mpendo katika Wilaya ya Chemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya tathmini ya marekebisho ya kipande cha Sanzawa – Mpendo chenye urefu wa kilomita 38.2 ambapo shilingi bilioni 2.06 zinahitajika. Serikali imeendelea kuihudumia barabara hiyo ambapo mwaka wa fedha wa 2022/2023 shilingi milioni 48 zimepelekwa kwa ajili ya kufanya matengenezo kwenye

maeneo korofi yenye urefu wa kilomita Nane kati ya Kwamtoro na Sanzawa katika Vijiji vya Kurio na Moto. Aidha, ukarabati wa *box culvert* katika Kijiji cha Moto umekamilika. Kwa sasa Mkandarasi anafanya maandalizi ya kuchonga barabara eneo korofi la Kurio lenye urefu wa kilomita Tatu.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2023/2024, serikali itatenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza kufanya matengenezo kwenye eneo korofi la mawe kati ya Sanzawa na Mpendo lenye urefu wa kilometa 34.2.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara za Jimbo la Chemba kulingana na upatikanaji wa fedha ili kuimarisha usafiri na usafirishaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni. Swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Moja, barabara hii inaunganisha Mikoa Mitatu. Inaunganisha Mkoa wa Singida, Dodoma na Manyara. Naomba kujua ni kwa nini, barabara hii tusiipandishe hadhi iwe *TANROADS* ili iweze kuhudumiwa kwa urahisi zaidi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Naibu Waziri Jimbo Lake na Jimbo langu linaunganishwa na barabara chafu kweli kweli, kati ya Seya na Zajiro kwake. Nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha barabara hiyo inatengenezwa? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupandisha hadhi barabara hii ambayo inaunganisha Mikoa Mitatu ya Singida Dodoma na Manyara, utaratibu upo wa kisheria kwa maana lazima vikao vianze katika ngazi ya Wilaya, vikitoka kwenye Wilaya viende kwenye Bodi ya Barabara ya Mkoa na baada ya kutoka Bodi ya Barabara ya Mkoa viende *RCC* na ndipo hadhi ya barabara hii iweze kupandishwa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili. Nikiri ni kweli barabara hii inayounganisha kati ya Jimbo la Mheshimiwa Monni na Jimbo langu mimi la Chamwino na tayari maelekezo yalikuwa yameshakwenda kwa Mameneja wote wa *TARURA* wa Mikoa, kuhakikisha kwamba wanatenga fedha ya kuhakikisha vipande vya barabara hii vinaanza kutengenezwa. Katika mwaka huu wa fedha tuliouombea wa 2023/2024 barabara hii vilevile imo katika barabara zilizoombewa fedha. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza kukarabati barabara ya kuanzia Bwakila Chini mpaka Bwakila Juu katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini ili iweze kupitika bila ya matatizo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Dkt. Ishengoma, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha kadri ya upatikanaji wa fedha kwenye bajeti kwa ajili ya ukarabati wa barabara. Ninaomba nichukue nafasi hii mbele ya Bunge lako Tukufu kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Morogoro na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Morogoro Vijijini kuhakikisha kwamba wanaenda kuiangalia hii barabara na kuona kama imetengewa fedha kwenye bajeti hii ambayo tumetoka kuiombea na Bunge lako Tukufu imepitisha ili kama ilitengewa fedha basi ukarabati wake uanze mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Justine Nyamoga, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kutokana na mvua zinazoendelea barabara ya kutoka Kitoho kwenda Mwatasi inayounganisha na Masisiwe kwa sasa imepata madhara makubwa na haipitiki.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha za dharura ili barabara hii iweze kupitika vizuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Nyamoga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, natoa tena maelekezo tena hapa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa Meneja wa TARURA Mkoa wa Iringa na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Kilolo kuweza kwenda kuifanyia tathmini barabara hii ya Mwatasi - Kilolo na kuona maeneo ambayo yameathirika sana ili waweze kuyafanyia kazi kwa haraka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuweza kuniona. Barabara ya kutoka Matundasi kuelekea Itumbi imeharibika sana baada ya mvua hizi ambazo zinazoendelea kunyesha.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha changarawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masache Kasaka, Mbunge wa Chunya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Matundasi mpaka Itumbi ni kweli ipo chini ukilinganisha na usawa wa barabara yenyewe na ardhi ya pembezoni, tayari katika mwaka huu wa fedha wa 2023/2024 barabara hii imeombewa fedha na ukarabati wake utaanza ili kuweza kuinyanyua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri ni lini Serikali itaanza kujenga kwa lami barabara ya Tabora Mambari ili kuunganisha Tabora Magharibi na Mashariki?

**SPIKA:** Barabara ya wapi na wapi?

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Barabara ya Tabora Mambari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Almas Maige kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hii unategemeana na upatikanaji wa fedha na tutaangalia katika bajeti hii ambayo imepitishwa ambapo ninyi Bunge hili Tukufu limeiidhinishia *TARURA* matumizi uya fedha ya zaidi ya Bilioni 830, kwa ajili ya kuweza kukarabati barabara mbalimbali nchini mwetu kwenye Majimbo yetu ikiwemo Jimbo la Mheshimiwa Almas Maige, kwa hiyo tutaliangalia na kuweza kulifanyia kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Makamu wa Rais alivyokuwa Shinyanga aliahidi barabara ya kutoka Ndala kwenda Mwawaza ambako kuna Hospitali ya Rufaa, ingetengenezwa kwa kiwango cha lami.

Ningependa kujua ni lini itaanza kutengezenzwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mnzava, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge barabara hii ni ahadi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vilevile inaunganisha

huduma muhimu kwenye jamii kama vile Hospitali hii ambayo iko hapo, hivyo basi Serikali itaipa kipaumbele na kutekeleza utekelezaji wa barabara hii kama ilivyokuwa maelekezo ya Makamu wa Rais lakini vilevile ni uhitaji mkubwa wa wananchi wa Shinyanga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 137

**Malipo ya *TASAF* mkononi badala ya simu au benki**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza: -

Je, kwa nini wanufaika wa *TASAF* wasilipwe mkononi badala ya kupewa kwa njia ya simu na benki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu Swali lililoulizwa na Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mwaka 2019 Serikali ilifanya majaribio ya mfumo wa kieletroniki wa malipo kwa walengwa katika mamlaka za utekelezaji 19. Baada ya majaribio, mwaka 2020 mfumo wa malipo kwa njia ya kielektroniki ulipitishwa rasmi na walengwa kuanza kutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakiri kutokea changamoto katika baadhi ya maeneo ya utekelezaji. Hivyo utaratibu wa malipo kwa sasa upo katika njia tatu; kwa njia ya simu, akaunti ya benki na njia ya malipo ya fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huu ni uchaguzi wa mnufaika mwenyewe atumie njia gani kadri ya mazingira yake. Aidha, naomba kutoa rai kwa Mheshimiwa Mbunge tusaidiane kuelimisha walengwa juu ya njia hizi kuu tatu za malipo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nimesikia majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali langu la kwanza, lengo la kuwapelekea hizi fedha lilikuwa ni kuwasaidia tukiamini ni masikini, kwa hiyo hawana uwezo wa kununua simu. Kwenye simu kuna makato na benki kuna makato. Hatuoni kuweka hilo jambo ni kuondoa lile lengo la kuwasaidia hawa wanufaika ambao hawawezi hata kununua simu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, mchakato wa kuwapata wanufaika uligubikwa na mambo mengi sana ikiwemo ubaguzi wa kivyama, kwa maana ya vyama vya siasa. Nini kauli ya Serikali kupitia upya tena mchakato huu ili tuwapate wenye sifa wanaostahili kuwa wanufaika wa *TASAF*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nataka nirejee tena maelezo ambayo nimeyatoa katika swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, malipo ya pesa hizi yako katika njia kuu tatu, ni *choice* ya mhusika mwenyewe njia gani aitumie. Kama akiona kwamba njia ya simu ni ngumu kwake kwa sababu hana simu hiyo inayopokea, anaweza kwenda katika njia nyingine ya benki. Kama akiona njia nyingine ya benki ni ngumu kwa sababu benki iko mbali, upo utaratibu wa kulipa fedha taslimu kupitia madirisha yetu. Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge *option* hizi zote zinawezekana katika maisha ya kawaida ya ubinadamu wetu na Watanzania wetu na mimi na Serikali tunaamini hivyo.

Mheshimiwa Spika, juu ya swali la pili la upatikanaji wa wanufaika. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba baadhi ya maeneo kumetokea changamoto juu ya utambuzi wa wanufaika katika miradi hii ya *TASAF,* Serikali imekwishayafanyia kazi katika baadhi ya maeneo na tunaendelea kutambua katika yale maeneo yenye changamoto, nataka nikuhakikishie katika Jimbo lako la Nkasi Kaskazini nako pia timu ya *TASAF* itafanya kazi, nasi tunategemea zaidi ushirikiano kutoka kwako Mheshimiwa Mbunge ili kuweka mambo ya wanufaika vizuri kwa sababu nia ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha kwamba wanufaika wote au walengwa wote wa *TASAF* wanafikiwa na kufikia malengo yao. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Wapo wanufaika waliowahi kunufaika na *TASAF* nazungumzia wazee, vikongwe ambao hawana wasaidizi walio katika Wilaya ya Korogwe, ambao wametemwa na mfumo wa *TASAF*.

Je, Serikali haioni kama imewaonea wazee wale kuwaondoa kwenye mfumo ingali bado hawawezi kujikimu maisha yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sekiboko, Mbunge wa Tanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utambuzi wa wanufaika wa *TASAF* ni utambuzi shirikishi ambao unaanza ngazi za vijiji na ngazi hiyo tunaamini kabisa kwamba kila mmoja anamtambua na kumjua mwenzake. Utambuzi ndani ya *level* ya Serikali ni *level* ya uhakiki tu. Tunachokiangalia kama Serikali ni zile taarifa ambazo zinatoka katika kijiji ambacho wahusika hawa au wanufaika wanatokea. Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge siyo nia ya Serikali kuwadhulumu watu au kuwanyima wanufaika haki yao.

Mheshimiwa Spika, natoa angalizo sana kwa Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Halmashauri zetu, kuhakikisha kwamba wanufaika wote wanaotakiwa kuingia kwenye mfumo wa *TASAF* wanaangaliwa na kutambuliwa ili Serikali iweze kufikia malengo yake ya kuwasaidia Watanzania wenye uhitaji katika mfumo huu mzima wa kunyanyua maisha ya wale ambao wanaonekana wanahitaji kuingizwa katika mfumo wa *TASAF* ili kuwawezesha kiuchumi.

**SPIKA:** Meshimiwa Waitara swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafsi.

Mheshimiwa Spika, ninataka kujua kwamba, kwenye vijiji vyetu kuna watu ambao walipaswa kuwa na sifa kupata

huduma ya *TASAF* na viongozi wengi wa vitongoji na vijiji wameweka watu ambao hawana sifa. Nini mpango wa Serikali kufanya *auditing* kuhakikisha kwamba watu wote ambao wanapaswa kuingizwa kwenye mfumo wanaingizwa na wale ambao hawapaswi kupata hiyo huduma watolewe katika huduma hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika swali lililoulizwa na Mheshimiwa Sekiboko, naomba kurudia tena mbele yako na kulieleza Bunge lako na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa utambuzi wa wanufaika wa *TASAF* ni mfumo shirikishi ambao unaanzia kwenye ngazi za vijiji vyetu, kwa hiyo ninachotegemea kutoka kwa wananchi ambao watashiriki mkutano wa utambuzi ni kuweza kuwatambua watu wote wanaotakiwa kushiriki katika mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe taarifa ndogo, tumewahi kufanya ziara katika baadhi ya Wilaya, tumekwenda pale tukakutana na kituko cha mwaka. Watu wanakataa watu walioingizwa kwenye mfumo wa *TASAF* ndiyo haya ambayo Mheshimiwa Waitara anayasema. Nataka nirudie tena mfumo huu ni mfumo shirikishi na nitoe wito kwa wananchi wote katika maeneo yote, mnapoitwa katika mikutano ya *TASAF* hebu jaribuni kushiriki ili kuondoa ubabaishaji wa baadhi ya watu ambao wanachomeka ndugu zao na watu wasio na sifa katika mfumo huu na kudhulumu wale watu wenye sifa, wanaostahili kuingia katika mfumo wa *TASAF*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nashukuru majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini zoezi zima la utambuzi katika Jimbo la Mwibara lime – *collapse*.

Je, ni lini Serikali itafanya tena zoezi hilo upya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwijage, Mbunge wa Mwibara, samahani kwa kukuchanganya majina nimekuita Mheshimiwa Mwijage badala ya Mheshimiwa Kajege. *(Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika eneo lako la Mwibara nikiri kwamba mimi kama Naibu Waziri sijapata taarifa za kina juu ya wapi tatizo lilitokea na nini kilitokea mpaka zoezi zima likasimama, lakini ninaomba nilichukue hilo jambo na baada ya kumaliza *session* hii ya maswali na majibu tukutane na Mheshimiwa Mbunge ili tuweze kujadili kwa kina tuone nini kinafanyika na wapi walikosea ili tuende tukasahihishe tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, naendelea kusisitiza tena kwamba ni nia ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba wanufaika wote wa *TASAF* tunawafikia na kuwatendea haki katika kupata wanachostahili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani kwa ujumla wake, hizi changamoto za *TASAF* kwa sababu zimeshakuwepo kwa muda mrefu, nadhani kufikia sasa zinapaswa ziwe zinapungua kuliko kuongezeka, ikiwa ni

pamoja na utambuzi na wale ambao wanastahili na njia bora za kuwafikia. Kwa sababu, kama huyu ni masikini, tena inabidi atumie nauli kwenda kufuata hiyo pesa, kidogo inakuwa mtihani. *(Makofi)*

Pia maswali ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna wengine wamo, wengine hawamo; kwa namna ambavyo Serikali imefanya vizuri kwenye mpango huu kwa sasa hivi inabidi mfanye tathmini ya kina ili zile changamoto kwa sasa ziondoke. Kwa nini? Kwa sababu tumeshafanya hii kazi kwa muda mrefu. Kama unavyosema nia ni kuwafikia wale walengwa ili wafikiwe, basi njia za utambuzi ziboreshwe ili asiachwe nje anayestahili halafu akaingia ambaye hastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kuambatana nami baada ya Bunge hili, kwenda Wilayani Nyang'hwale kuonana na akina mama wakongwe zaidi ya 80 ambao wameorodheshwa na zaidi ya miaka mitatu hawajapata stahiki yao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nipo tayari na tutaongozana ili kwenda kuwatambua na tuzungumze kwa pamoja. Siyo tu utambuzi wa hawa, lakini pia suala zima la changamoto zilizopo katika eneo lake la utawala kuhusiana na mradi wetu huu wa *TASAF*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya…

Mheshimiwa Naibu Waziri, una swali lingine bado?

*(Hapa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora alitikisa kichwa kukubali kwamba analo swali lingine la kujibu)*

**SPIKA:** Aah, basi subiri kidogo.

Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria waende wakakutane na Waziri muda huu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi Umma na Utawala Bora aende kwenye hiyo kamati ili wakashauriane jambo hivi la kibajeti, maana tunapitisha hiyo bajeti leo hapa. Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hiyo, tunaendelea na maswali lingine. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo sasa aulize swali lake.

Na. 138

**Kuifufua Tume ya Mipango**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itafufua upya Tume ya Taifa ya Mipango?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali namba 138 lililoulizwa na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za mwisho za maandalizi ya Muswada wa Sheria kuanzisha Tume ya Mipango. Muswada huu unatarajiwa kuwasilishwa Bungeni katika Mkutano huu wa Kumi na Moja wa Bunge lako unaoendelea sasa. Muswada wa Sheria ukipitishwa Bungeni, Tume ya Mipango inatarajiwa kuanza shughuli zake katika mwaka wa fedha 2023/2024 yaani tarehe 1 Julai, 2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kweli nafarijika kwamba sina swali la nyongeza. Ninaishukuru tu Serikali kwa hatua hii muhimu ya kuleta Muswada huu, nasi kama Wabunge tutautendea haki ili Tume hii ya Mipango ambayo ndiyo itatupa dira nzuri ya maendeleo ya nchi yetu iweze kuwepo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Shamsia Aziz Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo.

Na. 139

**Ujenzi wa barabara ya Iyari hadi Mkunwa – Mtwara Vijijini**

**MHE. TUNZA I. MALAPO K.n.y. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara ya Iyari hadi Mkunwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania imepanga kujenga kilometa 2.2 katika barabara ya Iyari – Mkunwa (kilometa 79) kwa kiwango cha lami na mkandarasi yupo anaendelea na ujenzi ambapo kazi zinatarajiwa kukamilika Juni, 2023. Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha hadi kuikamilisha yote, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Barabara hiyo ndiyo inaelekea Makao Makuu ya Halmashauri. Kwa kujenga kilometa mbili kwa mwaka

barabara ya kilometa 79; je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi kabisa wa kuimaliza barabara hii kwa wakati kwa kuzingatia umuhimu wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili. Nataka Serikali inieleze kwa dhati ya moyo kabisa, inamaliza lini Barabara ya kutoka Mtwara Mjini kupita Tandahimba – Newala mpaka Masasi ile ya kilometa 210? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii kweli ni ndefu na inaenda kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Ndiyo maana tumeshaifanyia usanifu, lakini kadiri fedha inavyopatikana tumeona tuanze kuijenga wakati tunatafuta fedha ya kuijenga yote kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, dhamira ipo ndiyo maana tumeanza.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili, barabara ya kilometa 210 ya kutoka Mtwara – Mnivata – Newala hadi Masasi, Serikali imeshaanza kuijenga; kilometa 50 kutoka Mtwara hadi Mnivata, na sasa hivi tuko kwenye maandalizi ya kuanza kuijenga barabara yote kuanzia Mnivata hadi Masasi. Tumegawa *lots* mbili, kwa wahisani ya wenzetu wa *African Development Bank* ambao wanafadhili hiyo barabara, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itatenga fedha za kutosha kwa ajili ya kujenga barabara ya Ramadhani – Iyai, Mkoani Njombe ambayo iko kwenye Ilani ya CCM kwa zaidi ya miaka 15?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii barabara ya Ramadhani – Iyai tumeshaanza kuijenga kwa awamu. Mwaka huu nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeitengea pia fedha kwa ajili ya kuendelea kuijenga. Matazamio ya Serikali ni kuikamilisha barabara yote hii kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zainab katimba, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Kakonko – Kinonko – Guarama mpaka mpaka wa Muhange, ambayo ni barabara itakayounganisha Tanzania na Gitega, ambayo ni Makao Makuu mpya ya Burundi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zainab Katimba, Mbunge Viti Maalum, Kigoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kuanzia Kakonko hadi Muhange ni kweli inaunganisha Tanzania na Burundi na sasa

hivi Makao Makuu yao yamesogea Gitega. Ilikuwa haijafanyiwa usanifu, lakini tutakamilisha usanifu ikiwa ni maandalizi kwa kuijenga barabara hii yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariki, Mbunge wa Viti Maalum, Katavi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ilishatolewa ahadi na ipo kwenye Ilani. Naomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, tuone bajeti tutakayopitisha, naamini kuna mapendekezo ya kuanza kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami, kuunganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Tabora, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Karera – Munzeze – Janda hadi Buhigwe, kilometa 72 kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kavejuru, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Karera – Muzenze hadi Buhigwe tayari ipo kwenye kukamilishwa kufanyiwa usanifu barabara yote ikiwa ni maandalizi kuijenga kwa kiwango cha lami. Tayari ipo kwenye usanifu na tupo kwenye hatua za mwisho, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Lyazumbi inayounganisha Mkoa wa Rukwa na Katavi kupitia Mbuga ya Wanyama Katavi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara hii ni barabara kuu, lakini kabla ya kuijenga hiyo barabara, ndiyo maana tumeamua kuijenga kwanza barabara ya Kizi – Kibaoni, Kibaoni kwenda Stalike. Kwa sababu hizo barabara zitakuwa zinakwenda *parallel,* baada ya kukamilisha, ndiyo sasa tutahamia pia kwenye hiyo barabara ambayo inapita katikati ya mbuga, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo, swali la nyongeza.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya lami kutoka *Airport* kwenda Nyanguge yenye kilometa 47? Kwa sababu, upembuzi yakinifu umeshafanyika na barabara hii ni *Bypass* ya kupita Serengeti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Furaha Matondo, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mwanza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni moja ya barabara ya *Bypass* katika Mkoa wa Mwanza, *Airport* – Igombe – Kayenze hadi Nyanguge. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira, tuone bajeti hii tutakuwa tumepanga nini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujua kwenye mwaka uliopita, katika bajeti Naibu Waziri, aliahidi kujenga barabara ya Bariri – Mgeta; je, sasa iko kwenye bajeti inayokuja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, barabara hii amekuwa anaifuatilia; na kwa kuwa bado hatujapitisha bajeti, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tuone kama hii barabara tumeshaipangia bajeti. Mpango wa Serikali ni kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini barabara ya kilometa tano ya kutoka Kinyanambo C – Mapanda mpaka Kisusa, Jimbo la Mufindi Kaskazini, itajengwa? Kwa sababu hii barabara inafungua uchumi wa Mufindi Kaskazini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge Viti Maalum, Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii aliyoitaja ni kweli inafungua uchumi, lakini ujenzi wake pia utategemea na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kadiri fedha zitakavyokuwa zinapatikana, barabara hii itajengwa yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, barabara inayoanzia Wilaya ya Rorya inapita Susuni – Sirari – Mbogi – Nyansincha mpaka Nyanungu ni barabara ya kiusalama ambayo iko mpakani.

Nilitaka kujua barabara hii ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuweza kuimarisha usalama katika mpaka wa Tanzania na Kenya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri barabara hii kabla ya kuja Bungeni nimeipitia yote, na ikiwa ina mahitaji makubwa sana pia ya Mkoa wa Mara kwa maana ya usalama. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inaifanyia kazi kuhakikisha kwamba hii barabara inaimarishwa na kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga.

Na. 140

**Ujenzi wa barabara ya *bypass* Kisaki hadi Unyambwa**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA K.n.y. MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya mchepuko kutoka Kisaki – Unyamikumbi - Unyambwa hadi Mtipa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imekamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa kina wa barabara ya

mchepuko katika Mji wa Singida *(Singida Bypass)* kutoka Kisaki – Unyamikumbi – Unyambwa hadi Mtipa yenye urefu wa kilometa 46. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Manispaa ya Singida ipo katikati ya nchi na malori kutoka upande wa nchi yanapita pale; je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuwahisha ujenzi wa *bypass* hii ili kuondoa msongamano unaokua kwa kasi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Wakati wenzetu wanaongelea *Bypass,* Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama haina hata mita moja ya lami; na kwa kuwa, upembuzi yakinifu wa barabara ya Simiyu – Singida umekamilika: Serikali haioni haja katika bajeti hii kutenga walau kilometa 20 Makao Makuu ya Halmashauri ya Mkalama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Francis Mtinga, Mbunge wa Mkalama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Singida kuna *traffic* kubwa. Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba tumekamilisha mwaka 2022 kufanya usanifu na tunavyoongea sasa hivi, tayari tumeshafanya tathmini ya wale watakaofidiwa kupisha barabara; na Serikali inaandaa

malipo kwa ajili ya kuwafidia hawa watu watakaopisha barabara. Kwa hiyo, tunataka tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Singida kwamba, Serikali imedhamiria kwa dhati kujenga hiyo *bypass*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunatambua kwamba barabara aliyoitaja ni muhimu sana ambayo pia ni kutoka Singida kwenda Sibiti hadi Bariadi. Naomba pia, avute Subira, tuone kwenye bajeti hii inayokuja tumetenga nini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. *(Makofi)*

Wizara ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 141

**Hitaji la mawasiliano ya simu Kata za Mbinga Mjini**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Minara ya simu katika Kata za Kikolo, Mbangamao, Kitanda na Kagugu - Mbinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma ya mawasiliano nchi nzima. Aidha, kupitia mradi wa Tanzania ya Kidijitali, Kata ya Kitanda imejumuishwa katika utekelezaji wa mradi huo ambapo utekelezaji wake umeanza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa upande wa kata zilizowasilishwa kuwa na changamoto ya mawasiliano ambazo ni Kata za Kikolo, Mbangamao na Kagugu, zitafanyiwa tathmini na kuchukua hatua stahiki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naishukuru Serikali kwa kuanza kutekeleza mradi wa kujenga mnara katika Kata ya Kitanda, kupitia mradi wa Tanzania ya Kidigitali. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Serikali imetoa maelezo kwamba, Kata za Kikolo, Mbangamao na Kagugu zitafanyiwa tathmini; na maeneo hayo watu wakati mwingine wanapanda kwenye miti kutafuta mawasiliano: Nataka nijue sasa ni lini tathmini hiyo itaanza kufanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika Kata ya Mpepai ulijengwa mnara ambao unaendeshwa na Kampuni ya *Airtel,* na wakati mwingine kunakuwa na changamoto ya mawasiliano, mtandao huwa haupatikani. Ninataka nijue ni lini sasa Serikali itafanya marekebisho katika eneo hilo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa fedha kwa ajili ya kufanya tathmini katika vijiji 2,116. Na katika upande wa Mbinga, Vijiji vya Luanda, Muhongozi, Matili na Kitanda zilifanyiwa tathmini hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini katika mwaka wa fedha huu wa 2023/2024, Kata za Kikolo na Kagugu zitaingizwa katika utaratibu wa kufanyiwa tathmini na baada ya hapo fedha zitakapopatikana zitaweza kufikishiwa huduma ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa kipengele cha pili kuhusu mnara wa *Airtel* uliopo katika Kata ya Mpepai; changamoto ya mnara huu ni kwamba unatumia nguvu ya jua *(solar energy)* na tumeshakubaliana na watoa huduma kufanya mambo mawili yafuatayo; la kwanza ni kwamba pale ambapo umeme wa Gridi ya Taifa umeshafika wafanye juhudi za kuhakikisha kwamba wanaunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, na pale ambapo umeme wa Gridi ya Taifa haujafika basi wahakikishe kwamba wanaweka jenereta ili iwe njia mbadala pale ambapo *solar* inakuwa imezidiwa. Na hayo tayari tumeshakubaliana na hatua zimeshaanza kuchukuliwa, ni pamoja na katika eneo hili ambalo Mheshimiwa Mbunge amelitaja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kata za Kijirishi na Nyaruhande, Wilaya ya Busega, kuna changamoto sana ya mawasiliano ya simu.

Je, ni lini Serikali itajenga minara ya simu katika kata hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Midimu, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Simiyu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo amelitaja Mheshimiwa Esther Midimu ni katika vijiji 2,116 ambavyo tayari vimeshafanyiwa tathmini. Hivyo, Serikali iko katika mchakato wa kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunafikisha mawasiliano katika maeneo hayo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. nilikuwa nimeomba kuuliza swali la nyongeza kwenye Wizara ya Kilimo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Wilaya ya Ngorongoro bado ina changamoto kubwa ya mawasiliano, na Mheshimiwa Naibu Waziri analifahamu hili suala vizuri.

Je, ni lini sasa mnara wa Simu wa Jema utawashwa ili basi wananchi wa Oldonyosambu na maeneo jirani waweze kupata mawasiliano ya kutosha? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zaytun Swai kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Zaytun alishalifikisha jambo hili katika Wizara yetu na tayari tumeshachukua hatua. Jambo ambalo linafanyika sasa hivi ni *technical audit* na ikishakamilika mnara utawashwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kuna changamoto ya mawasiliano kwenye Kata za Makanya, Malibwi, Kwai na maeneo mengine katika Jimbo la Lushoto: -

Je, ni lini mawasiliano yatapelekwa katika kata hizo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shabani Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba inafikisha huduma ya mawasiliano nchini kote na tunakwenda kwa awamu. Hivyo, nalipokea ili wataalam wetu waende wakafanye tathmini katika maeneo hayo na tujiridhishe changamoto yenyewe iko katika upande upi ili tuweze kuchukua hatua stahiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri Wabunge wengi wamesimama. Haya maneno 'kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri' yale unaachana nayo. Mbunge akishauliza tu swali wewe nenda moja kwa moja kwa sababu kusimama tu hapo ulishasema uko kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Michael Mwakamo, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka wakandarasi kwenye Vijiji vya Bokomnemera, Kimalamisale na Mpiji ambapo wana shida ya mawasiliano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwakamo tayari ameshalifikisha jambo hili na tulishaongea na tayari hatua zimeshaanza kuchukuliwa ili kufikisha huduma ya mawasiliano katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa na ya muda mrefu ya mawasiliano katika Mapori ya Kasindaga na Kimisi Mkoa wa Kagera: -

Je, ni lini Serikali itamaliza matatizo hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Conchesta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba nipokee changamoto hii ili tukaifanyie kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, viko Vijiji vya Mtawatawa, Ndapata, Ndunyungu na Ndinda, ambavyo havina mawasiliano kabisa. Ni lini Serikali itaona umuhimu wa kupeleka mawasiliano kwenye vijiji hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, wataalam wetu wameshafika katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, na tayari katika orodha ya vijiji 2,116 tukitoka hapa Mheshimiwa Kuchauka tuonane ili niweze kukuonesha maeneo ambayo tayari umeyataja, yamo tayari kwenye utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Katika Jimbo la Bagamoyo, Kata ya Magomeni,

maeneo ya Sanzale, Kata ya Makurunge, Kamata ya Fukayosi maeneo ya Kijiji cha Mkenge, hakuna kabisa mawasiliano, ni ya shida sana. Ni lini sasa Serikali itapeleka wataalam kule kwenda kuweka minara mawasiliano yapatikane?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Muharamu, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo: -

**SPIKA:** Anaitwa Mheshimiwa Muharami Mkenge.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kumlazi.

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu kama ifuatavyo; kama ambavyo nimesema kwamba tulianza na vijiji 2,116 ambapo ni katika mwaka wa fedha 2022/2023 na sasa katika awamu inayofwatia ambayo ni 2023/2024 vijiji na kata za Jimbo la Bagamoyo zitaingizwa katika utaratibu wa kufanyiwa tathmini na baadaye Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kwenda kufikisha huduma ya mawasiliano, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Wabunge wengi wamesimama na wewe umeshajibu maswali mengi sana hapo mbele, hebu watazame kidogo. Hebu simameni Waheshimiwa Wabunge wenye maswali kuhusu minara. Ehee, hebu watazame kidogo. Ulishawaona?

Sasa alikuwa amesema kuna Wabunge ambao amewajibu kwamba wamuone baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu, kwa hiyo, Wabunge wote ambao mna maswali kuhusu minara, ameshajibu maswali mengi sana.

mtakwenda muonane na Mheshimiwa Naibu Waziri ili awaeleze katika maeneo yenu watafika lini. *(Makofi)*

Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa tunaelekea Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, sasa aulize swali lake.

Na. 142

**Uhitaji wa umeme wa REA Kijiji cha Ikombe – Kyela**

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA** aliuliza: -

Je, ni lini umeme wa *REA* utafika katika Kijiji cha Ikombe – Kyela?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, kama Ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Ikombe kitapata huduma ya umeme kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili unaotekelezwa na Mkandarasi *M/s ETDCO Ltd.* Kazi ya ujenzi wa miundombinu ya umeme katika Kijiji cha Ikombe kutoka Kijiji cha Lyulilo inatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2023 na inatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mlaghila, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY A. J. MLAGHILA:** Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Ikombe ni kijiji ambacho kiko pembezoni sana na ni kisiwa ambacho hakifikiwi kirahisi. Leo hii tunapouliza hili swali wananchi wa Ikombe wamewatuma viongozi wao waje washuhudie majibu haya ya Serikali, wako hapa leo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *ETDCO* ambao wanasambaza umeme wa *REA* walianza kazi hii Agosti, 2021 na wamefikia vijiji 21 tu na vijiji vilivyobaki ni 14. Na katika vijiji hivyo 14 bado hata nyaya hazijavutwa wala hakujatokea uwezekano wa kupeleka nguzo na mkataba unaisha ndani ya siku kumi zijazo, swali la kwanza: -

Je, sasa Serikali haioni umuhimu mkubwa wa kushirikiana na *TANESCO* ili kwa Kyela vijiji hivyo viishe mapema?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ni maajabu gani yatatokea kufanikisha ndani ya siku kumi mkataba huu uendelee ufike mpaka watakapofikisha hapo Juni pale Ikombe? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa *spirit* ya kutotaja kumuwakilisha Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya muda naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu mawali ya nyongeza la Mheshimiwa Ally Anyigulile kwa ujumla wake kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kuna mikataba ambayo muda wake utaisha kabla kazi hazijakamilika, lakini nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata

umeme. Na tunachokifanya ni kukabana na wakandarasi wote wanaopeleka miradi yetu ya umeme kwenye maeneo mbalimbali kuhakikisha wanamaliza kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lakini sababu nyingine moja inayofanya kazi izidi muda wa mkataba wa awali ni kuongezeka kwa hizo kilometa mbili ambazo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa pesa ya nyongeza kwa ajili ya kuongeza *scope*. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Ally kwamba kama tulivyosema kabla ya mwezi Juni hicho kijiji kitakuwa kimepata umeme na wananchi wataweza kuutumia katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, na kwa mkandarasi *ETDCO* yupo zaidi ya asilimia 60 na vijiji 14 vilivyobaki vitakamilika katika huu muda ambao tumejipangia kwa spidi mpya ambayo tuko nayo kwa sasa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollol, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka au kusambaza umeme kwenye vijiji na vitongoji katika Jimbo la Arumeru Magharibi ambayo imekuwa ni changamoto sana wananchi kupata umeme? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Noah Saputi, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kama lfuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, upo mradi ambao unaendelea wa upelekaji wa umeme katika vijiji wa *REA III Round Two* ambao

pia unahusika katika kufikisha umeme kwenye vitongji. Lakini muda si mrefu tutaanza Mradi mwingine unaitwa *Densification IIC* ambao una takribani vitongoji 2,600, nao ni kwa ajili ya kupeleka umeme katika vitongoji.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ambavyo tumekuwa tukisema, tunatafuta pesa kwa ajili ya upelekaji wa umeme katika vitongoji vyote 36,000, takribani trilioni sita na bilioni mia tano ili kumaliza tatizo lolote la umeme. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba kwenye vile vijiji vilivyopo kwenye mradi kabla ya Desemba mwaka huu vitaisha na pesa nyingine itatafutwa kufikisha katika maeneo mengine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo kubwa la kukatikakatika kwa umeme Wilayani Urambo, Serikali inasema nini kuhusu kumaliza ujenzi wa Kituo cha Uhuru ambacho kitakuwa ukombozi kwetu sisi? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge wa Urambo, kama Ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Kupoza Umeme cha Uhuru kilichopo katika Jimbo la Urambo kinatekelezwa katika mradi tunaouita Mradi wa Gridi Imara ambao unapokea umeme wa kilovoti 33 kutoka Tabora Mjini na mkandarasi tayari ameshapatikana ameshaagiza vifaa, na kabla ya katikati ya mwaka unaokuja tunatarajia Mradi huu wa Gridi

Imara utakuwa umekamilika katika maeneo mengi likiwemo eneo la Kituo chetu cha Kupooza Umeme cha Uhuru kwa ajili ya kuhudumia wananchi walioko hapo na kupeleka Gridi ya umeme mpaka katika Wilaya ya Uvinza kupitia pale Uhuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika Jimbo la Bunda Mjini, hasa kata saba za vijijini, kumekuwa na changamoto ya umeme kutofika kwenye nyumba za wananchi, unaishia senta: -

Je, ni lini sasa mtapeleka nguzo za kutosha ili ile dhana ya umeme vijijini iwe imekamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya kama Ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hii miradi ambayo tunaitekeleza inalenga kumfikia kila mwananchi. Lakini kwa sababu ya bajeti tuliyokuwa nayo na fedha ambayo haitoshelezi kwa wakati huu kwa maeneo yote, *advancement* inakwenda taratibu.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mradi wetu wa ku-*electrify* vitongoji vyote ambapo tunatafuta trilioni sita na bilioni mia tano, tunaamini kwamba kila mtu atafikiwa na umeme na katika miaka mitatu, minne, mitano ijayo, hakutakuwa kuna mwananchi katika kitongoji au eneo lolote ambaye hana umeme kwa sababu hiyo ndiyo azma ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rose Busiga, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali la nyongeza: -

Ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata ya Ng'homolwa, Kijiji cha Nkweni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rose Busiga, Mbunge wa Viti Maalum Geita, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba naamini kijiji hicho na kata hiyo ipo katika mradi wetu wa *REA III Round Two,* na kabla ya mwaka huu kuisha kijiji hicho kitakuwa pia kimepata umeme kwenye baadhi ya vitongoji na sasa maendeleo yataendelea kwenye vitongoji ambavyo vitakuwa vimebaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Licha ya wananchi wa Kata ya Kibale, Kijiji cha Kigorogoro, lakini pia Businde na Lukuraijo Mkombozi kukatiwa migomba na mikahawa kwa ajili ya kuwekewa nguzo za umeme, ni zaidi ya mwaka mmoja hawajapatiwa umeme; ni lini wananchi hao watapatiwa umeme? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum Kagera, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mkandarasi anayepeleka umeme katika Mkoa wa Kagera anaitwa JV Pomina Kwihaya, na

yuko kazini anaendelea. Ni kweli alisuasua, katika wale wakandarasi saba ambao tulikuwa tunaona *progress* zao siyo nzuri na yeye alikuwemo. Lakini tumeweka *strategy* mpya na ninaamini Waheshimiwa Wabunge wengi wameona tumaenzisha ma-*group* ya *whatsApp* kwa ajili ya kupata *updates* za kila siku.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla ya mwaka huu kuisha umeme utakuwa umefika katika maeneo hayo kwa sababu ndiyo makubaliano yetu sisi na wakandarasi wote wanaopeleka umeme katika maeneo ya vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

Ni lini wananchi wangu wa Kata za Pangale, Mpombwe, Tutuo, Sikonge, Mkolye hadi Ipole watapata fidia ambayo wamepisha njia ya kupita umeme?

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Kakunda, hilo swali lako linahusu fidia. Mheshimiwa Waziri, unao uhuru kama unayo majibu ya kuhusu fidia mpe jibu lake, kama huna ataleta swali lake la msingi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inajenga laini ya kilovoti 33 ya kupeleka Gridi ya Taifa Katavi ambapo inatokea Kituo chetu cha Tabora inapita Ipole ambako ndiko katika jimbo lake, inakwenda Inyonga na baadaye inafika Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Spika, laini yote hiyo ina jumla ya kilometa 380 na pesa zimeshapatikana kwa ajili ya kulipa fidia, na mkandarasi anaingia *site* karibia kwenye mwezi Julai au Agosti. Kabla ya muda huo fidia itakuwa tayari imelipwa ili Gridi ya Taifa iweze kufika Katavi na wananchi wake wataweza kulipwa fidia ambayo wanastahili kupewa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kawekapina, Ipululu na Vumilia Kata ya Igalula wanacheleweshewa kupata umeme kwa sababu ya mgogoro wa *TANESCO, TRC* na *REA*:-

Je, ni lini mtaumaliza mgogoro huu wa kuvusha nyaya kwenda kwenye vijiji hivyo ili wananchi wapate umeme kwa wakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Venant, Mbunge wa Igalula, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* na *REA* wako tayari na wanayo fedha kwa ajili ya kuvusha umeme kwenye *line* ya *SGR* lakini wenzetu wa Wizara ya Uchukuzi walikuwa hawajajua eneo gani watuoneshe kwa ajili ya kupitisha njia na sisi tusingependa tutumie pesa nyingi kupisha eneo *temporary* halafu baadae kidogo tuhamishie kwingine. Tumekaa pamoja na wenzetu wa *TRC* watatuonesha sehemu ambayo ni ya kudumu tutakayopitisha miundo mbinu hiyo ili wananchi waweze kupata umeme katika maeneo hayo. Kwa hiyo nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba

tunalifatilia na tutalikamilisha kwa wakati ili wananchi waweze kupata huduma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Kilimo Mheshimiwa Shally Josepha Raymond Mbunge wa Viti Maalum sasa swali lake linaweza kuulizwa.

Na. 143

**Kuhusu ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga Mabwawa ya kuvuna maji ya Mvua pamoja na mifereji ya umwagiliaji ili kupunguza athari za mvua katika Mkoa wa Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kilimanjaro ni miongoni mwa mikoa ambayo ujenzi wa mabwawa kwa ajili ya kuvuna maji ya mvua pamoja na ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji umeendelea ili kupunguza athari za mvua na kusaidia wakulima kujihakikishia kilimo cha mwaka mzima kupitia umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika**,** Katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha mapitio ya usanifu wa ukarabati wa Bwawa la

Ikuini na taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa bwawa hilo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bwawa la Boloti na Yongoma sambamba na mifereji itakayoweza kuhudumia takribani hekta 2,000 ndani ya Wilaya ya Same.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Swali la kwanza, kwa kuwa katika majibu ya msingi ameitaja Boloti ambayo iko Siha na Ikuini ambayo iko Rombo tu; lakini kwenye swali langu niliuliza tambarare yote ya Mkoa wa Kilimanjaro. Sasa, ni lini wataweza kujenga mabwawa hayo Undugai katika Wilaya ya Hai, Arusha chini kule Chekereni Wilaya ya Moshi Vijijini na Kahe na kule Mwanga ikiweko na Ruvu kule Same?

Mhehimiwa Spika, swali la pili; ni lini mabwawa hayo yanayojengwa na yanayotarajiwa kukarabatiwa yatatumika kufundishia wananchi kutumia *drip irrigation* ambayo ni umwagiliaji wa matone ili uweze kuwa na tija kwa mazao ambayo yatakuwa yameoteshwa wakati wa ukame?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha maeneo yote yanayofaa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa tuweze kuyafanyia kazi ili wananchi wetu waweze kulima mwaka mzima, ni muondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti yetu ambayo tutakuja kuisoma hapa

tumeitengea eneo hili fedha za kutosha kuhakikisha kwamba tunapitia maeneo yote ikiwemo Mkoa wa Kilimanjaro katika maeneo ambayo ameyataja.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, teknolojia ya umwagiliaji wa matone ni kati ya teknolojia ambayo inatumika katika maeneo mengi sana hivi sasa nchini, na sisi kama Wizara ya Kilimo tunaiunga mkono. Isipokuwa tu katika Mabwawa ambayo ameyatamka teknolojia hii huwa inaendana na aina ya mazao yanayolimwa. Kwa hiyo kama mazao yanayolimwa yatakuwa yanahitaji teknolojia hii tumeshaanza, na ukienda katika Bwawa letu la Chinangali hapa Dodoma tayari kuna umwagiliaji wa matone katika zao la Mzabibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtega, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS L. MTEGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mabwawa sita Wilayani Mbarali ili kuboresha kilimo cha mpunga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika miradi yetu yote sita iliyoko Mbarali tumemaliza taratibu zote na miradi mingine wakandarasi tayari wako *site*. Miradi kama ya Utuo, Isenyera, Gonakuvagogoro, Helmanichosi yote yana mkandarasi na kazi inaendelea. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imedhamiria kujenga miradi hiyo na kazi inaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, swali la nyongeza.

**MHE. DAVID M. KIHENZILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kuna changamoto kubwa sana kwenye ukanda wa joto wa Mufundi kwenye zile kata Saba nadhani unazifahamu Mheshimiwa Naibu Waziri, Nyororo, Maduma, mbalamaziwa, Ihoanza, Itandula pamoja na Idunda;

Je, ni lini sasa Serikali watatuletea *scheme* za umwagiliaji ili wananchi wa pale waweze kulima kipindi chote?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika,napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja kati ya kazi kubwa ambayo tutaifanya katika mwaka wa fedha ujao ni kuhakikisha *scheme* zote za umwagiliaji tunazozijenga zinakuwa na chanzo cha maji ili wakulima waweze kulima mwaka mzima. Mheshimiwa Mbunge katika bajeti inayokuja maeneo uliyo yataja tutachimba mabwawa kwa ajili kuanza *scheme* za umwagiliaji ili wananchi wetu waweze kulima mwaka mzima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aleksia Asia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Mkoa wa Morogoro kuna maeneo mengi yana maji ya kutosha;

Je ni lini sasa Serikali itajenga *scheme* ya umwagiliaji katika maeneo ya Mvomero na maeneo ya Mofu katika Halmashauri ya Mlimba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mkoa wa Morogoro una maeneo mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na tunayo miradi mingi ambayo inaendelea. Maeneo ambayo ameyataja nayachukulia kwa uzito mkubwa na hivyo nitaagiza wataalam wangu waende kuyaangalia, ili kama yanafaa basi tuyaingize katika mpango wetu ili kuhakikisha kwamba wakulima wanalima kupitia kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, swali la nyongeza.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kwa kuwa Serikali ilikuja kujenga miundo mbinu ya umwagiliaji kwenye bwawa kwenye Bonde la Bigombo liliko Ngara mwaka 2013 na kwa kuwa Serikali ilitelekeza bwawa hilo na miundombinu yake mwaka huo huo wa 2013;

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuja kujenga lile bwawa na kulikamilisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimesikia kilio cha Mheshimiwa Mbunge juu ya mradi wa *scheme* ya Bigombo ambayo ameutaja. Namwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na timu yake nzima kwenda kuliangalia bwawa hilo na *scheme* hiyo ili kujua changamoto iliyopo tuweze kuitatua. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, timu yangu itaelekea huko kwenda kuangalia,

lengo letu ni kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanafanya kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA ALLY MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza;

Je, ni nini mpango au Mkakati wa Serikali kujenga *scheme* ya umwagiliaji katika ukanda ule wa *delta* kule kwetu Kibiti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha tunayatumia mabonde yote makubwa nchini kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Tarehe 30 mwezi wa tatu mwaka 2023 mbele ya Mheshimiwa Rais, wakandarasi 22 walisaini mkataba wa mabonde yote ya kimkakati likiwemo bonde la Rufiji, Mto Ngono, Mto Manongawembele, Ziwa Victoria, Mto Luhuhu, Mto Songwe, Mto Ruvuma, Ifakara Idete na mpaka Litumbandio kwa Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi. Mradi wa umwagiliaji wa Arusha chini upo katika bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu lakini hadi sasa kazi hiyo haijafanywa. Je, ni lini kazi hiyo itafanyika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema ipo miradi ambayo tuko hatua za mwisho za manunuzi ikiwemo mradi huo. Kwa hiyo nimwondoe hofu kwamba ilikuwa imeshapangwa na itatekelezwa kama ilivyopangwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Swali langu nilikuwa nataka kujua, Serikali itueleze kiujumla imejipangaje kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kimkakati kitaifa katika mabonde yale ya kimkakati kitaifa yakiwemo na mabonde ya Namtumbo katika Bonde la Mwangaza, Liyuni, Likonde, Kitanda, Lusewa, Amani, Namahoka na Nambecha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimetoka kusema hivi sasa, kwamba Serikali tunayo dhamira ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba tunayatumia mabonde yote ya kimkakati katika kilimo cha umwagiliaji ili kuwawezesha wananchi wetu kulima mwaka mzima na zaidi ya mara mbili katika mwaka na maeneo ambayo ameyataja ni katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, eneo la Namtumbo pia tumeliweka katika mkakati wetu lakini kwa hivi sasa katika Mkoa wa Ruvuma tayari tunalo Bonde la Mto Luhuhu ambapo pale tuna zaidi ya hekta 3700; ambayo tumeanza kuyafanyia kazi, pamoja pia na bonde la Mto Ruvuma. Kwa hiyo sehemu ya Namtumbo ambao ameitaja Mheshimiwa Mbunge

tutakwenda kuyapitia ili kuona, kama yanafaa tutayaingiza katika utaratibu wa kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Simon Fiyao, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi; nataka kujua ni lini *scheme* ya umwagiliaji itajengwa Makwale Wilayani Kyera?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, *scheme* ya Makwale Wilayani Kyera ni moja kati ya *scheme* muhimu sana kwa wakulima wa Wilaya ya Kyera. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge, kwamba tarehe 25/4/2023 tunakwenda kusaini mkataba na mkandarasi na kazi itaanza mapema kwa ajili ya ujenzi wa *scheme* hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, *scheme* ya umwagiliaji ya Mkoka ni moja ya *scheme* ambazo zimeharibiwa na mvua zilizokuwa zinaendela na hivyo kuleta kero kwa wakulima; Mheshimiwa Waziri unatusaidiaje kwa ghafla au kwa dharula?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika,napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nitaelekeza timu yangu ya wataalam kuangalia athari iliyojitokeza na tuweze kukarabati *scheme* hiyo ili wananchi waendelee na kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nadhani tukubaliane Mheshimiwa Naibu Waziri amaejibu maswali mengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Tamima Haji Abbas Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na.144

**Sababu ya uwepo wa watoto wa mitaani**

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza: -

Je, kuna utafiti uliofanywa na Serikali kujua sababu za uwepo wa Watoto wa mitaani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wananwake na Makundi Maalum napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017/2018 ilifanya tafiti katika Mikoa ya Dar es salaam, Mwanza, Dodoma, Mbeya,

Arusha na Iringa ili kubaini idadi na sababu za watoto kuishi na kufanya kazi mitaani ambapo walibainiwa jumla ya Watoto 6,393 (wavulana 4,865, wasichana 1,528). Vilevile, mwaka 2020/2021 Serikali ilirudia utafiti katika maeneo hayo na kubaini kuwa idadi ilipungua hadi watoto 4,383 (wavulana 3,508 wasichana 875).

Mheshimiwa Spika,miongoni mwa sababu zilizobainiwa ni pamoja na, malezi duni, yatima, migogoro kwenye familia, shinikizo la makundi rika, ukatili na unyanyasaji nyumbani, umasikini wa kipato katika familia na utumikishaji wa watoto mijini, ahsante.

**SPIKA:**Ahsante sana. Mheshimiwa Tamima Haji Abbas swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; baada ya kutambua sababu za uwepo wa watoto hao, Je, Serikali ina mpango gani? Swali la pili kwa kuwa mikoa iliyofanyiwa utafiti huo ni michache; Je, Serikali ina mpango wa kuendelea na utafiti kama huo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika,napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tamima kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na mikakati endelevu kutoa malezi bora kwa wazazi na mafunzo ili kuwatunza watoto katika ngazio ya familia lakini itafanya iwakutanishe watoto hao na wazazi wao. Watoto wasio na wazazi watapata huduma na haki zote stahiki katika vituo vyetu vya watoto tunavyolelea watoto yaani, Kikombo –

Dodoma na Kurasini – Dar es Salaam lakini pia tutaimarisha ulinzi na usalama kwa watoto hao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, Serikali itaendelea kufanya tafiti mbalimbali katika mikoa ambayo inachangamoto za mitaani ili kuhakikisha usalama wao. Lakini pia nitoe rai kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanakaa na familia yao familia za watoto wao ili kuhakikisha wanapata malezi bora. Pia mtoto wa mwenzio ni wako, na watoto wote wanastahili kupewa haki muhimu kwa vile mtoto wa leo ni Taifa la kesho, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:**Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu lakini majibu kutoka upande wa Serikali. Ninayo matangazo machache, Waheshimiwa Wabunge mnao zungumza tusikilizane; Waheshimiwa Wabunge mnao zungumza tusikilizane. Mheshimiwa Kundo na wenzako hapo tusikilizane.

Waheshimiwa Wabunge tutaanza na matangazo ya Wageni, kwanza ni Wageni walioko jukwaa la Spika, hawa ni Wageni 18 wa Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kutoka nchini Kenya. Tunaanza na ndugu Christine Kwenda ambaye ni *First Counselor, Kenya High Commission* Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Geoffrey Kaituko ambaye ni *Principal Secretary, State Department for Labour and Skills Development*, yupo pia ndugu Edith Okoki ambaye ni *Acting Director General* wa *National Employment Authority,* yupo pia ndugu Hellen Apiyo ambaye ni *Acting Commissioner of Labour*, yupo pia Doctor Musa Nyandusi ambaye ni *Secretary*

*Occupational Safety and Health Services*, yupo pia ndugu Jane Wanjiru Kamau *Director of Industrial Training, NITA*, yupo pia ndugu David Mwangangi ambaye ni *Acting Managing Trustee, NSSF Kenya*, yupo pia ndugu Angela Mbaya ambaye ni *Deputy Director, Labour Migration Services, National Employment Authority NEA* na hawa wameambatana na wenyeji wao ambao ni watendaji Waandamizi kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu wakiongozwa na ndugu Joseph Nganga, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia Wageni mbalimbali ambao ni Wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni Mgeni wa Mheshimiwa Saimon Songe ambaye ni Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa *CCM* Taifa kutoka Mkoa wa Morogoro, ndugu Sheilla Lukuba, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni sita wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambao ni Viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Kijiji cha Mwaoga Mkoa wa Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Ally Mlaghila ambaye ni mtoto wake, na huyu ni ndugu Mtemi Mlaghila na viongozi saba wa *CCM* kata kutoka Jimbo la Kyera Mkoani Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Kamonga ambao ni ndugu zake kutoka Dar ES Salaam kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Jacline Kainja ambao ni wadogo zake kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni wajumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Kilolo Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Kembaki ambaye ni Katibu wa CCM Kata ya Turwa Tarime Mkoa wa Mara ndugu Julius Mwita, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 13 wa Mheshimiwa Emmanuel Cherehani ambao ni viongozi wa Vyama vya Ushirika kutoka Ushetu, Mkoa wa Shinyanga wakiongozwa na Ndugu Emmanuel Nyambi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni pia ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo kwanza, ni wanafunzi 86 na Walimu sita wa Shule ya secondari *Steps* kutoka Halmashauri ya Meru Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri tusikilizane.

Wapo pia wanafunzi 66 wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni Umoja wa Vijana wa CCM, Tawi la *UDOM* cha Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 90 na Walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mtakatifu Monica ya Jijini Arusha. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano kutoka Jijini Arusha ambao ni wadau wa Sekta ya Sanaa na Utamaduni wakiongozwa na Ndugu Samweli Malugu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ninazo taarifa mbili za Spika na baadaye kuna mambo mawili halafu tutaendelea na ratiba yetu.

Ya kwanza ni kuhusu taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Bunge yaliyotokana na Taarifa iliyopita ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyolijulisha Bunge, tarehe 13 Aprili, 2023 nimekwishapokea kutoka Serikalini

Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kufuatia taarifa za Kamati za *PAC, LAAC* na *PIC* zilizowailishwa Bungeni mwezi Novemba, 2022.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea tarifa ya Serikali naelekeza sasa Kamati husika zinazoshughulikia Matumizi na Fedha za Umma yaani *PAC, LAAC* na *PIC* ziifanyie uchambuzi ili kubaini ni kiasi gani hoja zilizowasilishwa na *CAG* kupitishwa kuwa Maazimio ya Bunge na hatimaye kuwasilishwa Serikalini zimetekelezwa.

Waheshimiwa Wabunge ili Bunge lipate mrejesho mzuri naelekeza kwamba Kamati zinazohusika mara baada ya kumaliza uchambuzi wake ziandae taarifa ambayo itawasilishwa Bungeni wakati wa kipindi cha siku sita za majumuisho ya Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 124. *(Makofi)*

Ni matumaini yangu kuwa utaratibu huu utaliwezesha Bunge kutekeleza kikamilifu jukumu lake la kuisimamia Serikali kwa kujua ni namna gani Serikali imetekeleza Maazimio yanayotolewa na Bunge kuhusu Taarifa inayotolewa kila mwaka na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Kamati hizi zitapewa muda wa kulifanyia kazi jambo hili na tutapata nafasi kama Wabunge kwa niaba ya wananchi kujua Serikali imetekeleza yapi na yapi inaendelea na utekelezaji na yale ambayo watakuwa hawajakamilisha utekelezaji, Kamati hizi zitaleta taarifa ya hayo yatakayokuwa yametekelezwa Novemba na yale ambayo yatakuwa hayajatekelezwa tutajua pia tuseme nini kwa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa nyingine ni kuhusu Mkataba wa Mauziano ya Trekta wa Kampuni *URSUS* kati ya Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* na wakulima kwa

utaratibu wa mkopo. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka hivi karibuni wakati wa mjadala wa Makadirio wa Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, iliibuka hoja kuhusu changamoto na athari zilizojitokeza katika utekelezaji wa mkataba wa ukopeshwaji wa matrekta ya Kampuni ya *URSUS* uliofanyika kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* na wakulima.

Kwa kuwa mjadala huo ulivuta hisia kali miongoni mwa Wabunge na wananchi walioathirika na mikataba hiyo, niliagiza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kukutana na Wabunge wa maeneo hayo yaliyopata athari ili kuwasikiliza na kubaini tatizo lililopo na kunijulisha matokeo ya kikao hicho.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati kuhusu suala hili iliyowasilishwa kwangu nimebaini kuwa kuna umuhimu wa kazi zaidi kufanyika katika kushughulikia malalamiko ya wananchi ambayo yametolewa hapa Bungeni na wawakilishi wao. Hivyo, naielekeza Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ikutane na Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uwekezaji Viwanda na Biashara, Shirika la Maendeleo la Taifa.

Baada ya hapo, Kamati isafiri kuelekea Mkoani Manyara ili kuwasiliza wakulima walioathirika na mikopo hiyo na kupata taarifa za kina kuhusu changamoto za Mkataba huu na athari zake ili hatimaye kupendekeza hatua za kushughulikia malalamiko yaliyopo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yawezekana suala hili linagusa mikoa mingine pia ila kutokana na changamoto ya muda nimeona Kamati itembelee Mkoani Manyara kwa uwakilishi.

Waheshimiwa Wabunge, ili Bunge liweze kupata mrejesho kamili wa suala hili, nimeelekeza kuwa Kamati

husika mara baada ya kukamilisha kazi yake iandae taarifa ambayo itawasilishwa Bungeni wakati wa kipindi cha siku sita (6) cha majumuisho ya Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 124. *(Makofi)*

Kwa hivyo nafikiri kwa wakati huo tutapata suluhisho la changamoto hii ya haya matrekta ya *URSUS* na kwa hivyo kwa hapa Bungeni tutakuwa tumeishauri Serikali nini cha kufanya wakati huo. Kwa hiyo, Wabunge wote ambao wanaathirika na hili suala la haya matrekta ya *URSUS* wakati Kamati itakapokuwa inakutana wanaruhusiwa kwenda kwenye Kamati ili wakaseme hizo hoja zao. *(Makofi)*

Samahani kuna jambo lingine hapa kabla hatujaendelea, Chombo cha Habari cha *East Africa TV* wameripoti taarifa ya uchangiaji wa Mheshimiwa Janejelly Ntate, wakasema aliyechangia ni Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Kwa hiyo, wafanye hayo marekebisho kadri wanavyonisikiliza ninavyosema wafanye marekebisho ili waandike Mbunge aliyechangia mchango huo kwa usahihi. Kwa sababu huwa inaleta usumbufu ukimwandika mtu ambaye siye aliyesema na yule aliyesema kama ni sifa basi apate aliyesema na kama kuna jambo lingine ambalo wananchi wanataka kulisema basi apate yule ambaye amelisema jambo hilo. Kwa hiyo, wafanye marekenbisho hayo kwa kadri wanavyonisikia nikiwaelekeza kufanya hivyo. Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea

Katibu.

**20 APRILI, 2023**

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Ninayo orodha hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameomba kuchangia. Tunaanza na Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya na Mheshimiwa Anatropia Rweikila Theonest ajiandae.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo mawili. Upande wa utawala bora na upande wa masilahi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwenye utawala bora, nina ushauri mmoja kwa TAKUKURU, kwa sababu kuna masuala mengine yako wazi kabisa lakini michakato yake inachukua muda mrefu sana. Nakumbuka mwaka 2017/2018 kuna mchakato ulianzishwa pale Jijini Arusha, wenzetu wa boda boda wakaweza kuchangisha fedha kiasi cha shilingi milioni 400 ambazo baadaye zilikuja kuibiwa na baadhi ya watu.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, mnamo tarehe 18 Juni, 2021, katika Tawi la *NMB* Mbagala kuna Mtu anaitwa Maulid, mwingine anaitwa Makongoro, Mwingine anaitwa John F. Fungameza, walikwenda kuchukua fedha kwenye akaunti kiasi cha shilingi 39,500,000. Mnamo tarehe 8

Julai, 2021, kuna mtu mwingine tena ambaye anaitwa John na mwingine anaitwa Edwin, walikwenda kwenye Akaunti na kuchukua fedha kiasi cha shilingi 43,500,000. Mnamo tarehe 31 Agosti, 2021, kwenye Tawi la Kariakoo wakachukua tena Fedha kiasi cha shilingi 43,800,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia tena mnamo tarehe 25 Novemba, 2020, kupitia *NIDA* namba ya T100027912657 walikwenda kuchukua shilingi 15,000,000. Orodha ndefu na inaendelea. Hoja yangu hapa ni kwamba hawa watu wa bodaboda fedha zao zimeibiwa na walioiba fedha wanajulikana, wameenda benki wamechukua fedha na wametoa vitambulisho vya *NIDA* na wamechukua kwa majina yako. Hata hivyo, toka mwaka 2020 mpaka leo suala hili halijapelekwa Mahakamani na wahusika hawajakamatwa, badala yake inatolewa fursa kwa baadhi ya watu kuanza kuchafua majina ya watu ambao hwahusiki kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, tuwaombe TAKUKURU, najua wanafanya kazi kubwa na wanafanya kazi nzuri. Kama wezi wanajulikana na ushahidi upo, kigugumizi ni cha nini kuhusu kuwakamata na kuwapeleka mahakamani ili kuweza kuondoa changamoto hii kwenye maeneo mengine?

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili, maana hapa ukiangalia fedha zilizochukuliwa ni kiasi cha shilingi 214,500,000. Hizi ni fedha nyingi sana kama zingepatikana zingewasaidia vijana wa bodaboda kuendelea kukopeshana kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili ni kuhusiana na madai ya watumishi. Ukiangalia Jiji la Arusha ulifanyika uhakiki mwaka 2017 wa kuangalia ni watumishi gani ambao walikuwa wanadai masilahi yao. Ukiangalia mfano, kwenye upande shule ya msingi na shule ya sekondari kwenye uhakiki huo, kwenye upande wa likizo kwa upande wa shule za

msingi zinadaiwa shilingi 105,000,000; Kwenye upande wa sekondari ni shilingi 94,000,000; jumla ni shilingi milioni 200.141.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa waliokwenda masomoni kwenye shule ya msingi shilingi 2,800,000 na shule za sekondari shilingi 600,000, jumla ni shilingi 3,400,000; Ukienda kwenye matibabu jumla ni shilingi 14,775,000; Ukienda kwenye uhamisho wa watumishi ni shilingi 56,757,000; Ukienda kwenye fedha za kujikimu ni shilingi 2,211,000; Ukienda kwa waliostaafu yaani kuna watu waliostaafu kabla ya mwaka 2017, wamelipwa stahiki zao zote, lakini mpaka leo hawajalipwa fedha za kusafirisha mizigo yao ambazo ni kiasi cha shilingi 26,837,013.94; Kuna ambao walifiwa mpaka leo wanadai shilingi 3,150,000; Kuna ambao wanadai hela zao za mizigo shilingi 12,000,000; Kuna nauli pia kwa ajili ya ajira mpya, mtu ameajiriwa nauli yake ya kumpeleka kituoni hajapewa na asingeenda kituoni pengine angepewa adhabu ya kutokuwa kazini. Wanadai na wenyewe kiasi cha shilingi 998,000 tu; na ukiangalia stahiki za Wakuu wa Idara zenyewe ni shilingi 38,050,000. Kwa hiyo jumla yake ni shilingi 358,420,582.89.

Mheshimiwa Spika, ndio maana tunapoona kwenye Jiji la Arusha kuna ufisadi na wizi tunapiga kelele kwa sababu tunaamini tukidhibiti ule wizi, zile fedha zitakuja kuwasaidia hawa wanyonge ambao wanasaidia kufanya kazi mbalimbali kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni ombi langu, si lazima kila kitu tuchukue fedha kutoka Hazina. Zile halmashauri ambazo zina mapato makubwa kama vile Arusha, Ilala, Mwanza zile za majiji zote, wangepewa maelekezo na utaratibu hela ndogo kama hizi milioni 358 wangezilipa wao wenyewe ili kuwaondolea wananchi wetu kero pamoja na masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia fedha hizi katika ufisadi uliofanyika Arusha zile risiti *fake* peke yake tu milioni 699 peke yake zingeweza kulipa deni hili na *change* ingebaki na masuala mengine pia yangeweza kuendelea.

Mheshimiwa Spika, suala lingine pia ambalo ningependa kulizungumzia kuhusiana na watumishi wetu ni kuhusiana na kupanda madaraja kwa watumishi. Kwenye suala la kupanda madaraja, katika hili naomba niipongeze Serikali kwa sababu kwa kweli kuna kazi kubwa imefanyika. Kwa sababu kwanza nafahamu kuna mwongozo wa Serikali ulitoka wa tarehe 27 Machi, 2018 ambao ulielekeza kwamba ukurasa wa pili, kifungu cha 3(b) ulikuwa unasema, kufuta barua za awali za kuwapandisha vyeo na badala yake barua za vyeo hivyo zionyeshe kuwa vyeo vya watumishi hao vinaanza tarehe 1 Aprili, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tafsiri yake ni kwamba walikuwa wamenyimwa miaka miwili ya kupandishwa mishahara yao. Hata hivyo, bahati nzuri kwa sababu ya usikivu wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumeona mwaka huu 2023 tarehe 23 Desemba, umetoka mwongozo wa Serikali ambao umeelekeza watumishi walioathirika na zoezi la uhakiki katika upandishaji vyeo mwaka 2016 ambao walipandishwa kwa makundi mawili ya mwezi Novemba, 2017 na Mwezi Aprili, 2018 na kupanda vyeo walivyonavyo sasa mwezi Mei, 2022, lengo la hatua hii ni kuwezesha uwepo wa msawazisho wa vyeo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni imani yangu kwamba wenzetu Wizara ya Utumishi watahakikisha kwamba wafanyakazi wote hawa kama Serikali ilivyoelekeza, wanaingizwa kwenye utaratibu na wanapata haki zao kama ambavyo Serikali imeelekeza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kulikuwa na changamoto za jumla, Serikali siku za nyuma imekuwa inapandisha mishahara kutokana na uwezo wake wa kibajeti. Kwa hiyo, sisi ombi letu ni kwamba wasiangalie uwezo wa kibajeti, waangalie kama miaka mitatu imefika watumishi wote wajue mwaka huu wanatakiwa wapandishwe, wapandishwe wote. Kwa sababu, mwaka huu ukipandisha nusu halafu mwakani ukapandisha wengine watakuwa wanatofautiana vyeo na mishahara wakati walianza kazi siku moja na sifa kwa ujumla wake zinafanana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, kengele ya pili imekwishagonga.

**MHE. MRISHO M. GAMBO**. Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Rwehikila Theonest na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro ajiandae.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na nikupongeze sana kwa kuweza kusimamia Bunge letu kikamilifu kabisa. Pia nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa Manyoni sisi ametuletea fedha nyingi sana. Vilevile nimshukuru Waziri Kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, lakini vile vile Naibu Waziri Ndugu yangu, Mheshimiwa Ridhiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo nina maeneo matatu ningependa kuchangia. Eneo la kwanza linahusu upungufu wa Maaskari na hali ya usalama Manyoni, eneo la pili

linahusu upungufu wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na muda ukiniruhusu nitachangia kuhusu *Standing Orders* (Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma).

Mheshimiwa Spika, tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi hususani Maaskari katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na katika Wilaya ya Manyoni. Vile vile, sanjali na hilo, Manyoni kumekuwa na matukio mengi sana ya uhalifu. Tangu 2017 kumekuwa na matukio ya aina tatu ya uhalifu. La kwanza, kumekuwa na matukio ya mauaji, watu wanauawa wanatupwa pale Manyoni Mjini. Pili, kumekuwa na tabia ya kufukua makaburi na kuchukua viungo na vitu mbalimbali. Hali hii imekithiri tangu 2017 tumekuwa na haya matukio.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru sana *RPC* wa Mkoa wa Singida na Mkuu wa Mkoa wa Singida, lakini vile vile niishukuru Serikali, hivi karibuni imetuletea Mkuu wa Wilaya mpya Mheshimiwa Kemilembe. Wiki iliyopita Waziri wa Mambo ya Ndani amefanya mabadiliko pale Manyoni, ametuletea *OCD* mpya na amefanya mabadiliko ya Mpelelezi wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, tunahitaji sasa Serikali ituongezee watumishi wa Polisi lakini vile vile iangalie kwa ukaribu hali ya usalama wa Manyoni. Wastani kila mwezi mtu mmoja anaokotwa amekufa pale Manyoni Mjini, lakini watu wanafukua makaburi. Siku hizi wananchi wa Manyoni wanalinda makaburi, tukishazika inabidi uweke mlinzi kwa sababu ndani ya siku tatu unakuta makaburi yameshafukuliwa. Kwa hiyo, naomba tuliwezeshe Jeshi la Polisi, wana upungufu wa magari, hawana pikipiki na wana upungufu wa zaidi ya watumishi 10 pale Manyoni. Pia niombe wapeleke timu ikachunguze yale mauaji, kwa nini yale mauaji yanatokea pale Manyoni?

Mheshimiwa Spika, suala la pili, ni suala la upungufu wa watumishi pale Manyoni. Katika Halmashauri ya Wilaya ya

Manyoni, tuna upungufu mkubwa sana wa watumishi. Upande wa Afya mahitaji ni watumishi 642, lakini waliopo ni 289 na upungufu ni 353. Mgao wa mwaka jana tulipata watumishi wa afya 33 tu. TAMISEMI wametoa tangazo la kuajiri watumishi, tunaomba na kwa kupitia Waziri wa Utumishi, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni tuangaliwe.

Mheshimiwa Spika, upande wa Walimu mahitaji upande wa sekondari ni 460, waliopo ni 268, upungufu ni takribani 138. Vivyo hivyo hata upande wa shule za msingi. Vilevile kwenye kada zingine, upande wa Uhasibu tuna upungufu mkubwa sana pale tuna Wahasibu watatu tu. Kati ya hao ni Mweka Hazina tu ndio ana *CPA,* lakini wengine wote hawana *CPA*. Nimeona hilo nalo niliombe na nimwombe kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Naibu Waziri watusaidie tupate watumishi pale Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, upande wa Walimu, mahitaji upande wa Sekondari ni 460 lakini vilevile waliopo ni 268 upungufu ni takribani 138. Vivyo hivyo hata upande wa shule za msingi. Vilevile kada zingine upande wa Uhasibu tuna upungufu mkubwa sana pale, tuna Wahasibu Watatu tu na kati ya hao ni Mwekahazina tu ndiyo ana *CPA* lakini wengine wote hawana *CPA,* nimeona hilo nalo niliombe na nimuombe Kaka yangu Simbachawene na Mheshimiwa Naibu Waziri mtusaidie tupate watumishi pale Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la wanaokaimu. Halmashuri ya Wilya ya Manyoni haina Mkurugenzi tangu mwaka jana mwezi wa Nane, tunae anaekaimu. Nilisikia wenzangu wakichangia hapa kanuni ya kukaimu, mtu anakaimu zaidi ya miezi Saba miezi Nane, kwa hiyo niliona nalo hilo tulione pia Wakuu wengi wa Vitengo wanakaimu, kwa hiyo hilo nalo niliona nilichangie.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho naomba nichangie upande wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma. Katika Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma kuna maeneo matatu ningependa kuchangia. Eneo la kwanza kuhusu wazazi tunapofiwa sisi na wazazi watumishi wa umma, wazazi hawawi *considered* kwenye suala la mazishi, lakini mnajua msiba unapotokea wa mzazi tegemeo kubwa ni kwa mtumishi. Ningeomba Mheshimiwa Waziri hebu liangalieni hili, wazazi wawe *considered* kwenye suala la kuwahudumia kwenye mazishi, baba, mama anapofariki. Kwa kweli, huwa watumishi wetu wanapata shida sana inapotokea msiba wa mzazi, anaanza kuhangaika kukopa na kadhalika, kwa hiyo hili ni eneo la kwanza ambalo nilidhani ni eneo ambalo tunahitaji kubadilisha zile *standing order* zetu tuweze kuwa-*accommodate* wazazi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mtu kuwa Mkuu wa Idara, taarifa ya *CAG* inaonesha kwamba maeneo mengi Wakuu wa Idara wanakaimu, wanakaimu kwa sababu ya vigezo vyetu vya mtu kuwa Mkuu wa Idara. Ili mtu awe Mkuu wa Idara anatakiwa awe Afisa Mwandamizi, sasa hicho ni kigezo cha juu sana, lakini huko nyuma tulikaa muda mrefu watu hawajapata *promotion*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni nini? nadhani tungeangalia maeneo kwa mfano, kuna kada ambazo ni ngumu sana kupata watu wenye kuwa Waandamizi kwa mfano TEHAMA, Sheria, Manunuzi, hawa watu tuwachukue hata wale wa *Grade One* ili angalau wawe Wakuu wa Idara nadhani hilo litasaidia sana kuhakikisha kwamba tunakuwa na Wakuu wa Idara ambao wanakidhi vigezo lakini vilevile tutajibu ile hoja ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, lingine suala la likizo ya uzazi. Katika likizo ya uzazi kuna mambo matatu ningependa kuchangia, kwanza ni pale mama anapojifungua halafu bahati mbaya mtoto akafariki. *Standing order* inampa siku 42 za kupumzika,

lakini jamani siku 42 ni siku chache sana, mama anapojifungua mtoto akafariki bado anakuwa na machungu mengi, mnataka ndani ya siku 42 arudi tena kazini, mimi ningeshauri hata wale mama ambao wanajifungua mtoto anafariki wapewe zilezile siku 84 kwa sababu anakuwa bado anapitia mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ni kuhusu wanaume, mama amejifungua *standing order* inasema inampa siku tatu, mama amejifungua kwa *operation,* siku tatu mwanaume ndiyo anatakiwa amhudumie *then* aendelee na kazi zingine, nadhani hapa kuna tatizo vilevile kwa hiyo nishauri na yenyewe muiangalie na ningependekeza angalau basi na baba apewe angalau siku Saba ili apate muda mzuri wa ku-*take care* mke wake wakati huo anauguza vidonda vya *operation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la mamlaka ya nidhamu katika Halmashauri zetu kuna mkanganyiko. Kanuni zilizorekebishwa zinasema mamlaka ya nidhamu ni Mkurugenzi lakini sheria inasema mamlaka ya nidhamu ni Baraza la Madiwani. Sasa hapa ningeshauri iangaliwe hii kama tumeamua mamlaka ya nidhamu katika Halmashauri zetu awe Mkurugenzi kote isomeke Mkurugenzi, lakini kama tunasema mamlaka ya nidhamu katika Halmashauri zetu wawe Madiwani basi kote kuwe Madiwani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya nakushukuru sana na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na mimi niongee mawili, matatu

kwenye suala zima linahusu watumishi. Tutakubaliana kwamba maendeleo yoyote, iwe ya nchi, iwe ya taasisi, iwe ya familia inategemea nguvu kazi, pale ambapo unakuwa na nguvukazi ambayo si tu hairidhishi lakini pia inakuwa imekatishwa tamaa na kulegalega, hata kwenye familia binafsi huwezi ukapata mafanikio. Tuangalie mfano mdogo wa *private companies* ni kwa jinsi gani zinaweza zikafanikiwa *vis a vis The Government activities* au *government other things,* unajua ni kwa nini? Kwa sababu wanaweza kuwa *motivated*.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kutoa mfano mdogo tu Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba kuna watumishi ambao wanakuwa ni zaidi ya mwaka mmoja wanadai mishahara, tunategemea mtu afanyeje kazi anadai mshahara kwa mwaka mmoja, *totally impossible!* Mchukue mtu huyo huyo mpeleke kwenye *private company au private business* anaweza kufanya kazi bila kulipwa? Kwa nini tunapaswa ku-*assume* kwamba watu wanaweza kufanya kazi za umma wanaweza kufanya kazi Serikalini bila kulipwa na wakaendelea kufanya kazi? Tunaendelea kujidanganya.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme Mheshimiwa Waziri na nitataka baadae nitatoa Shilingi atuambie ni kwa namna gani hili suala halitajirudia la Watumishi wa Umma kudai malimbikizo, kudai mishahara wakati huo huo tunategemea walete *productivity,* hicho kitu hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali nitataka niseme kwa kifupi kuna suala zima la *TASAF*. Kila mmoja anelewa umuhimu wa *TASAF,* na swali langu ninalotaka ku-*pause* ni kwa kiwango gani *TASAF* inaweza kuwa endelevu kama inategemea kuwa *financed na donors* au misaada kwa maana Wizara haitengi fedha kwa ajili ya *TASAF?* hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwa nini *TASAF* imekuwa inatumika kama siasa kwenye maeneo yetu, huwa napokea simu nyingi sana wananiambia Mheshimiwa Mbunge nimetishiwa kuondolewa *TASAF* kwa sababu nimeonyesha nina i*nterest* ya Chama fulani. Mimi nadhani haya masuala yafikie mwisho, siyo mara ya kwanza linasemwa hapa Bungeni na siyo mara ya pili na siyo mara ya tatu *unless* Waziri atuambie kwamba *TASAF* inatumika kama kiboko kwa ajili ya *interest* za siasa za Chama Fulani. Nadhani ifikie mwisho na niseme bayana kama itatokea Watendaji wanataka kuwa-*punish* watu kwa sababu ya *interest* fulani za vyama na nini kwa kuwanyima *TASAF* hatutakubali, na tutakaa kuipinga sasa kwa sababu itakuwa haina tija au itabidi itengenezewe jina jingine kwamba hii siyo *TASAF* bali ni *motivation* ya kujiunga na itikadi fulani hilo naomba niliweke wazi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuje kwenye suala zima la upungufu wa watumishi….

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatriopia nieleweshe vizuri kuhusu jambo hili, kwa sababu niliwaona Wabunge hapa ambao ni wa Chama cha Mapinduzi na walisimama kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali kuhusu *TASAF* kwamba kuna watu ambao hawamo na wanastahili.*(Makofi)*

Hii hoja ya kwamba ambao hawamo wanaokutafuta wewe lazima wahusishe hoja ya kutokuwemo na Chama fulani inatokana na nini labda au kwa sababu wewe ni wa Chama kingine kwa hivyo wakikupigia lazima kuna uhusiano na Chama chako. Kwa sababu nimeona nimeyasikiliza maswali hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu maswali mengi sana kuhusu *TASAF* na hao ni Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, hebu nieleweshe mimi ili nijue jambo hili limekaa vipi, Mheshimiwa nakuomba uendelee.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo tunatoka ukionekana una-*element* za Upinzani moja kati ya kitu ambacho wanaambiwa tutakutoa *TASAF* na *the next month* hapokei fedha, anachopaswa kukifanya ni kwenda kufuatilia mchakato ni wangapi wana uwezo wa kwenda kufuatilia mchakato kama akikubali imeishia hapo, lakini kama ni mtu *fighter* anasimama *firm* anapambana mpaka anarudishwa kwenye *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, *point* ninayotaka ku-*make*…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nimekuona nitakupa nafasi. Unajua Mheshimiwa Anatropia mimi nisingependa Bunge hili lifikie mahali kwa sababu siku moja niliwahi kusema hapa hatuelekei kufanya maamuzi lakini sasa tunaelekea kufanya maamuzi ukituweka kwa sura hiyo, nimeuliza hivi Wabunge kuna Mbunge mmoja sema sikumbuki ni nani, aliyesema kwake kuna watu ambao wameondolewa kwenye *TASAF* wakati vigezo bado wanavyo ni nani? Ni Mbunge gani? nadhani Mheshimiwa Sekiboko pale na anatoka Tanga na yeye ni Mbunge wa Viti Maalum. Tanga hakuna Jimbo la Upinzani kule, sasa mimi nawaza kule wale wananchi wa Tanga aliowasemea anatoka Korogwe siyo? Hebu washa kisemeo. Ulisema ni Korogwe au ni wapi?

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, ni Korogwe Mkoa wa Tanga, Korogwe Mjini.

**SPIKA:** Sasa Korogwe Wabunge wote wawili wa Wilaya ya Korogwe ni wa Chama cha Mapinduzi na kule wapo ambao walikuwepo na sasa wameondolewa kwenye mfumo na ndiyo Wabunge walikuwa wanasema wameondolewa kimakosa kwa sababu vigezo bado wanavyo. Hii hoja ya kwamba wanaokupigia wewe wameonesha alama pengine ama namna fulani kwamba ni wa Chama.

Waheshimiwa Wabunge, nisingependa Bunge lifikie hapo mahali na sababu ni za msingi kabisa, Wabunge wa CCM kama wanaongea na wewe unazungumza hoja yako ni ya msingi, kwamba watu wanostahili wapewe na wasiostahili waondolewe na vigezo vitumike vile vilivyopo, sasa ukiiweka kisiasa kidogo inakuwa mtihani. Hapo ndiyo shida yangu ilipo.

Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi wito wangu ninaotaka kauli ya Mheshimiwa Waziri aseme bayana watu wasionewe au wasipewe kwa sababu iwayo yoyote na kigezo kibaki kilivyo leo. Haya maeneo tumetofautiana uelewa. Korogwe wanaweza kuwa waelewa na eneo jingine vipi maeneo ambayo wengine tunatoka? Ndiyo nataka kauli iwe *firm* kwamba mtu apewe *TASAF* kwa sifa ya yeye kuwa na uhitaji wa *TASAF full stop*, hiyo ndiyo *call* yangu.*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, nadhani hujanielewa vizuri, Mbunge wa jimbo unalotoka wewe ni wa Chama gani? Jimbo unalotoka wewe walimchagua Mbunge wa Chama gani?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Tume ilimtangaza Mbunge wa CCM.

**SPIKA:** Ndiye aliyechaguliwa. Kwa hiyo, hoja ya kwamba walioko kule wakikupigia wewe ni wa CHADEMA hilo ondoa kabisa, *TASAF* hata Majimbo ya CCM yameulizwa maswali hapa ndani. Kwa hiyo, iondoe kabisa hiyo sijaelewa ambapo wewe hunielewi ni wapi. Ukiiweka tu kisiasa kwamba kuna mtu hapewi kwa sababu ya siasa humu ndani Wabunge wa CCM wameuliza maswali, ukisema kuna mtu anaondolewa kwa sababu ya kisiasa pia unakuwa hauko

sawasawa kwa sababu Wabunge wa CCM wameuliza vivyo hivyo.

Kwa hiyo, wewe changia kwamba kuna hiyo changamoto kwenye *TASAF* na sote tumeisikia hapa, usiiwekwe kisiasa kwa sababu *TASAF* kwa maelezo mimi nikikaa hapa mbele nimewasikia na leo uzuri swali lilikuwepo hakuna mtu aliyeuliza swali kwamba kuna mtu alionyesha kadi ya chama fulani ndiyo akapewa au chama fulani ndiyo akanyimwa Hapana! Kwa sababu hata wewe nikikuambia uthibitishe huna uwezo huo. Ama unao Mheshimiwa Theonest ndiyo maana nilikuwa nakuwekea mazingira hayo mchango wako uwe wa jumla kwa changamoto za *TASAF* na siyo kwamba wenye changamoto wana viashiria vya Chama fulani hapana.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru niendelee. Naomba mchango wangu uwe jumla katika changamoto…...

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ngoja kwanza Mheshimiwa Rose lazima uitwe kwanza ndiyo uanze kuzungumza. Mheshimiwa Anatropia kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Rose Busiga. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Dada yangu kwamba kwa uzoefu nilionao kuhusu *TASAF*. *TASAF* wanapochaguliwa ni Kijiji husika, kinakuwa na Mkutano wa hadhara, Mwenyekiti wa Kijiji pamoja na Mtendaji wa Kijiji wanapokuwa pale kwenye mkutano wanakijiji wenyewe wanajua maisha ya wenzao ndiyo wanachagua pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Theonest unaipokea taarifa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, naendelea. Kwa sababu wakati mwingine haya mambo huwa yanashamiri sana ikififika wakati wa maneno mengi, nakushukuru sana niendelee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya watumishi. Kuna changamoto kubwa na *CAG* ameainisha dhahiri kwamba kuna upungufu wa asilimia za kutosha, anasema silimia 35 tukiongela kwenye kada nzima ya elimu.

Mheshimiwa Spika, kwa tathmini ambazo kwa *projection* za kuwa na wanafunzi 50 mwalimu mmoja katika shule ya msingi, lakini mwalimu mmoja wanafunzi 20 kwa shule ya sekondari tumeona bado ni changamoto na hatuoni dalili ya kuifikia kama kuajiri bado kunaendelea kwa kusuasua. Hii hapa imekuwa na *impact* kubwa, nitatoa mfano. Katika taarifa aliyoitoa kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* inaonyesha wanafunzi asilimia 66 wamepata *Division Four* mpaka *Division* Zero na hiyo inatokana na kwamba wanafunzi wengi hawajaweza kupata *access* ya mwalimu. Walimu hawajaweza kufundisha vya kutosha kwa sababu madarasa yetu ni makubwa na hiki ni kilio nikitoe kwenye eneo langu ambalo ninatokea kwenye Mkoa wangu wa Kagera hususani Wilaya ya Kyerwa, kuna changamoto kubwa ya walimu.

Mheshimiwa Spika, niombe katika uajiri unaoenda kuufanya katika ajira zilizotangazwa tupewe kipaumbele, moja haya ni Majimbo ya Vijijini hii nitoe ni *general call*, Majimbo ya Vijijini na maeneo mengine lazima yawe na motisha ukilinganisha na maeneo ya Mjini. Kwanza kila mtu anajaribu ku-*avoid* vijijini, iwapo mishahara ya walimu na watumishi wanaofanya kazi vijijini ikiwa juu pamoja na *allowance* za posho za kufundisha posho za maeneo

inaweza kuvutia kwa wingi haya maeneo kuwa na walimu wa kutosha kinyume na hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia tuna changamoto ya walimu wa kike ni maeneo mengi nchini. Walimu wa kike ni muhimu kwa sababu mkumbuke kwamba katika *level* ya chini wanafunzi wengi pia ni wa kike, wanahitaji *assistance* ya walimu wa kike lakini wanahitaji *role models* ya walimu wa kike. Tunawezaje kuwa-*motivate* walimu wa kike kubaki kwenye maeneo yetu. Moja ni lazima tuwaongezee posho, mbili ni lazima tuwape mazingira ambayo wanaona kwamba ni rafiki, nyumba za watumishi na maeneo.

Mheshimiwa Spika, nataka pia niongelee kukosa *motivation* kwa watumishi kama nimeeleza tangu awali nikianza na kuwa na malimbikizo makubwa ya mishahara, siyo hiyo tu hata wanaosataafu unatumikia leo una uhakika kwamba hata ukija kustaafu utalipwa posho zako na kiinua mgongo, hiyo michango yenyewe ambayo mamlaka na taasisi mbalimbali zimekuwa haziwasilishi zimekuwa ziki-*accrue interest from time-to-time*.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mmoja tu, kwa ajili ya kutopeleka hayo makato Halmashauri kadha wa kadha zimepata faini mfano mmoja Halmashauri ya Muheza ililipa *twelve million*, Biharamulo *six million*, Kaliua *five million*, Mlele *five million*, kwa ku-*sum up* zimetumika zaidi ya Billion 260 katika kulipia faini za kutokusanya michango. Sasa leo hatuajiri kwa sababu hatuna fedha lakini hizohizo fedha zinaenda kutumika kwa ajili ya *interest* za kutopeleka fedha za makato mbalimbali kwenye taasisi husika, na hilo ni swali la jumla ambalo naweza kulitoa hapa, tujiulize sisi kama Serikali mjiulize ninyi kama Wizara mnataka ku-*achieve* nini? Kusimamia watu kupeleka hayo makato ili msilipe *interest* na badala yake hiyo pesa ndogo tuitumie kuajiri watumishi? Au tubaki nazo mezani ili kesho tulipe *interest?* Kupanga ni kuchagua!*(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mambo makubwa na mazuri yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita ni kuongeza *motivation* kwa watumishi na hasa kupitia haki na stahiki zao.

Mheshimiwa Spika, ninazo taarifa rasmi na ni za uhakika mwaka 2020/2021 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati anaingia madarakani alikuta bajeti ya Watumishi kupandishwa madaraja ilikuwa ni watumishi 91,000 lakini mpaka Januari mwaka huu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amepandisha madaraja zaidi ya Watumishi 263,555. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani alikuta tatizo kubwa la malimbikizo ya mishahara, mpaka mwezi Januari Tarehe 30, alikuwa amekwisha kulipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi zaidi ya 116,000 katika Serikali hii. Kwa hiyo, ninachotaka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge ni kwamba siyo kweli Serikali haioni umuhimu wa haki na stahiki za watumishi ili kuwapa *motivation* katika kufanya kazi zao za kila siku. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kitu ambacho napaswa nikiweke wazi mtumishi

kupandishwa daraja siyo hisani, ni kwa mujibu wa Kanuni na Utaratibu lakini pia ni *increment* kwa kazi aliyoifanya. Huwezi kuajiriwa leo ukalipwa sawa sawa na yule aliyekaa miaka Mitano, huo ni wajibu wa Serikali kupandisha madaraja ndiyo tunayaongea hapa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

**TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa taarifa Mheshimiwa Anatropia kwamba madai ya Watumishi wa Umma mwaka 2019/2020 ilikuwa Bilioni 334, mwaka 2020/2021 yakaongezeka yakafika Bilioni 429, taarifa ya juzi ya CAG inaonesha madeni ya Watumishi yamefika Bilioni 509, ni taarifa tu nilikuwa nampa Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, naipokea sana, na hilo ndiyo ninalolisema leo. Tunaweza ku-*achieve* tunachokitaka kama tuna *right people on the ground*. Ni lazima watumishi wawe *motivated* kwa kulipwa malimbikizo, kwa kupandishwa madaraja, kwa kulipwa fedha za uhamisho, kwa kulipwa posho kadha wa kadha ambazo zipo kwa mujibu wa utaratibu. Hivyo ndivyo watakavyofanya kazi. Tunakwama wapi? Nilikuwa naangalia *clip* moja inayoonesha ni namna gani nchi kama Singapore iliweza kufika ilipo. Jibu lilikuwa moja, lazima uwe na watumishi sahihi, ndiyo utaweza ku-*achieve* hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, na Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Waziri. Siku ya leo nitazungumzia Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, na nitazungumzia *narrative* na mkanganyiko uliopo kwenye eneo la maadili, umasikini, uzalendo na utajiri katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiona mtumishi yeyote wa umma anapotajirika, anapomiliki gari, anapomiliki nyumba, umbea unaanza kwenye maeneo mbalimbali ya kazi. Inafika mahali baadhi ya viongozi, hata Waziri akienda nje ya nchi, akikutana na wawekezaji wakimpenda yule Waziri kwa utaalamu wake na uwezo wake alionao wakataka kuja kuwekeza nchini, hata kama wanataka washirikiane naye, yule Waziri anaruka maili 100. Anaogopa, anajiuliza, hii fedha nikiipata kwa kuwekeza na hawa watu, nitaiweka wapi? Ni kwa sababu kwenye Taifa letu kumekuwa na mkanganyiko kati ya hayo mambo matatu mpaka manne.

Mheshimiwa Spika, wale watu wa Tume ya Maadili ya Utumishi wa Umma, wame-*focus* mara nyingi kwenye kuangalia *properties* na kwenye fedha za watu, wakichukulia hicho kama kigezo kikuu cha kujua kwamba huyu ni mzalendo ama sio mzalendo. Sijui hiyo *narrative* imetengenezwa kuanzia mwaka gani? Inafika mahali mtu kuwa na mali, kuwa na utajiri anakuwa na msongo wa mawazo, anawaza atauweka wapi.

Mheshimiwa Spika, Taifa letu katika mchakato wa maendeleo na makuzi ya Watanzania tunapopeleka watoto shuleni, wanakwenda kusoma kuanzia Chekechea mpaka

Vyuo Vikuu. Wanasoma, wanamaliza *degree* zao, wanakuwa na kipindi kile cha kuhangaika kutafuta ajira. Kipindi kile vijana wengi wanakuwa wametawaliwa na mawazo ya ku-*enterprise,* wanakuwa na *startups* nyingi sana. Asilimia 99 ya *startups* nyingi zinafia pale kwa sababu nyingi zinakosa mitaji ya kuziwezesha ili ziweze kukua. Sasa wale Watanzania wachache wanaobahatika, labda ataajiriwa *TANESCO*, Wizara ya Madini, au eneo lingine, ile *knowledge* aliyoipata shuleni inamsaidia kupata ajira kwenye ile taasisi ya umma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwa ameingia kwenye taasisi ya umma, atafanya kazi miaka mitano mpaka 10, na pale ataweza kupata uzoefu wa kutosha. Eneo sahihi ambalo binadamu yeyote anaweza akawekeza ni eneo lile ambalo amelifanya kazi na amelisomea. Sasa Watanzania kwa hizi sheria zetu tulizoziweka za Tume za Maadili ya Viongozi wa Utumishi wa Umma, wanapoanza kuwekeza siku ile ile tu amejenga kakibanda, umbea unaanza. Ataandikwa kila sehemu, atashtakiwa kwa bosi.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri amejitihadi basi kwenye zile fomu zetu tunazozijaza kila mwaka za maadili ya viongozi, awe ameandika nina nyumba mbili, nina viwanja viwili, basi nimenunua na Subaru. Sasa figisu zitakazoanzia hapo, pamoja na ku-*disclose* ile, pamoja na ku-*declare* kwamba mimi pamoja na kwamba ni mtumishi wa *TANESCO* ninamiliki hiki na hiki na hiki kinachofanana na yale ninayoyafanya. Bado figisu ni nyingi, ni nyingi tena huyo ndio asahau kabisa hata kuja kupandishwa cheo. Kwa sababu ataonekana sio mzalendo, ataoneka huyu mtu hana maadili, ni mwizi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine tunataka Taifa letu liendelee, tunataka Watanzania wawekeze, tunataka Watanzania wawe na mali, tunataka makampuni ya Watanzania, tunataka tutoze kodi. Sasa hii *confusion* mimi huwa najiuliza, ni lazima ifike mahali kama Taifa tuweke mipaka ya *definition ya conflict ya interest.* Mwisho wa siku

tunajikuta sheria tunazoziweka kama Taifa zinakuja kuwabana Watanzania na watu wanashindwa kuwekeza kwenye Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, nimeona hii Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma wamekwenda mashuleni, wanaanzisha *club* za wanafunzi, wamekwenda huko kwenye sekondari na shule za misingi, sijui wanawafundisha vitu gani kule. Maana unaweza ukakuta *confusion* ya *narrative* tuliyoanza nayo kwenye enzi zile pengine ni wakati wa ujamaa bado wanaiendeleza. Mimi ningejua kama wanakwenda kwenye ile shule ambako kuna mwanangu Ndairagije na Irakoze ningewaondoa pale ningewapeleka shule nyingine. Wasiwapelekee *confusion* hiyo.

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu ni kwamba hawa watu wanavyofundisha maadili ya umma, basi wafundishe na Watanzania kujifunza kuwa na kiu ya kuwekeza, kutunza mali, ku-*enterprise* ili Taifa letu na sisi tuwe na mabilionea ambao ndani ya Afrika watasikika na ndani ya ulimwengu watasikika wanaotoka Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunaenda kuwapitishia bajeti na wameshaanza kazi ya kwenda mashuleni kwenye sekondari na shule za msingi kufundisha watoto wetu, naomba kabisa waende watengeneza mtaala mzuri unaochanganya maadili, uzalendo na utajiri. Isifike mahali kwenye Taifa letu mtu akiwa na hela kidogo anajiuliza Mungu wangu, nitazificha wapi?

Mheshimiwa Spika, hawa watu wanapokuja kwako, siku wakigundua kuna ka-*issue* ama labda kuna kiwanja kimoja ulikisahau, yaani wanakuja kama Polisi, *as if* gereza liko mlangoni kwako, kesho wanakufunga. Nilitarajia hawa wenzetu wawe *facilitative,* yaani wawe *engaging,* waende kuwa-*engage* Watanzania, umepataje hii? *Okay* ulipata vizuri, endelea kuwekeza na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, sasa imefika mahali kwenye Taifa letu kwa kweli Watanzania wengi wanaishi kwa uoga, wale walioko kwenye Ofisi za Serikali ni waoga, hata Mawaziri wenyewe. Mimi nilitarajia kwenye Taifa letu tuwe na Mawaziri wanamiliki hata ndege, sasa sijawahi kusikia hata Waziri mmoja hapa anamiliki ndege. Ni waoga! Nilitarajia kwamba kwenye Taifa letu tuwe na Mawaziri ambao akienda nje kweli ametumwa na Serikali kwenda kufanya kazi hii na hii; pia ni *expert* kwenye eneo lile, watu wanapenda kufanya nao *partnership, joint venture,* lakini wote ni waoga. Sasa matokeo yake ni kwamba tunajinyima fursa. Kama mtu anataka kufanya *partnership,* sheria zetu zinatubana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba hii ofisi ya masuala ya Utumishi na Utawala Bora waende waangalie kwa kina haya masuala ya maadili, uzalendo, umaskini na utajiri. Waangalie *confusion* inatoka wapi? Watusaidie huko mashuleni wanakokwenda kuwafundisha watoto wetu masuala ya uzalendo, wakajifunze masuala ya kuwekeza, masuala ya kuweka akiba, masuala ya kutunza; yaani wawe na kiu ya kuwa matajiri. Hii *narrative* ya kuonesha kwamba mtu ukiwa na mali ni fisadi; yule ni fisadi yule, yule ni mwizi, ona sasa ameanza kuwa na kitambi, mwizi yule! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kote Tanzania, vijiweni wapi, mtu yeyote, tena baadaye wanavuka wanasema, aah, yule ni *Freemason*. Kwa hiyo, tumekuwa na *narrative* ambayo kwa namna moja inaturudisha nyuma. Kwa unyenyekevu mkubwa, nimalizie kwa kusema kuwa, naomba watu wa Utumishi na Utawala Bora watutengenezee mtaala unaohamasisha utajiri ndani yake.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo, na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Shukrani zangu ziambatane na pongezi za kukupongeza wewe binafsi, kwamba unawatia moyo wazazi wengi ambao wamewekeza kwa watoto wa kike. Wanawaambia wasome kwa bidii ili siku moja wawe ma-*lecturer* kama wewe; wanawaambia wasome kwa bidii ili siku moja wawe Wanasheria kama wewe; wawe wanasiasa kama wewe na ikiwekezekana waweze kushika Mhimili kama wewe ulivyo. Kwa hiyo, unatutia moyo sana mabinti wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kabisa kwa kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Kwa dhati ya moyo wangu kama mwakilishi wa wana-Momba, naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Hassan Suluhu kwa miradi yote ya maendeleo ambayo tumepewa ndani ya Jimbo la Momba. Ingekuwa naruhusiwa kupiga magoti hapa, ningepiga goti la heshima la kuonesha shukrani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo utajielekeza kwenye kuwasemea vijana wa Kitanzania, hususan kwenye suala la ajira. Ajira kwa vijana ni suala la usalama kama ambavyo tunavyoangalia usalama wa afya zetu na usalama wa chakula. Vijana ambao wanaajiriwa katika kipindi hiki, miaka 20 ijayo ndio viongozi wakubwa wa mhimili kama wewe, ndio atapatikana Mheshimiwa Rais hapo, Baraza la Mawaziri, na Wabunge kama sisi. Kwa hiyo, ni usalama wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya ajira nchini kwetu, lakini changamoto ya ajira siyo *issue,* ila ni namna ambavyo ajira hizi zinagawanywa; ni

namna ambavyo ajira hizi zinaenda zikiwa na usawa sawia, *especially* kwa sisi ambao tunatoka vijijini ambako hakuna fursa nyingi za biashara, hakuna makampuni binafsi ambayo tunajua kwamba watu wanaweza wakaajiriwa huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba changamoto ya ajira inawezekana inasababishwa na jambo fulani. Kwenye uchumi kuna kitu kinaitwa *demand and supply*. *Supply* inapokuwa *low* au inapokuwa *limited, demand* ikiwa *high* inapelekea bei kupanda kwa kitu husika. Kwa hiyo, mahitaji yanapoongezeka, bei inapokuwa juu, lakini vitu hivi huwa vinaboreshwa, kwa sababu watu wanalipia gharama kubwa kupata hicho kitu.

Mheshimiwa Spika, sasa tuangalie kwenye ajira zetu, inawezekana changamoto ya ajira imetokana na kuwepo kwa teknolojia na kuongezeka sana. Teknolojia imechukua ajira nyingi za vijana, lakini pia nchi yetu imepiga hatua kwenye kuboresha elimu. Wasomi wameongezeka ukilinganisha na nyuma, lakini mambo yalivyoendelea sana, kwa mfano mambo ya *artificial intelligence* mambo ya *Web3,* mambo ya *Blockchain,* yamechukuwa ajira za vijana, lakini tunaongelea hicho kidogo ambacho kinapatikana chenye thamani, kinatakiwa kipatikanaje? Changamoto ndiyo inaanzia hapo.

Mheshimiwa Spika, mimi naona kwamba ipo misingi ya utawala bora iliachwa kwa namna ambavyo ajira hizi zinagawiwa. Kwenye misingi ya utawala bora, kuna vitu ambavyo unaambatana navyo. Lazima kuwe kuna uwazi, namna ambavyo ajira hizi zinapatikana, ni kwa uwazi? Zinagawiwa kwa uwazi? Ushirikishwaji; ajira hizi zinapokuwa zinagawanywa kunakuwa na ushirikishwaji kila mtu aweze kuona? Kuwajibika; watu wanawajibika wanapogawa hizi ajira kwenye Halmashauri zote na kwenye maeneo yote, na kwa watu ambao hawana watu wa wakuwasemea? Ufanisi; kuna ufanisi kwenye jambo hili? Je, kuna usawa na ujumuishi?

Je, watu ambao hawana watu wa kuwasemea, hawana ndugu zao viongozi, usawa umefanyika? Je, makubaliano yanayoelezeka, yapo makubaliano ambayo yakionekana kwamba hapa palifeli tukubaliane ili wakati mwingine iweje? Je, usikivu wa karibu wa Serikali, jambo hilo linafanyika? Lingine ni kufuata utawala wa sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo hili likapelekea jamii kuanza kukosa Imani. Siyo kwamba labda inakosa imani na Rais wao, lakini inakosa imani na wale ambao watu Rais amewaamini, mamlaka zimewaamini, ambapo wao ndio wanachakata hizo ajira ziweze kuwafikia watu wote. Kwa nini wananchi wakapoteza imani? Kwa nini wananchi waache kuamini mfumo ambao unachakata ajira, waanze kutufuata sisi Wabunge? Kila Mbunge anafuatwa ili aweze kumsaidia mwananchi kuweza kupata ajira? Mimi mwenyewe kwenye simu yangu nini meseji zaidi ya 300; kila mtu ananiambia wewe ni mtu mkubwa. Mimi ni mtu mkubwa kuanzia lini? Mimi kazi yangu ni kuwasemea wananchi, kuyaleta mahitaji yao hapa kwa Serikali. Kwa nini wananchi wapoteze imani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi watakapopoteza imani kwa vyombo ambavyo vinachakata ajira zetu, tutatengeneza jamii ambayo itakuwa na matabaka sana. Miaka 20 au 30 inayokuja tutakuwa na watu ambao wanaamimi kila mtu aliyeko madarakani ni mtoto wa kigogo, kitu ambacho siyo kweli. Sisi wengine ni watoto wa wakulima, mbona tuko hapa ndani! Kwa hiyo, ni lazima ajira hizi ziwe jumuishi, ajira hizi zizingatie utawala bora ili kila mtu aweze kupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini imani ni kitu cha muhimu? Hebu tuangalie, mimi kwa imani yangu kama Mkristo, tunaamini kwamba hata Mungu wakati anaumba ulimwengu, aliumba kwa imani. Nisome kwa Waraka wa Waebrania Sura ya 11 mstari wa kwanza mpaka wa tatu.

Biblia Takatifu, inasema hivi: "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasionekana. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa. Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa na kwa neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Biblia yenyewe inasema kwamba imani ni kuwa na hakika na mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Kwa hiyo, wananchi wakianza kuamini kwamba sisi hatuwezi kutendewa haki, mbele tunaweza kutengeneza kizazi ambacho ni cha waasi. Mbele tukatengeneza watu ambao hawatawaamini tena viongozi walioko madarakani, kwa sababu watakuwa wanamwona kila aliye Spika ni kwa sababu alikuwa ni mtoto wa kigogo. Jaji Mkuu labda wa Mahakama, ni mtoto wa kigogo. Ni lazima tuweze ku-*balance* kama ambavyo wazee wetu wa zamani, kila mahali ambapo nchi hii ilitoka, alitoka kiongozi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiangalia Kanda ya Ziwa, alitoka Rais wa kwanza; tukiangalia sijui Rais wa Awamu ya Nne Dkt. Jakaya Kikwete, ametoka Pwani; tukiangalia sijui Mtwara kule, alitoka Rais. Pia nchi hii, wako Viongozi kama akina Kawawa, walitoka sehemu za kawaida. Kwa hiyo, ni lazima ajira hizi ziwa-*spot* vijana kutoka maeneo yote. Ni lazima Serikali ifike hatua itengeneze imani kwa Watanzania kwamba ajira hizi zinapotokea, wakikaa chini huko sirini ambapo sisi hatuoni, wawaaminishe Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni nini? Ushauri wangu ni mambo yafuatayo: Wapo vijana wengi wa Kitanzania ambao ni ma-*programmer* wazuri sana. Mimi mwenyewe *by professional ni programmer*. Tunaomba vijana hawa wa Kitanzania waitwe, wawasaidie kutengeneza *system* ambayo mtakapokuwa mkikaa sirini, mkiwaita vijana; kwa mfano, kama nafasi zilizotolewa ni 21, kama 100,000

wana sifa, *system* ile iwe ya wazi. Tuweze kuona kwamba kama watu 100,000 wana sifa, *system* iweze kuwachakata tuone. *System* yenyewe iwa-*terminate* kulingana na *system* ilivyo. Hii itafanya tusindelee kuona kwamba Serikali ni *bias*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imani hiyo hiyo kwa Watanzania ambayo imejengeka kwamba nafasi ambazo zinatolewa, zinatolewa kwa kujuana; mwaka 2022 ulivyotupeleka sisi Jeshini, kuna nafasi za Watendaji zilitolewa kwenye Halmashauri yangu. Kule ambapo nafasi zilikuwa zimetangazwa kulikuwa na watoto wengi ambao wanajitolea kwenye Halmashauri ya Momba. Yule mtu aliyetoka Tume, cha kushangaza, sisi hakuna hata mtoto mmoja aliyetoka Momba. Sasa kwa sababu tumejenga imani ya kwamba nafasi hizi zinatolewa kwa madili na janja janja na mbambamba nyingi, hata mimi mwenyewe Mbunge naamini yule mtu aliyetoka kule Tume alikuja na majina yake mfukoni, ndiyo maana hakutaka kuwapa nafasi watoto ambao walitoka kwenye Halmashauri ya Momba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu jambo hili liliteta uchungu kwenye Jimbo la Momba…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, jambo hili liliumiza sana wazazi wa Momba kwamba ilikuwaje kwamba watoto hawa ambao Halmashauri ilikuwa imewaamini, wanajitolea na wanakusanya mapato TAMISEMI, halafu leo walipoingia kuhojiwa, eti watoto wao hawakuwa na sifa. Ni kitu ambacho hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye misingi ya utawala bora inasema, lazima kuwe na usawa na ujumuishi. Sasa hiyo usawa na utawala bora ulikuwepo wapi ambapo sisi hatukufanyiwa usawa na hatukujumuishwa? Hivyo naomba,

hata kwenye ajira hizi ambazo zimetolewa, watoto wote wa Kitanzania, misingi ya utawala bora ifuatwe wakati watakapokuwa wanapewa ajira. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** …bila ya kujali ni mtoto wa kigogo, bila ya kujali ni mtoto wa nani, tunatamani kuona hata watoto wa masikini na wakulima wakishika nafasi kubwa kwenye nchi hii kama ilivyo kwenye viongozi wetu wa zamani. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Unajua ilikuwa ngumu hata kuruhusu taarifa hapo, maana alikuwa haweki hata koma wala nukta. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, hata mimi nikashindwa hata pa kumwambia kwamba muda wako umeisha. Imebidi nimsikilize mpaka aweke nukta. Sasa alipoweka nukta, ndiyo nimeweza kumwambia muda wake umekwisha. Kwa hiyo, kulikuwa hapo na…

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkoni hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa ninyi wawili mlikuwa mmesimama hapo mnataka kumpa taarifa, sasa mwenye kupokea taarifa ameshakaa. Sasa kwa sababu taarifa ni mchango, enhe, Mheshimiwa Getere ulikuwa unataka kusemaje?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa.

**SPIKA:** Sasa usimpe taarifa, wewe sema tu ulivyotaka kusema.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, maelezo yangu yalikuwa hivi, tumezungumza Wabunge hapa kwenye jambo hili, wanaoenda kufanya usahili kwenye watu wanaoajiriwa, ni watu wanaitwa sijui menejimenti kutoka kwenye mashirika ya umma, sijui wapi? Hawa watu ndio wanaofanya usahili, ndio wanaotunga mitihani, ndio wanaosahihisha, wao ndio wanaotoa majina na wao ndio wanaopeleka majina.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kweli nani anayeamini maneno hayo? Anayeamini nani? Watu wale wale tu ndiyo wanafanya kazi zote na kutoa majina na kupeleka. Kwa kweli hapa kuna upendeleo wa kutosha. Lazima tufanye mabadiliko kwenye jambo hili. Kwa nini hili jambo tunaliona kwamba kila wakati lina matatizo tunaendelea nalo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi hii. Niseme tu kwa kifupi kwa kutoa taarifa na kuweka kumbukumbu sahihi ni kwamba tukiliacha likaenda hivi kuna athari kubwa ya kupotosha kwamba masuala haya hayafuati utaratibu, hakuna utawala bora, hakuna sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba katika kuzungumza uhalisia wa jambo, mamlaka ambayo inatunga mitihani siyo ile iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala

Bora. Kuna tume maalum ambayo inafanya hivyo lakini kimsingi huo huo ni sisi wenyewe tumetunga sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, weka vizuri kisemeo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, ni sisi wenyewe tumetunga sheria na kuzipitisha katika Bunge hili. Ibara ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelezea kuhusu usawa na Ibara ya 13 inaelezea kuhusu kuto kuwa na ubaguzi lakini kwenye msingi wa sheria zetu za ajira hizi. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini inakataza kwa namna yoyote kazi kutolewa kwa misingi ya ubaguzi, ukanda, upendeleo au kwa misingi yoyote ile ambayo itakuwa kinyume na hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sheria itatoa maelekezo na miongozo ya utaratibu wa kupata watumishi wa umma kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na kunakuwa na majopo maalum ambayo yanapatikana kwa utaratibu kabisa ulio na uwazi na ufasaha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, niweke kumbukumbu tu sahihi kwamba ni kweli ajira huwa zinatolewa lakini kwa sababu ya wingi na changamoto zilivyo, inafikia hatua wanatengeneza watu mazingira ya kudhani kwamba mtu anaweza akapata ajira kwa *memo,* siyo kweli. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, hatuna utaratibu wa kutoa ajira kwa

*memo* isipokuwa tu ambalo tunalichukua kama Serikali na kulifanyia kazi katika Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, na Ofisi ya Waziri Mkuu ni hili la kwamba utaratibu sasa wa kusahili wa watu ambao wameomba ajira tuliangalie upya kwa sababu mamlaka pia za kidola zipo kama TAKUKURU ili kutoa misingi hii ya upendeleo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais lakini pia kwa kushirikiana na *Chief Whip* mtaangalia huko baadae pengine siyo kwa Bunge hili kwa sababu mko sasa katika hizo ajira ambazo ndiyo zimetangazwa lakini ni muhimu pengine Wabunge tukaelewa ule ujumla wake mambo haya huwa yanafanywaje. *(Makofi)*

Ili iwe rahisi hata kuwaelekeza wale tunaowawakilisha kwamba mfumo unaenda hivi na hivi na hivi na mtu akikosa tunakuwa tunajua kwa sababu la sivyo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba watu wote waliokuwa wanajitolea na wanafanya kazi hizo hizo na wanapaswa kuajiriwa kwa ajili ya kazi hizo hizo halafu wote wamekosa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, pamoja na idadi na nini nafikiri ni muhimu tukielewa namna mfumo unavyofanya kazi itatusaidia sana sisi kuweza kuwaeleza wananchi kama wawakilishi wao kuwaeleza mifumo inavyokwenda na watu ili warudishe hiyo imani badala ya kuweka kwenye vikaratasi waweke imani mioyoni mwao kwa Serikali yao kuhusu ajira. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Furaha Ntengo Matondo atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mheshimiwa Aida Kenani ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia katika Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema lakini kunipa ridhaa na kibali cha kuweza kusimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikushukuru wewe mwenyewe kwa kazi yako nzuri ya weledi ya kuliendesha Bunge hili lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri kaka yangu Simbachawene, nimshukuru pia Naibu Waziri kaka yangu kwa kazi kubwa ambazo anazifanya. Katibu Mkuu na timu yao nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwa wananchi wa Tanzania kuhakikisha wananchi wako salama na wanafanya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuagiza watumishi wote walioondolewa kwenye utumishi wa umma kuweza kupata mafao yao. Ni jambo ambalo ni zuri sana kwa watumishi wetu ambao waliachishwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nipende kumshukuru Mheshimiwa Rais kuagiza watumishi ambao walikaa zaidi ya miaka mitano bila kupandishwa madaraja kuweza kupandishwa madaraja. Ninamshukuru sana sana kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea tena kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa juzi tu kutangaza ajira nyingi, ajira 21,200 kwa vijana wetu wa Tanzania. Kwa kweli ni jambo kubwa kwa sababu ni muda mrefu ajira zilikuwa hazijatangazwa. Ajira hii ni kada ya afya na kada ya elimu. Ajira 13,130 kwa kada ya elimu, lakini tuna ajira 8,070 kwa

kada ya afya. Ni jambo kubwa na ni jambo la kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda niongelee katika Mkoa wangu wa Mwanza. Katika Mkoa wangu wa Mwanza, walimu wa shule ya msingi tunauhitaji wa walimu 19,842. Walimu waliopo ni 12,529, tuna uhitaji wa walimu 7,313.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuajiri lakini tunaona ni jinsi gani changamoto ya ajira ilivyokuwa kubwa katika nchi yetu. Huu ni Mkoa tu mmoja wa Mwanza ambao shule za msingi tuna uhitaji wa walimu 7,313. Unaona ni jinsi gani hata weledi wa watoto wetu kupata elimu inakuwa ni changamoto kwa sababu ya walimu ambao bado ni wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo, walimu wetu wa sekondari kwa maana ya sayansi tunao wachache sana. Kwa Mkoa wangu wa Mwanza uhitaji ni 3,750 lakini walimu tulionao ni 1,731. Upungufu tuna 2,019. Unaona ni jinsi gani changamoto ya walimu wetu wa sayansi katika Mkoa ilivyo ni kubwa. Hii inaonyesha wazi tutakuja kukosa vijana wetu madaktari lakini pia tutakosa ma-*engineer,* hata watu ambao wanatusaidia kwa maana ya kada muhimu kama hii kuweza kuwa na shida. Kwa hiyo, nizidi kuiomba Serikali yangu tukufu pamoja na kwamba ajira zimetolewa lakini ione changamoto hii tunaweza kwenda kuitatua vipi kwa kuongeza watumishi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Mwanza tuna changamoto kubwa sana tena kwa watu wa afya. Watumishi tulionao, waliopo ni 3,411; wanaohitajika ni 10,136 lakini upungufu tuna watumishi 6,975. Huo ni mkoa mmoja tu na tumeajiri 8,070. Utaona ni jinsi gani tuna mahitaji makubwa ya wataalam wetu, madaktari wetu. Tunajenga vituo vya afya lakini tunajenga zahanati. Bila kupata wataalam hawa

tutakwenda kufanya kazi gani katika hizo zahanati zetu na vituo vya afya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizidi kuiomba Serikali yangu tukufu iweze kuliona hili changamoto ni kubwa. Tusije tukajenga majengo yakaja kuishia kwenye popo tu. Bila kupata wataalam hatuwezi kufanya kitu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yangu iendelee na mkakati huu maalum ambao wanao wa kuweza kuendeleza wataalamu wetu ili angalau tuweze kuendana na kasi ya wananchi wetu tuliopo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongee kidogo kuhusu suala la wastaafu wetu. Wafanyakazi wetu wanaajiriwa. Anaajiriwa mtu akiwa na miaka 20, anaajiriwa kwenye Mfumo wa *LAWSON* wote wanajua wanaingia mle lakini hata kabla hajastaafu, ndani ya miezi sita anaandika barua ya kustaafu lakini inakuja kufika kipindi anatakiwa kustaafu, anaanza kuambiwa mfumo wako hauonekani vizuri, mara barua zako hazionekani. Tuliwezaje kumlipa huyu mtu mshahara wakati anafanya kazi kama barua zake hazikuwemo kwenye mfumo? Tuliwezaje kuwa na huyu mtu miaka 20,30 kazini kama tulikuwa tunajua ana matatizo? Wazee wetu wamehangaika sana. Walipata changamoto kubwa sana, walimu shule zilikuwa ni mbali, mtu anatembea kwa baiskeli kwa mwendo mrefu saa 10 usiku anaamka. Inakuja kufika mwisho ameishiwa nguvu anaanza kuambiwa barua zako hazionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaumiza sana, tuone ni jinsi gani tutaendelea kuwasaidia wazee wetu waliotufikisha hapa kuweza kuwaachia maisha yao ya baadaye yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali yangu kwa kuleta Mfumo mzuri wa *TASAF* kwa ajili ya kupunguza

umasikini kwenye kaya zetu. Mfumo wa *TASAF* ni mzuri sana na ninaupongeza sana lakini changamoto iliyopo kwa wananchi wetu ni kukosa elimu.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali yangu tukufu kuona kuna haja sasa ya kuwapelekea wananchi wetu elimu, waweze kujua nini maana ya *TASAF*? Pia waweze kujua *TASAF* ina malengo gani kwao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** ...Waweze kutambua taratibu zake zikoje kwa wananchi na walengwa ni watu wa namna gani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Furaha Matondo kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge ya kukubaliana naye kwamba Mfumo ama *program* ya Mradi wa *TASAF* ni mradi muhimu sana na unahitaji elimu na jambo hili lilithibitishwa pia na Diwani wa Chama cha CHADEMA katika Kata moja ya Masasi Mjini alipokuwa anaishukuru Serikali kwa kazi nzuri iliyofanywa na *Program* ya *TASAF* katika kata yake ya CHADEMA pale Masasi Mjini na akaomba elimu itolewe nchi nzima, Watanzania wote ikiwemo vyama vyote vya siasa waelewe mradi huu wa *TASAF* ulivyo mzuri na unavyosaidia wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo unamfahamu huyo Diwani jina lake ili Mheshimiwa Waziri…

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa ngoja, subiri. Mheshimiwa Tunza Malapo unalifahamu jina la huyo Diwani?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, hapana simfahamu.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Furaha Matondo unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Waziri?

**MHE. FURAHA N. MATONDO:** Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo ninaipokea kwa sababu *TASAF* wanafanya kazi nzuri, changamoto ilikuwa ni elimu tu kama alivyosema. Kwa hiyo, niombe wananchi wetu waweze kupata elimu waweze kujua nini misingi ya *TASAF* lakini taratibu zake zikoje kwa wananchi na walengwa ni watu wa namna gani?

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kweli mikutano inaitishwa na watu wanaitwa lakini wengine hawawezi kuhudhuria maana hawaelewi nini maana ya *TASAF*. Licha ya hivyo, kuna wazee wengine ambao familia zao vijana na watu wanaowazunguka wanauwezo wa kufanya kazi. Kwa hiyo, wananchi wengi hawajui ni kitu gani kinatakiwa kwa wale baba zetu na ndugu zetu walioko kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo naomba niseme kidogo tena kwenye changamoto iliyopo kwenye ajira zetu. Kuna nyumba watu wako wanne, ameanza kuomba ajira wa kwanza huu ni mwaka wa tano mpaka wa sita lakini mpaka na wadogo zake wamekuja kusoma wamekuwa watu wanne wanasomeshwa kwa shida lakini mpaka leo hawajapata ajira. Kila wakiingia kwenye mfumo kuomba ajira, ajira zikitoka hawamo. Inaumiza, ni kweli Wabunge tuliomba humu wote wala siyo wachache, simu zetu zimejaa kuombwa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wabunge unajua kabisa ni jinsi gani hatuwezi kuajiri lakini tunajua mfumo wetu ni mfumo ambao unatenda haki. Basi ukatende haki kwa wananchi wetu. Kama ambavyo tumesema changamoto kubwa iliyoko hata kwenye Mkoa wangu wa Mwanza, tuna vijana wengi ambao hawajaajiriwa. Wamemaliza wana zaidi ya miaka mitano, miaka sita wanahitaji ajira lakini mpaka leo ajira hazijapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuombe sasa haki ikatendeke, vijana wetu waweze kupata ajira. Changamoto iliyopo iweze kupatikana. Mkate tunaoupata tuweze kugawana wote *ratio* sawa. Mikoa mingi tuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naunga mkono hoja, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Joseph Kenani, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ajiandae.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote kwa vile Wizara hii iko chini ya Ofisi ya Rais mwenyewe, nichukue nafasi hii kumpongeza sana na kumshukuru kwa ajili ya kazi kubwa, mageuzi makubwa yanayofanyika katika sekta hii ya utumishi na hata sekta ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna anayebisha kwamba yako mageuzi makubwa ambayo yamefanyika ndani ya muda mfupi katika maeneo hayo yote mawili. Watanzania wanaona na hata dunia nzima inaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Waheshimiwa hawa nikianza na Mheshimiwa George Simbachawene pamoja na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete kwa kuaminiwa kuongoza

Wizara hii nyeti. Ni wanasheria na mawakili wabobezi lakini nakwepa kuwaita wasomi kwa sababu historia inaonyesha kwamba suala hili la wanasheria kuitwa wasomi ilitengenezwa kwa ajili ya mahakamani ili kutawala zile nyongo zao na nini na kuheshimiana wakati mambo yanapokuwa makali kwenye mabishano. Sasa mnapotuita wasomi huku nje kuna kaujanja hapa mnataka kututenga na mambo fulani fulani mazuri, tumeshtuka tunaanza kukataa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la utumishi changamoto ambazo Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezizungumza katika maeneo yao pia zipo katika Jimbo letu la Mwanga hasa katika sekta ya elimu na afya. Upungufu ni mkubwa na changamoto zote zilizozungumzwa zipo. Naungana na wale ambao wameshauri kwamba pamoja na vigezo vizuri ambavyo TAMISEMI imeviweka katika kuajiri kama vilivyozungumzwa na Mheshimiwa Waziri katika Bunge hili, bado kile kigezo cha wanaojitolea ni kigezo cha muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, unaweza ukakuta hizi kazi za ualimu hasa ualimu na afya pamoja na kwamba ni kazi za mshahara lakini ni kazi za wito. Mtu anaweza akawa alimaliza 2015 akaomba ajira, alipoikosa akaenda kufanya shughuli zake. Leo 2022 nafasi zimetoka anaomba, tunasema kwa vile ni wa 2015 tumpe lakini yuko mwingine ambaye amehitimu 2018 akakosa ajira lakini akajitolea mpaka leo. Kwangu mimi huyu ndiye mwalimu au mhudumu wa afya mwenye wito kwa hiyo apewe kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko suala la *ATCL* ambalo nimeona kwamba kamati imeshauri kwamba Serikali iiondolee mzigo Wakala wa Ndege za Serikali mzigo wa kumiliki hizi ndege za biashara ambazo zinaendeshwa na *ATCL*. Wazo hilo ni zuri lakini naamini kabisa kwamba utekelezaji wake ni wa kiufundi sana ambao unahitaji makamati makubwa makubwa ya

wataalamu waliobobea katika fani mbalimbali. Nachangia kwenye eneo hilo kama kuchochea tu kufikiri ili Serikali ione umuhimu wa kulikabili jambo hili kwa utaalamu wa hali ya juu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kumbukumbu zangu ziko sawa, nikikumubuka Hotuba ya aliyekuwa Waziri wa sekta hiyo, Dkt. Harrison Mwakyembe kipindi fulani ambapo aliwashambulia sana watu walioingiza fedha kwenye akaunti ya *ATCL* ilihali wakijua kwamba kuna madeni. Nadhani utaratibu huu wa kuzinunua hizi ndege kupitia wakala wa ndege za Serikali umesaidia katika kutibu hili jambo kwamba *ATCL* imepata muda wa kupumua kuweka mambo yake sawa kabla haijaingia kwenye biashara hii nyeti ya kumiliki na kuendesha ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili limetuokoa katika madeni ya *ATCL* hasa yale ya ndani kwa sababu sheria yetu hairuhusu kukamata mali za Serikali katika kutekeleza hukumu.

Mheshimiwa Spika, sasa katika madeni haya ya nje hasa yanayotokana na maamuzi ya mahakama za kimataifa imeonekana kwamba sasa ndiyo tumeizamisha huko ndiyo maana baadhi ya ndege zetu kwa taarifa zinazokuja ni kwamba zimekamatwa na pia hatujui kwamba na hizi ambazo hazijakamatwa ziko salama au ziko namna gani kwa sababu suala la kushtakiwa na kuwa na hukumu ambazo ni dhidi yetu ni suala la kawaida tu kwa sababu kama nchi inakuwa inaingia kwenye mikataba inafanya mambo makubwa haiwezekani ikakaa tu bila kukabiliana na majanga kama hayo ya kesi. Kwa hiyo, hatuwezi kukwepa, dawa yake ni kuangalia jinsi ya kulinda mali zetu katika matatizo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tufanye nini? Mimi ushauri wangu, muundo wa *ATCL* mpango wake wa uwekezaji

pamoja na masuala ya madeni yapitiwe upya kitaalamu. Ikiwezekana tufanye, sasa naomba kutumia lugha ya Kingereza, tufanye *restructuring* ya madeni yake kwa kupitia benki. Baada ya kufanya hivyo, yatakayoonekana kwamba bado ni madeni au ni fedha ambazo tunahitaji kwa uwekezaji tukope kwenye benki. Tunaweza kutumia benki yetu kama *TIB.* Tukope kwenye benki halafu tu-*charge assets* zote za *ATCL* kwenye benki katika maana kwamba tuweke rehani *assets* zote kwenye benki. Tukifika hapo maana yake ni kwamba hizi *assets* zitakuwa zinamilikiwa na benki. Kwa hiyo, hakuna anayezidai wa ndani wala wa nje wala anyeidai Serikali ambaye anaweza akagusa mali hizi kwa sababu zitakuwa zinamilikiwa na benki.

Mheshimiwa Spika, nadhani hii ni njia mojawapo ambayo ikifanyiwa kazi kitaalam inaweza ikatufikisha katika utatuzi wa tatizo hili la *ATCL* ambalo tumelia nalo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimejaribu kuangalia mashirika mengine ya ndege, umiliki wake uko namna gani. *Kenya Airways* kwa takwimu zilizoko kwenye mitandao na tovuti zao za 2022, za mwaka jana, 48.9% ndiyo inayomilikiwa na Serikali na katika hizi 48.9%, 38.1% inamilikiwa na fungamano *(consortium)* ya mabenki ambayo yameikopesha *KQ.* Kwa hiyo, utakuta zaidi ya 51% haimilikiwi na Serikali. Ukija *South African Airways,* 51% inashikiliwa na fungamano la makampuni *(consortium)* inayoitwa *TAKATSO,* 51%.

Mheshimiwa Spika, *Rwanda airways* yeye alikuwa anamilikiwa na Serikali lakini mwaka jana kuna mazungumzo yalikuwa yanaendelea, sijapata matokeo yake ya mwisho, walikuwa wanakusidia kuuza asilimia 49 kwa *Qatar airways*.

Mheshimiwa Spika, British Airways wakongwe wenyewe wanamilikiwa na *Parent Company* inaitwa *International Airline Group,* asillimia 25.1 hii *Parent Company* inamilikiwa na

Qatar Airways. Ninachosema ni nini? tukitoa asilimia 51 ya hisa za *ATCL* ikawa haimilikiwi na Serikali ina maana kampuni hii haitakuwa ya Serikali kwa sababu *majority share*…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, *private,* kwa hiyo hii itasaidia…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:…** hakuna atakayeweza kuikamata ndege zetu kwa ajili ya madeni ya Serikali kwa sababu mmiliki hatakuwa Serikali katika maana ya *majority shareholding.* Na suala la kumiliki…

**SPIKA:** Mheshimiwa Tadayo kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

**TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, taarifa kuchagiza tu kidogo, Indian Airways ambayo imebeba jina la nchi inamilikiwa kwa asilimia 100 na Kampuni binafsi ya *TATA*, kwa hiyo nakubaliana na wewe kwamba haya mambo lazima tuyafikirie na kuyachakata. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tadayo unapokea taarifa hiyo.

**MHE. JOSEPH A. TADAYO:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo mimi nilizozifanyia utafiti Indian Airways haikuwa mojawapo lakini mimi ninaona fahari kwamba *airline* yetu imefufuliwa *in the National Carrier.* Wakati ulikuwa ukisafiri kwenda hata Nairobi au Ethiopia ukiangalia ndege zao zimepangwa pale *National Carrier* kama ng'ombe wa Mmasai halafu sisi tulikuwa hatuna ndege ilikuwa ni jambo la kusikitisha. Kwa hiyo huu ni mchakato ni mzuri, nakubaliana

na hiyo taarifa; lakini tuendelee kufanya mchakato wa kulinda na kuokoa ndege zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata suala zima la kumilikiwa hizi ndege na Wakala wa Serikali nadhani kuna *benefit* zingine ambazo tulikosa. Kwa mfano kuna taasisi inaitwa *International Civil Aviation Organization (ICAO)* ambayo inashughulikia mambo ya kufanya tathmini zinapotokea ajali za ndege, mambo ya bima na vitu vingine vingi sana. Sasa sidhani kama ile taasisi inaweza ika-*admit* ndege ambazo zinamilikiwa na Serikali kwa sababu ile ni *purely* kwenye mambo ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wangu nafikiri bado dakika chache naomba tu nizungumzie suala moja tu juu ya sekta ya utoaji haki. Naipongeza sana Serikali kwa uwekezaji mkubwa katika sekta ya utoaji haki hasa kwa mfano katika eneo la Idara ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, majengo haya mazuri na *facility* zingine bado hazitaweza kutufikisha tunapotaka, kama sheria zetu za *procedure* hatujazibadilisha. Mwalimu wangu Marehemu Dkt. Lamwai Mungu amlaze mahali pema, aliwahi kuniambia kwamba kila mtu anajua haki yake lakini jinsi ya kuipata ndio ambayo watu hawafahamu. Kwa hiyo tusiporahisisha sheria zetu hizi katika kupata haki mbalimbali bado sheria zitakuwepo pale zinatupa haki lakini jinsi ya kuifikia inakuwa changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kengele imegonga nisiendelee sana kwenye hilo naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa; Aida Joseph Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi niweze kuchangia, ieleweke tu kwamba tunayokuwa tunayazungumza mengi ni kwenye kuboresha na sio tuchukulie kwa nia mbaya.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na suala la *TASAF*. Nimeuliza swali asubuhi hapa, natambua kwamba miongoni mwa wananchi walionichagua mimi wapo ambao ni wanufaika wa *TASAF* na wapo ambao wana-*enjoy* na hili jambo, lakini nataka niboreshe kidogo.

Mheshimiwa Spika, nia inaweza ikawa njema, na kwa sababu si Mawaziri wanaoshuka chini kwenda kukutana na wanufaika, *approach* inayotumika kwanza kuwapata wanufaika ina changamoto nyingi sana; na tusikwepe kwamba hilo jambo halipo wakati lipo. Leo tunapozungumza Wenyeviti wa Serikali waliokabidhiwa hilo jukumu, nchi nzima ni wa Chama cha Mapinduzi. Wanavyokuwa wanakwenda hawaitishi mikutano kama ambavyo mwongozo umesema, walipita na madaftari yao, wanaona hii nyumba huyu mtu ni CHADEMA hawapiti wanaenda nyumba nyingine, na ikitokea aliingia kwa bahati mbaya lazima uenguliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi fedha lazima ziende kwa nia iliyokusudiwa na tusikwepe hapa kwamba sio la kisiasa lipo. Mimi ninayezungumza nimeshazungumza kwenye Baraza la Madiwani…

**SPIKA:** Mheshimiwa kwa sababu hilo jambo nimeshalieleza hapa mbele, wewe niletee majina ya hao wananchi wako ambao ni wa CHADEMA waliokosa kwa sababu ya chama chako; niletee hayo majina. Kwa sababu na wa CCM wamesema na kwao wamekosa sijui kama wale waliokosa pia ni wa CHADEMA, ila wewe kwa sababu umesisitiza kwenye hoja hiyo niletee majina ya hao ambao wamekosa kwa sababu ya CHADEMA. Ukishaniletea hayo majina mimi nitachukua hatua. *(Makofi)*

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nimesema miongoni mwa changamoto zilizojitokeza kwenye kuwapata wanufaika suala la ubaguzi wa kisiasa lilikuwepo, jambo…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Kama lilikuwepo si ndio utaniletea majina.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, sawa nitakuletea.

**SPIKA:** Wewe niletee majina ya wapiga kura wako wa Jimbo la Nkasi Kaskazini walionyimwa *TASAF* kwa sababu ni CHADEMA, niletee hayo majina ili mimi nichukue hatua. *(Makofi)*

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nitafanya hivyo kwa maslahi mapana…

**SPIKA:** Mheshimiwa Agness Marwa kwa sababu niliyekuwa nazungumza ni mimi ukisema taarifa wakati mimi naongea ni kama unanipa taarifa mimi. Kwa hiyo, inabidi usubiri aanze kuchangia muhusika halafu ndipo uombe taarifa. Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nitambue kwamba aliyekuwa Naibu Waziri wa Wizara hii Mheshimiwa Deo alifika mpaka Nkasi na alikutana na hayo mambo na akasema wanakwenda kufanya utaratibu wa kupitia upya…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Aida, mimi nimekaa hapa mbele, unataka kusemaje? Kama mlishamalizana na

Mheshimiwa Waziri basi agizo langu linaisha na huo mchango wako ninauondoa kwa sababu ndio hoja niliyokuwa naongea na Mheshimiwa Lwehikila hapo, sasa na wewe unarejesha hiyo hiyo. Nakwambia niletee ushahidi ili nichukue hatua unasema Naibu Waziri alikuja kama tatizo halikwisha?

Kama Naibu Waziri alikuja na tatizo halijaisha mimi nakwambia nikusaidie bado unang'ang'ania hivyo sasa unataka mimi nikusaidieje? Kama huna ushahidi ondoa hayo maneno, kama unao ushahidi niletee ili Bunge lianze kuchukua hatua, kwa sababu kuna watu wanaonewa kwa sababu ya vyama vyao. Kama huna ushahidi kwa usalama wako ondoa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kama unao ushahidi niletee ili Bunge lichukue hatua kwa watu kuonesha upendeleo kwenye kupewa *TASAF,* ndio hoja iliyoko hapa mezani. Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nategemea muda wangu unalindwa pamoja na maboresho na majina nitaleta…

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Kombo mpe nafasi achangie halafu ndio utampa taarifa.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, haya ahsante.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema hiyo kuna masuala ambayo yanaendelea ya watu kufanya kazi ambao ni wanufaika wa *TASAF,* ningeomba Wizara iweke utaratibu huo vizuri, wananchi waeleweshwe vizuri. Kama ni vibarua kama vibarua wengine basi lisiwekwe kama wanufaika ili watu wakafanye kazi, kwa sababu wanahitaji kufanya kazi, kwa sababu wale wanufaika kuna wazee, wanafunzi, watu wenye ulemavu ambao hawawezi

kufanya hizo kazi. Kwa hiyo, sura inayokwenda huko kwenye jamii yaani *as if* kwamba wote ambao ni wanufaika wanatakiwa kufanya hiyo kazi ya vibarua ambao kwa siku ni shilingi 3,000 jambo ambalo si sawa. Kwa hiyo, kama kuna maboresho ya hilo jambo au elimu basi itolewe vizuri ili nia ya hilo jambo ieleweke.

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye utumishi. Changamoto ya watumishi ni kubwa sana…

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani kwanza alisimama Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa.

**TAARIFA**

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana nilitaka kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba anapaswa ajue kwamba hasa jimboni kwake hakuna ubaguzi wa vyama, na ingekuwa kuna ubaguzi wa vyama yeye asingechaguliwa na asingekuwa Mbunge wa jimbo leo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa sijajua hiyo taarifa inaelekea kwenye hoja gani ya Mheshimiwa Aida Khenani, lakini kanuni zinataka nikuulize Mheshimiwa Aida Khenani unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, hiyo taarifa nilikuwa nimeshamaliza nimeingia kwa watumishi na naomba niendelee.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya watumishi…

**SPIKA:** Mheshimiwa Kombo.

**TAARIFA**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa tu dada yangu kwamba mimi hata kule jimboni kwangu kuna Mwenyekiti wangu wa Tawi wa Chama cha Mapinduzi ana sifa za kuingia kwenye mpango na amekuja kunilalamikia mpaka leo hajaingia. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kumwambia kwamba hili haliko kisiasa, ni kila mwenye sifa ndio anaingia, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa sasa kwenye hilo wacha nimsaidie yeye kasema anao ushahidi akishaniletea mimi ndipo tutachukua hatua kuanzia hapo. Mheshimiwa Aida Khenani malizia mchango wako.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kuna mambo tunatoana kwenye reli kidogo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya watumishi ni makubwa sana nchini pamoja na kwamba tunatofautiana. Mahitaji ya watumishi Wilaya ya Nkasi ni 3,946 walioko ni 2,071 upungufu ni 1,265.

Mheshimiwa Spika, kipindi cha nyuma walikuwa wanajua watu wakipelekwa Nkasi ni sehemu ya adhabu na wengi walikuwa wanakimbia, lakini tunatakiwa tuondoje hiyo dhana kwamba ile si sehemu ya adhabu? Ni kutofautisha hawa watumishi wanaokwenda huku wapewe motisha ili waone na wao ni watumishi kama maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, leo ukiangalia miongoni mwa mikoa ambayo ilikuwa nyuma kielimu ni pamoja na Mkoa wa Rukwa, lakini utakuta kuna shule ambazo hakuna mwalimu wa kike kabisa wakati hapo tunategemea tupate akina Samia wengine kutoka Nkasi, wakina Tulia Ackson wengine kutoka Nkasi, wakina Aida wengine kutoka Nkasi. Sasa unawapataje wakati hiyo shule haina mwalimu wa kike? Kwa

hiyo, hata yale mambo mengine ambayo mtoto wa kike anaweza akatengenezewa mazingira rafiki ili kufikia malengo yanakuwa hayafanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna watumishi ambao wamekuwa wanakaimu kwa muda mrefu kinyume na utaratibu. Aidha, ni Wakurugenzi kutokujua kwamba mtu anatakiwa akaimu kwa kibali cha Katibu Mkuu au kwa makusudi. Kwa hiyo, anapokuja anatafuta haki zake kwamba mbona nimekaimu muda mrefu unakuta kwamba kukaimu kwake ni kinyume na utaratibu. Kwa hiyo, mambo hayo niwaombe Wizara, ni vizuri pia wanapopata taarifa za kila wakati wawe wanajua ni wangapi wanakaimu na wamekaimu kwa muda gani na je, wamekaimu kwa mujibu wa sheria ama la.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la maadili kwa watumishi; nimeona Mbunge mwenzangu alikuwa anazungumza hapo kwamba imefikia mahali sasa tumejenga hofu sio kufata sheria tena, hofu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mtumishi anaweza akawa mfanyabiashara na anaweza akawa mkulima, haimzuii yeye kuwa mtumishi kwamba hawezi kufanya biashara nyingine za kumuingizia kipato. Nini kinatokea hapo? Aidha, ni suala la uwazi ndio imekuwa shida kwa Watanzania au ni hofu imetawala zaidi kuliko suala la uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapaswa kujua kwamba pamoja na changamoto nyingi ambazo zinawakabili watumishi, watumishi hawa wanaweza kufanya shughuli nyingine isipokuwa zisiathiri zile shughuli zao za kiutumishi na lengo litakuwa ni jema tu ili waendeleze maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda niingie kwenye utawala bora; tunapozungumzia utawala bora

tunazungumzia utawala wa sheria, demokrasia na uwazi. Hivi ninavyozungumza nimeona hata taarifa zinazokuja hapa; mimi ni Mbunge wa kuchaguliwa na wananchi. Hapa nazungumza Mbunge wako, Wakuu wa Idara wote na watumishi wote wa Wilaya ya Nkasi wamepigwa marufuku na Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kutokunipa ushirikiano wa aina yoyote. Mimi ni Mtanzania na ni Mbunge na najua ofisi inajua. Hapa ndani Bungeni nimezungumza leo ni mara ya tatu.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua huu ni utaratibu wa wapi, kwa nini tuwapangie watu wamchague mtu fulani ndio apewe ushirikiano, hawa watumishi ni wa Serikali. Wana-Nkasi na wao ni miongoni mwa Watanzania wengine ambao wanatakiwa kupata huduma. Ninapokuwa ninatengwa leo mimi Serikali inajua. Nilishaandika barua kwa Waziri mara kadhaa hakuna kitu kinafanyika. Huo utawala bora tunauzungumza hapa, kama tumeamua kutokukubali mfumo wa vyama vingi mtoke kwenye huo mfumo kuliko haya yanayoendelea leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inaumiza wakati mwingine, leo tunawanyima haki Wana-Nkasi kwa sababu za *interest*. Natamani Serikali iniambie leo kwamba wanajua taarifa hizo, na kama wanajua ni maelekezo yao, na kama si ya kwao wamechukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge, natakiwa nipewe haki zangu zote kama Mbunge kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida umesema umepeleka barua, umepeleka barua ya malalamiko wapi?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nimepeleka kwa Katibu Mkuu, TAMISEMI, nimepeleka kwa Waziri mwenyewe amepewa nakala, lakini Mkuu wa Mkoa

mwenyewe nilianza kumlalamikia kwa Mkuu wa Wilaya kwamba yeye ni Mkuu wa Mkoa achukue hatua, hakuna chochote kilichofanyika mpaka leo, ni mwaka wa tatu sasa.

**SPIKA:** Jamani jambo zito hili linaloonesha kwamba kuna ubaguzi. Japo nina maswali mengi, lakini sina haja ya kuyauliza sasa, lakini Mheshimiwa Aida nimeshawahi kumsikia wakati akimpongeza hapa Rais kwamba maendeleo na kule kwake yanaenda; na kwa hatua anazozichukua Mheshimiwa Rais sidhani kama wateule wake wanaweza kutoa maagizo kama hayo ya kukataza ushirikiano na kiongozi aliyechaguliwa na wananchi. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu sina taarifa za kutosha hapa Mheshimiwa Aida na umesema uliandika barua TAMISEMI, nadhani Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alifuatilie hilo jambo, halafu mimi nitapata mrejesho kutoka kwa Mheshimiwa Aida Khenani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kama ni katazo kwa namna anavyolisema yeye maana yake ni katazo lililotolewa hadharani pahala, kwa hiyo pengine upo ushahidi, kwa sababu sidhani kama pengine una ziara halafu Mkuu wa Wilaya hajaja, halafu ukaona huo ndio ushirikiano ulionyimwa. Lakini kama ni katazo basi nadhani mtusaidie hizo taarifa, Mheshimiwa Aida Khenani utaniletea mrejesho. Nadhani tupeane mwishoni mwa wiki ijayo utaniletea huo mrejesho wa wewe kubaguliwa na viongozi walioteuliwa kwenye eneo lako la kazi.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim

Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Ofisi ya Rais – Utumishi, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Ofisi ya Rais – Utumishi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utumishi, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika kuboresha maisha ya wananchi na pia utayari wetu wa ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya kipindi cha bajeti 2022/2023, Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na Utawala Bora imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya utumishi na hasa kurudisha uwabikaji kazini iliopelekea ufanisi mkubwa hasa kwenye utekelezaji wa miradi. Jimbo la Mbeya Vijijini limenufaika kupitia miradi ya *TASAF* ambapo imebadilisha maisha ya wananchi katika vijiji husika. Pia kwa kusimamia vizuri, rushwa na upendeleo umepungua kwa kiasi kikubwa kupelekea ufanisi mkubwa sehemu za kazi na hata miradi kukamilika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, napendekeza kuendeleza mafunzo ili kuboresha weledi wa watumishi ikiwemo upanuzi wa Chuo cha Watumishi Mbeya na eneo muafaka kwa ujenzi wa chuo kipya na cha kisasa, ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambapo kuna maeneo mazuri ikiwemo yaliyokuwa

mashamba ya *Tanganyika Packers*, Mbalizi. Kuna mahitaji makubwa ya elimu/mafunzo ya uongozi kwa viongozi wa ngazi mbalimbali, napendekeza Serikali irudishe utaratibu wa mafunzo maalum ya viongozi kwa kushirikiana na Vyuo Vikuu ikiwemo Mzumbe, *UDSM, IFM* na hata nje ya nchi. Mafunzo yanahitajika ni kama vile *Executive Development Pragrammes* kwa viongozi kulingana na ngazi zao. Mafunzo nje ya nchi ni muhimu kwa kuleta ujuzi kutoka nje hasa nchi zilizoendelea na hata zile zinazoendelea na zinafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta mbalimbali, napendekeza Serikali iendelee kutoa ajira zaidi hasa kwenye maeneo ya kuchochea uchumi na pia sekta ya afya, elimu na kilimo. Kutokana na idadi kubwa ya wahitimu kukosa ajira, na wametapakaa kila kona ya Tanzania hasa vijijini, napendekeza Serikali kuhakikisha ajira zinatolewa kwa usawa wa maeneo yote ya Tanzania kulingana na sifa. Serikali iangalie kuboresha sera za kikodi ili zichochee kuongeza ajira pamoja na kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na majukumu na unyeti wa mashirika ya kadhaa ya umma ikiwemo ushindani wa kupata watalaam wazuri, mashirika haya yaruhusiwe moja kwa moja kutoa ajira ili yaendane na mahitaji yao na Tume ya Ajira wawe na jukumu la ushauri/udhibiti. Taasisi kama *CAG* kisheria anatakiwa awe huru ikiwemo uhuru wa kuajiri, na hata taasisi kama mabenki, *TANESCO*, Bandari, *TRA* ni muhimu wakapewa uhuru wa kuajiri kulingana sifa ila kupata watalaam wazuri kiushindani na pia kulingana na bajeti za mashirika husika.

Mheshimiwa, Spika, pamoja na maboresho ya mfumo wa *TASAF,* napendekeza pia kuboresha zaidi mfumo huo ikiwemo msukumo wa miradi ilenge maeneo yatakayochochea uzalishaji wa mali ili zisaidie jamii kwa upana mkubwa. Pamoja na maeneo ya uzalishaji, msukumo

ujumuishe kuimarisha masoko ya bidhaa zitakazozalishwa katika maeneo ya mradi. Miradi ilenge kuboresha elimu na hata kusomesha watoto wanaotoka kwenye kaya maskini ya maeneo husika. Serikali iboreshe taratibu za kupata maeneo ya miradi ya *TASAF* ili kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda niombe kuleta mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nilpongeze Serikali kwa ajira ambazo imetoa kwa kipindi cha miaka miwili, lakini nitoe ushauri kwenye ajira kama ifuatavyo:-

Kwanza imefika wakati sasa tujikite na kwenye ajira za kada ya uchumi, maafisa mipango, na kadhalika, hawa wamesahaulika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2020 Menejimenti ya Utumishi ya Umma walitoa kibali cha kuajiri wahandisi kuwa walimu wa shule za ufundi kama Ifunda, *Moshi Technical* na kadhalika. Vijana hawa 60 miundo ya ualimu hasa Tume ya Walimu haiwatambui hivyo hawana barua za ajira, hawawezi kuthibitishwa kazini. Niombe suala hili litafutiwe ufumbuzi.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi walivyosimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM 2020/2025. Kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Mbulu Mjini napenda kuchukua nafasi hii kwa jinsi tulivyotatua changamoto nyingi zilizoshindikana kwa zaidi ya miaka 20 kwa kupatikana fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mifano hiyo ni ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji la Endayaya Tlawi ambayo usanifu wake ulikamilika toka mwaka 2003 na sasa linajengwa kwa shilingi bilioni saba.

Pili, ujenzi wa barabara ya lami Karatu – Mbulu - Haydom ambayo ni ahadi ya Serikali ya Awamu ya Nne inayotekelezwa; tatu, ujenzi wa sekondari mpya katika Kata ambazo haziko, ujenzi wa vituo vya afya kikata; na nne, kupatikana kwa fedha za mfuko wa jimbo kwa ajili ya matengenezo ya barabara *TARURA* na fedha zingine nyingi.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mpango huu wa mapendekezo ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; kwanza Serikali itazame upya mfumo wake wa kujaza nafasi wazi za watumishi wanaostaafu, kwa mfano halmashauri yangu ya Mbulu Mjini kuna watumishi wengi waliostaafu toka mwaka 2015; mpaka sasa hakuna kibali cha ajira mbadala iliyotolewa hali inayopelekea halmashauri kubakiwa na maafisa kilimo watatu badala ya 54 na maafisa mifugo, uvuvi na ushirika kubakiwa watano badala ya 52. Mbaya zaidi hivi karibuni kuna mtumishi wa ajira mpya aliyepangwa mpaka leo hajaripoti, kwa hiyo, halmashauri yetu ina upungufu mkubwa sana wa watumishi, Serikali ichukue hatua za haraka.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali iangalie upya utaratibu wa kuwaingiza walengwa wa *TASAF* hasa wale walioko kwenye maombi ya rufaa; tatu, Serikali iangalie uwezekano wa kuingiza somo la uzalendo kuanzia elimu ya msingi hali itakayowaandaa kizazi cha Watanzania kitakachokuwa na uzalendo mkubwa kwa nchi yao. Nasema hayo kwa sababu ukipitia taarifa nyingi za *CAG* ni wazi kuwa kizazi chetu kinazidi kupoteza maadili na uzalendo; nan ne, Serikali ijaze nafasi zinazokaimiwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta zingine zijazwe au kuthibitisha wale wanaokaimu nafasi

hizo haraka ili kuboresha utendaji na uwajibikaji kwa watumishi wetu.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali iangalie uwezekano wa muda mzuri wa Bunge kujadili taarifa ya CAG mara itakapokabidhiwa kwa Mheshimiwa Rais ili kuondoa hisia nyingi za wananchi kama ilivyo sasa kujadiliwa mwezi Novemba kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake kwetu nyanja mbalimbali za ustawi wa kijamii, kiuchumi, kisiasa kidiplomasia na kutuepusha na majanga mengine mengi. Pia tunampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa mambo mengi sana katika kuiongoza nchi yetu na utekelezaji wa Ilani ya CCM 2025, kwa kweli sisi kama Wabunge wa CCM tuna mengi ya kujivunia kupitia Rais wetu, tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie ulinzi, baraka na mafanikio katika utume wake kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sekretarieti ya Ajira nchini ndiyo chombo pekee cha kufanya usaili wa ajira nchini ambapo nchi ina wahitimu wengi sana wanaotuma maombi ya nafasi ya ajira pindi tangazo litakapotolewa, Serikali iangalie uwezekano wa kuijengea uwezo wa fedha, magari na vitendea kazi mbalimbali ili usaili wa nafasi za kazi ufanyike kikanda hapa nchini kwa kuwa wanaofanikiwa ni wachache.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niongeze sehemu ya mchango wangu kupitia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbulu ni Wilaya kongwe hapa nchini, kwa sasa inakabiliwa na upungufu mkubwa wa miundombinu ya huduma hususan majengo ya taasisi mbalimbali, kwa hiyo toka mwaka 2005 serikali ilifungua ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Mbulu, toka muda huo mpaka leo

taasisi hiyo haina jengo la ofisi kwani walipangisha nyumba ya mtu binafsi ambayo ni ndogo sana na iliyojengwa kwa ramani ya makazi. Hivyo ninaiomba sana Serikali itujengee ofisi ya taasisi hiyo muhimu kwa maendeleo na ustawi wa jamii na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya utaratibu wa kuongeza malipo ya pensheni ya kila mwezi kwa watumishi wastaafu wa miaka ya nyuma kwa kuwa kiasi kinacholipwa kidogo sana ambayo haiwezi kumpatia hata bima kubwa, sote tunafahamu kundi hili linakabiliwa na maradhi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia moa moja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa George Simbachawene na Naibu wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pamoja na watendaji wa Serikali katika Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye utaratibu uliotumika mwaka 2020 kuhitimisha ajira na kusimamisha mishahara kwa watumishi wa Serikali Watanzania waliogombea nafasi za kisiasa (Ubunge) na madhara yake; na umuhimu wa Serikali kupitia upya sheria inayowafanya maprofesa kustaafu wakiwa na miaka 65 na kutokupata mikataba maalumu ya kuendelea kufundisha.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuhitimisha utumishi wa umma kwa kugombea nafasi za kisiasa umeanishwa kwenye Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa tarehe 2 Januari, 2015 unaohusu utaratibu kwa watumishi wa umma wanaogombea nyadhifa za kisiasa nchini. Waraka huo umefafanua utaratibu wa watumishi wote wa umma wenye nia ya kugombea nyadhifa za kisiasa kama ifuatavyo:-

Kwanza, mtumishi wa umma atakayeamua kugombea nafasi ya Ubunge wa kuchaguliwa, Viti Maalumu vya Ubunge au nyadhifa nyingine za kisiasa ataruhusiwa kufanya hivyo, baada ya Tume ya Uchaguzi kumtangaza kuwa mgombea wa Ubunge na atalazimika kuacha kazi na kulipwa mafao yake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliotumika ulikuwa tofauti na waraka ulivyoelekeza hapo juu. Serikali iliiagiza Hazina kutowalipa mshahara wa kuanzia mwezi Julai watumishi wake wote waliochukua fomu ya kugombea nafasi ya uongozi wa kisiasa kupitia vyama vya siasa. Siyo tu kuwa mishahara ilisimamishwa, bali baadhi ya waajiri walichukua hatua ya kuwaondoa kazini watumishi waliochukua fomu za kugombea uongozi wa kisiasa mara walipobainika kuchukua fomu za kugombea Ubunge.

Mheshimiwa Spika, watumishi wengi sana wenye uwezo walichukua fomu za kugombea Ubunge, na baada ya kunyimwa mishahara kwa kipindi cha kuchakata majina ya wagombea, hii ilisababisha hofu na usumbufu mkubwa. Watumishi wengi walichukua fomu wakijua kuwa kisheria hakuna shida kutia nia. Kitendo hiki kitatia hofu watumishi wa Serikali (hasa vijana) wenye uwezo wa kugombea katika chaguzi zijazo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyochangia kwa maandishi katika bajeti ya mwaka 2022/2023, katika vyuo vyetu vikuu vya Serikali, kuna changamoto kubwa ya tatizo la rasilimali watu likiwa limesababishwa kwa kiasi kikubwa na kitendo cha Serikali kubadilisha utaratibu wa maprofesa kuendelea kufundisha kwa mikataba maalumu hadi wanapofikisha umri wa miaka 70.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa miaka michache iliyopita, maprofesa wengi katika vyuo vya Serikali wamestaafu katika umri wa miaka 65 kwa mujibu wa

sheria. Katika vyuo vikuu vya Serikali kuna uhaba mkubwa wa walimu katika ngazi ya maprofesa na kwenye soko la ajira si rahisi kuwapata wataalamu wenye vipaji hivi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya rasilimali watu vyuo vikuu Tanzania inasababishwa pia na masharti magumu ya kuajiri wataalamu kutoka nje ya Tanzania. Kuajiri wataalamu kutoka nje kwenye maeneo ya kimkakati ni muhimu ili kutusaidia kwenye kukuza rasilimali yetu, na kutuunganisha na mifumo ya kimataifa. Upatikanaji wa vibali huchukua muda mrefu na husababisha walengwa kutoka nje kubadili mawazo na kuacha kuja kufanya kazi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea changamoto za hapo juu, naishauri Wizara yafuatayo:-

Kwanza, Serikali ifuate sheria na kanuni za kiutumishi kwenye masuala mbalimbali. Naishauri Serikali iwalipe mishahara iliyosimamishwa watumishi wote wa Serikali waliotia nia ya kugombea kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa tarehe 2 Januari, 2015 unaohusu utaratibu kwa watumishi wa umma wanaogombea nyadhifa za kisiasa nchini kwani hawakuvunja sheria wala kanuni kutia nia.

Pili, Wizara ya Utumishi na Utawala Bora itoe vibali vya kuajiri wanataaluma wa kutosha kuendana na idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. Hii ni pamoja na kuajiri wataalamu kutoka nje katika maeneo ya kimkakati kama yale ya sayansi, uhandisi na hesabu.

Tatu, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora wapitie sheria na kuongeza umri wa maprofesa kutumika kwa mikataba uanzie pale wanapostaafu wakiwa na miaka miaka 65 na waendelee hadi wanapofikisha miaka 75 au watakapokuwa hawana uwezo wa kufanya majukumu yao.

Hii haina hasara kwa Serikali kwani wanapostaafu mishahara yao inakuwa bado iko kwenye ikama.

Mheshimiwa Spika, kuwaandaa hawa wataalamu, Serikali hutumia gharama kubwa sana. Tunapositisha huduma zao, vyuo binafsi huwachukua bila gharama na kuwatumia kuwajengea sifa, ilhali vile vya Serikali vinadorora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri, ukurasa wa 28 Serikali imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 14,398 yenye jumla ya shilingi 25,655,898,954.61 hadi Machi, 2023. Vilevile madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 2,942 waliokoma utumishi wao yamelipwa, na kwamba kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Februari, 2021 hadi Machi, 2023 Serikali imelipa madai ya malimbikizo ya mishahara 119,098 yenye thamani ya shilingi 204,420,741,285.25.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili tukufu madai hayo inayosemekana yamelipwa yanatokana na kiasi gani kinachodaiwa na cha muda gani? Na kiasi gani bado hakijalipwa na kina muda gani? Hii inatokana ukweli kwamba bado madai ya watumishi ambayo hayajalipwa ni mengi na malalamiko yamekuwa mengi sana.

Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu ambalo Wakala wa Ndege za Serikali iliongezewa mwaka 2016 ni jukumu la kuratibu ununuzi wa ndege na kukodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL),* halikadhalika kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo kwa niaba ya Serikali. Ningependa kufahamu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 tunatarajia kutumia kiasi gani kwa ununuzi wa ndege? Lakini pia kumekuwepo na malalamiko toka *ATCL,* moja ya sababu

linalolifanya shirika husika kujiendesha kwa hasara ni mkataba mbovu wa ukodishaji na matengehezo ya ndege. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na hili na hatua gani inatarajia kulichukua kunusuru shirika letu la ndege?

Mheshimiwa Spika, naomba nipate ufafanuzi wa kina kwenye maeneo hayo mawili.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, kuna waliokuwa watumishi Serikalini mfano Magereza baada ya kustaafu wanapata malipo kidogo sana ya kila mwezi jambo ambalo linapelekea wastaafu hawa kuishi maisha magumu sana.

Mheshimiwa Spika, ombi lwangi; Serikali ipitie upya mafao ya wastaafu wetu ili wasidhalilike sana baada ya kustaafu

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa utendaji mwema, pamoja na changamoto kadhaa kama vile rasilimali watu na fedha kwa ujumla mnafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, nina mchango katika maeneo yafuatayo; kwanza ni kuhusu kulegeza masharti kwa watumishi wanaokaimu.

Mheshimiwa Spika, wapo watumishi ambao wanakaimu kwa dokezo na sio kwa barua ile ambayo inatoka Utumishi. Kwa mfano nina mwanasheria katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga, yeye alikuwa mwalimu akasoma sheria, na amekuwa msaada katika Halmashauri. Kwa mfano *Mafinga TC* imetokana na kugawanywa kwa Halmashauri mama ya Mufindi, bahati mbaya sana japo ndio utaratibu katika kugawana mali na madeni, *Mafinga TC* ilirithi migogoro mingi ya ardhi kutoka Halmashauri mama ya Mufindi ambayo ilikuwa migumu sana. Ni kweli kwamba ni

wajibu wa mwanasheria kutetea kesi za Serikali/Halmashauri, hata hivyo ameshiriki kuokoa Halmashauri kulipa mamilioni ya fedha ambayo ni kutokana na kesi za madai ya migogoro ya ardhi ambayo tulirithi kutoka Halmashauri mama ya Mufindi. Mwanasheria huyu alifanya kazi bega kwa bega na mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kesi za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, kwa vipindi vifupi tuliletewa mwanasheria kamili kuwa Mkuu wa Idara lakini hakukaa sana, kwa hiyo katika kipindi cha miaka takribani nane kutoka Julai, 2015 mwanasheria huyu amefanya kazi kwa miaka zaidi ya sita akiwa ni Mwanasheria Daraja la II.

Mheshimiwa Spika, ninaleta hoja hii kama *case study* ya suala la watumishi wanaokaimu kwa madokezo na hususani wale ambao wametokea katika kubadilishwa kada kwa maana ya *recategorization*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa kuwa mtumishi wa aina hii na wote wa aina, wamethibitisha uwezo katika kazi na kwa kuwa walishakuwa watumishi, napendekeza moja; wafanyiwe mserereko ili kuwasogeza kwenye ngazi ambayo wanaweza walau wakawa wanakaimu sio kwa dokezo bali kwa barua rasmi kutoka Utumishi, nasisitiza hili la Mwanasheria wa *Mafinga TC* nimelitumia kama mfano.

Mheshimiwa Spika, pili, kuwaachia mshahara binafsi watumishi waliofanyiwa *recategorization;* ninashauri, pale ambapo mtumishi amekidhi vigezo na kufanyiwa *recategorization,* nashauri ikiwa alikuwa amefikia *TGS F* kwa mfano lakini baada ya *recategorization* akarudi katika kada mpya kwa kuanzia daraja la kuingilia ambapo mara nyingi ni daraja la pili la kada husika, mshahara wake ubakie *TGS F* kuliko kurudi *TGS D.* Hii itasaidia sana kuwapa morali watumishi.

Mheshimiwa Spika, tatu, wastaafu kulipwa kwa wakati; lipo tatizo kubwa kwa watumishi wanapokaribia kustaafu au wakishastaafu hasa walimu. Kuna hali fulani kama ya kuwa *desperate* mtu anapoingia hatua ya kustaafu, wanakuwa na hofu kubwa, *stress* na mashaka kwamba je, nitalipwa kwa wakati au nitacheleweshewa kama mwenzangu fulani.

Mheshimiwa Spika, suala hili lipo zaidi kwa walimu, kiasi Mbunge kila mara unapokea simu au ghafla mwalimu mstaafu anakupigia anakuambia nipo Dodoma naomba nikuone nimekuja kufuatilia suala la mafao. Mara nyingi wakienda kwenye mifuko hupewa majibu mapokezi kwamba jambo lako linashughulikiwa, hii anaweza kujibiwa mara kadhaa na baadae anakata tamaa, anafunga safari anakuja Dodoma. Hili hujitokeza mara nyingi kama kwa mfano, kuna michango haikuwasilishwa kwa wakati, hufikia hatua mstaafu kuamua kujilipia ile tofauti kusudi tu mafao yake *yawe processed.* Nashauri tuwe na utaratibu mzuri zaidi wa kuandaa mafao ya wastaafu wetu kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, angalizo; nashauri suala la ajira libakie huko huko na kwa mfumo huu, suala la kusema mnagawa nafasi kwenda kwenye majimbo ni hatari, ni ugomvi kwetu Wabunge, fikiria jimbo lipate nafasi 20, wahitaji wako 200, wakikosa 180 lawama kwa Mbunge, sisi tubaki na kazi ya kushauri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejiment ya Utumishi wa Umma na Tawala Bora, Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nami ninaomba awali ya yote naomba nianze kumshukuru sana

Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia afya njema. Kwa kipekee kabisa nikushukuru wewe kwa jinsi ambavyo unaongoza Bunge letu hili, lakini kwa kweli pamoja na wote wanaokusaidia ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wetu, kwa hakika tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awajalie heri ili mambo yaendelee kuwa mazuri kama yalivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo niruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kama ambavyo nilimshukuru siku ya kwanza niliposimama baada ya kupata uteuzi wa kuja kuwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ninaendelea tena kumshukuru yeye kwa kuniamini pia naendelea kumwahidi kwamba nitachapa kazi kwa maarifa yangu yote na vipawa vyangu vyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu nimpongeze na kumshukuru sana *Comrade* wangu Waziri wangu Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge, kwa ushirikiano mzuri anaonipa mimi na wenzangu wote ndani ya wizara lakini kwa hakika uongozi wake, miongozo yake na michango yake kwa kweli inatufanya sisi ndani ya wizara kwenda katika *direction* nzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa kipekee kabisa niruhusu niwashukuru sana Makatibu wangu Wakuu wawili na Naibu Katibu Mkuu mmoja; hapa nakusudia kuzungumzia Ndugu Maendeka wa Katibu Mkuu Ikulu na Ndugu Juma Mkomi Katibu Mkuu Utumishi wa Umma na Ndugu Xavier Daudi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yetu. Kwa hakika ushirikiano wao umekuwa ni nguzo ya mafanikio katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, sio mwisho kwa umuhimu niruhusu nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mke wangu Mama Aziza na watoto wangu wote. Kwa hakika upendo wao na

kunivumilia kwao nikiwa nachapa kazi za umma ndio jambo moja ambalo linanisukuma kwenda mbele zaidi, pia bila kuwasahau wananchi wa Jimbo la Chalinze kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wananipa. Nataka niwahakikishie kwamba Mbunge wao nipo kazini na sijawasahau naendelea kuchapa kazi nikiendelea kuwapa heshima wana-Chalinze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba uniruhusu niingie kwenye hoja ambazo zimetajwa au zimeelezwa na Wabunge. Kwa kipekee kabisa nianze na hoja ambazo zimeelezwa na Kamati yako ya Bunge inayosimamia Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, katika moja ya hoja ambayo imeelezwa na kamati lakini pia na michango ya Wabunge ni hoja inayohusu eneo la *TASAF*. Ni hakika na ukweli kabisa maneno yote mazuri, michango yote mizuri iliyotolewa na Wabunge sisi kama Wizara kwanza nataka niwahakikishie Wabunge tunayachukua. Kwa sababu katika maelezo waliyoyatoa Waheshimiwa Wabunge yako baadhi ya maeneo ni kweli kwamba Wizara inakiri yanatakiwa yafanyike marekebisho, lakini pia yako baadhi ya maeneo wizara inakiri kwamba huenda kuna tatizo la taarifa au uaminifu wa watu wetu ambao tunawatuma kwenda kufanya kazi. Kwa hiyo nataka niwahakikishie Bunge lako, kwamba sisi kama Wizara yale maeneo yenye mapungufu tunakwenda kuyafanyia kazi pia yale maeneo ambayo yanatakiwa yaendelee kusisitizwa ni lazima tuendelee kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, liko eneo la utambuzi ambalo limelalamikiwa sana na mimi binafsi yangu nimshukuru sana Mheshimiwa Aida Khenani ambaye alichokoza hoja asubuhi wakati wa maswali ya msingi ndani ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo hili limekuwa na changamoto, lakini Serikali yako imekuwa kila mara inafanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba jambo hili linabadilika au linaboreka ili kuweza kuhakikisha wafaidika wa *TASAF* wanapata faida ya mradi huu. Katika miaka hii ya karibuni nataka nilihakikishie Bunge lako na nitoe taarifa kwamba Serikali imekuja na utaratibu wa kuelekeza Serikali zetu za Vijiji kuhakikisha kwamba mikutano ya vijiji inawakusanya watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikia yapo baadhi ya malalamiko juu ya siasa kuingizwa katika taratibu hizi. Nataka niwahakikishie Wabunge na hasa kwako, sisi kama Wizara tunalibeba hili jambo la mwingiliano au mgongano wa maslahi ya kisiasa na tutakwenda kulifanyia kazi ili kuondoa vilio vya Bunge lako. Pamoja na hilo pia baadhi ya Wabunge wamezungumza juu ya malipo madogo ya wafaidikaji wa *TASAF*. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie wananchi hawa kwamba, Serikali imefanya juhudi kubwa sana. Mwaka 2022 wakati tulipoanza mchakato wa mjadala wa kupitia tena mafanikio ya *TASAF,* hili jambo lilionekana na tulifanikiwa kupeleka ile pesa wanaolipwa wafaidikaji mpaka Sh.3,000, lakini ni kweli hali za maisha zimebadilika na hitajio la kuongeza linafanyika. Sasa ninapozungumza mchakato wa kujadili taarifa na kuthamini utekelezaji wa Mradi wa *TASAF,* awamu ya tatu, kipande cha pili unaendelea.

Mheshimiwa Spika, tutakapofanikiwa kumaliza uchambuzi huo, nataka nilihakikishie Bunge lako na Watanzania na wafaidikaji wa *TASAF* kwamba changamoto kama hizi ambazo zinaonekana ni moja ya jambo ambalo tunakwenda kulishughulikia na tutakuja kuleta mrejesho hapa ili wananchi na Wabunge wapate kuelewa kwamba Serikali yao ni sikivu na Mheshimiwa Rais, anaendelea kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka vilevile niwatoe wasiwasi ndugu zangu Watanzania, Mradi wa *TASAF* huu kwa kutegemea pesa zetu za ndani, siyo rahisi kuweza kuwafikia watu wote. Nchi yetu haiishi katika kisiwa, nchi yetu inashirikiana na nchi mbalimbali, wahisani mbalimbali ili kuhakikisha kwamba programu za maendeleo ya nchi na watu wake zinakwenda mbele. Hivyo, hawa watu wote au wadau wote tuliyowataja katika taarifa yetu ya mwanzo ni wazi kwamba wanatusaidia sana Watanzania ili tuweze kufikia miradi vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hilo, moja ya mafanikio makubwa tuliyoyapata ni sasa Mradi wa *TASAF* umeweza kufikia kaya zisizopungua 2,300 ambayo ndani yake ina wafaidikaji wasiopungua 5,200,000 ambao wao ni Watanzania wenye uhitaji ambao Serikali yao inaendelea kuwaangalia.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie kwamba, changamoto nyingine zote ikiwepo changamoto ya *NIDA* tutaendelea kuifanyia kazi na sisi tunaendelea na mazungumzo na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Idara husika inayohusika na Vitambulisho vya Taifa ili kuweza kuwafikia wananchi ilimradi waweze kufaidika na programu hii ya *TASAF*. Kwa wale ambao hawana vitambulisho vya *NIDA,* maelekezo yamekwishatolewa kwamba waende kwa sababu utambuzi wa kwanza ni katika ngazi yao ya kijiji tutawatambua na kuwaingiza katika mfumo ili waweze kuendelea kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo pia limezungumzwa jambo la ajira katika maeneo ya vyuo vikuu, aliyezungumza ni Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na nataka nikiri mbele ya Bunge lako kwamba, maelezo aliyotoa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo yana ukweli kabisa, nini kimefanyika na nini kimetufikisha hapo, kwa muda nisingependa nirudi huko, lakini Serikali ilishakutana na Uongozi wa Vyuo Vikuu vya

Umma wakiongozwa na *Dean* wao ambaye ni *Vice Chancellor* wa Chuo cha Ardhi kilichopo Dar es Salaam. Mazungumzo yamefanyika nimwombe Mheshimiwa Kitila Mkumbo na wenzake katika eneo la chuo kikuu watupe nafasi Serikali tupate kuangalia, nini zilikuwa sababu za kufika hapa tulipofika na nini kifanyike ili tuweze kuondoka hapa tulipofika twende mbele kwa kasi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie na Bunge lako kwamba si nia ya Serikali kuchukua mamlaka ya vyuo vikuu na kuyafanya ya kwake, lakini zipo kada mbalimbali, zipo kada za *administrations* au eneo la kiutawala, lakini pia zipo kada za Walimu au kwa maana ya Wakufunzi wetu. Kada hizi mbili *treatment* zake ni tofauti ndugu Watanzania. Kada ya *Administrations* imeendelea kubaki chini ya utumishi, lakini pia kada ya wale wenzetu ambao ni wakufunzi imeendelea kuratibiwa katika jicho la mbali, lakini mambo yote yanaendelea kufanyika ndani ya vyuo vikuu vyenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko jambo limezungumzwa na walio wengi juu ya malipo ya madai ya malimbikizo ya mishahara. Ni kweli zipo kazi na juhudi kubwa ambazo Mheshimiwa Rais wetu anazifanya katika kipindi cha miaka miwili zaidi ya Shilingi Bilioni 2.4 zimelipwa kwa wale ambao walikuwa wanadai malimbikizo. Hata hivyo ni kweli kama walivyosema, kwenye Taarifa ya *CAG* inaonyesha kwamba bado ile ada ya malipo imeendelea kupanda juu. Nataka nilihakikishie Bunge lako, katika kipindi cha miaka miwili Mheshimiwa Rais, ameweza kulipa nusu ya yale ambayo anayodaiwa.

Mheshimiwa Spika, lingine kubwa, nataka niliambie Bunge lako, Serikali hii imechaguliwa kawa kipindi cha miaka mitano. Tumpe nafasi Mheshimiwa Rais aweze kufanya, kama ndani ya miaka miwili ameweza kulipa nusu ya madeni yanayodaiwa, iweje ashindwe katika miaka mitatu iliyobakia! Nataka niwahakikishie kuwa, tunaye Rais ambaye

anawapenda na kuwajali watumishi wa umma, tunaye Rais ambaye anawapenda na kuwajali Watanzania katika hali zote. Tumpe nafasi Mheshimiwa Rais na sisi wasaidizi wake, nataka niwahakikishie kwamba madeni na malimbikizo yote wanayodai watumishi wa umma katika Tanzania tunakwenda kuyamaliza na kwenda kuyafikia yote katika maeneo yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile pamoja na hilo nataka nizungumzie juu ya uwiano wa watumishi wa umma katika vijiji na miji…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA.** Dakika tatu malizia muda wako, kengele mbili zilishagonga.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kupitia watalam tulionao wa TEHAMA mfumo kwa ajili ya kuchakata na kujua idadi ya watumishi katika maeneo yote ikiwemo mijini na vijijini umekamilika na unafanya kazi. Mfumo huo unatambulika kama *HR Assessment,* mfumo huu unawezesha siyo tu Serikali lakini pia hata Serikali za Mitaa kujua idadi ya wafanyakazi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kupitia mfumo huu, inatuwezesha sisi kuweza kupanga pia ikama za wafanyakazi katika maeneo hayo. Nataka niwahakikishie Watanzania na Bunge lako kwamba Serikali imejizatiti kimifumo kuhakikisha kwamba changamoto zote zilizopo katika maeneo haya tunazikabili na kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mengi ya kuzungumza, lakini naomba kwa ruhusa yako sasa nimkaribishe Mheshimiwa

Waziri ili aweze kuendelea hapa palipobakia. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nasubiri nimwone Mheshimiwa Waziri akisimama kwa mwaliko wa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa George Simbachawene, aje ahitimishe hoja yake.

Mheshimiwa Waziri samahani, kabla hujaanza kusoma, nililetewa ujumbe hapa na Mheshimiwa Dkt. Ndugulile kwamba kuna mgeni wake tulisahau kumtangaza, anaitwa Ndugu Abdu Msangi sijui kama yupo humo Bungeni? Haya karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, karibu uhitimishe hoja yako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson, Waheshimiwa Wabunge, awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha na kutuongoza katika kusimamia mjadala wa Bunge wakati wa hoja ya Bajeti Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao na hasa Kamati ambayo inaongozwa na watu mahiri sana Dkt. Mhagama pamoja na Makamu wake. Kwa kweli Kamati hii imetusimamia vizuri na hata kufikia hatua kwa kweli Kamati inastahili sifa kwa sababu tumetumia nao muda mwingi lakini pia wamekuwa watu wema sana katika kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote yamefanyika kwa sababu wachangiaji wote wamejikita katika kutuwezesha kutekeleza majukumu tuliyokasimiwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sambamba na kutatua changamoto za waajiri, watumishi wa umma na hatimaye kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sote tunafahamu na tumesikia katika michango ya Waheshimiwa Wabunge waliyowengi hakuna ambaye hakumpongeza Mheshimiwa Rais. Tunawashukuru sana kwa pongezi zenu kwa Mheshimiwa Rais na tutazifikisha salamu hizi ingawa alikuwa anasikia. Bila shaka sote tunafahamu dunia ipo katika mazingira magumu sana kutokana na majanga mbalimbali, lakini nchi yetu iko salama salimini. Iko salama kiuchumi, kijamii, kiulinzi na iko salama kidemokrasia na ndiyo maana nchi imetulia chini ya Uongozi wa Mama yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango iliyosemwa hapa mingi pamoja na Kamati kuwa imekuwa na mchango wa uongozi, lakini ni kama imejirudia kwenye maeneo yaleyale yaliyosemwa na Kamati, tukiichukua michango yote. Wachangiaji waliyochangia kwa kuongea ni 25 na waliyochangia kwa kuandika ni wawili uki–*group* michango hiyo yote unaikuta imejikita katika maeneo takribani 15.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya 15 ni haya yafuatayo na kwa sababu ya muda pengine nisipate fursa ya kuweza kuyamaliza lakini michango hii ilikuwa ni mizito, ni muhimu kwa Taifa letu, ni muhimu kwa umoja wa Taifa, ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu, lakini pia ni muhimu kwa ustawi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa maneno ya dakika 20 sidhani kama naweza nikatosheleza sana, lakini nitajaribu hata hivyo kupitia baadhi ya maeneo kwa haraka ili angalau

iweze kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge kuweza kutupitishia bajeti. Tukishapitisha bajeti maana yake siyo kwamba tumefika mwisho wa kuwasikiliza, tutaendelea kuwasikiliza na kuboresha eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu masuala ya ajira kwa utumishi wa umma ni mhimili muhimu sana katika usalama wa nchi. Watumishi wa UMMA NA UTUMISHI WA UMMA kwa ujumla ni rasilimali muhimu sana katika maendeleo na mshikamano na umoja wa Taifa lolote lile. Mathalani ili kuweza kuajiri watu wanaotosha, ili kuweza kuwalipa mishahara watumishi wakaridhika kabisa, kabisa, hakuna nchi imefikia kiwango cha asilimia 100. Katika kila nchi yako madai, watu wanadai kwa viwango tofauti na pengine nchi yetu inaweza ikawa imefikia hatua nzuri sana katika kuutunza na kuusimamia utumishi wa umma tofauti hata na nchi nyingi zinazotuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnasikia wenyewe baadhi ya nchi sasa hivi hata kulipa mishahara ni tatizo, lakini sisi wananchi wetu wanalipwa mishahara. Kama mishahara kulipa ni tatizo utazungumzia ajira mpya? Siyo rahisi kuzungumzia ajira mpya. Kama kulipa mishahara ya watumishi siyo rahisi, utasimamia utendaji wa kazi? Siyo rahisi kuusimamia utendaji wa kazi. Kwa hiyo, tujivunie na tujipongeze kwamba mpaka sasa pamoja na changamoto za kidunia na majanga mbalimbali, Taifa letu na nchi yetu iko salama na tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema nitoe mfano tu, mishahara lazima iendane na pato la Taifa, haipangwi tu, lazima unapoipanga mishahara iendane na mapato ya ndani ya nchi yetu na uwezo wa uchumi. Tunaweza tukalipana tunavyotaka, liko Taifa moja duniani siwezi kulisema hapa, limewahi kuamua kupanga mishahara kadri ya maneno, wakaachana na uhalisia, Taifa lilianguka na mpaka leo Taifa hilo halijawahi kusimama, liko *America* huko. Halijawahi kusimama pamoja na u–*giant* wake kwa sababu

walikosea tu kwa kipindi cha makubaliano ya hela, baadaye kutoka kule ikawa ni ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mathalani kwa mwaka 2020/2021, Bajeti ya Mishahara ilikuwa ni trilioni 7.7, wakati mapato ya ndani yalikuwa ni trilioni 24, hii ni sawa sawa na asilimia 32. Mwaka 2021/2022, Mishahara ilikuwa ni trilioni 8.1, wakati mapato ya ndani yalikuwa ni trilioni 26.3. Mwaka 2022 Mishahara ilikuwa ni trilioni 9.8 na pato la Taifa lilikuwa ni trilioni 28, sawa sawa na asilimia 34. Sasa hivi kwa Bajeti ya 2023/2024 tutakwenda trilioni 10.8 wakati mapato ya ndani ni trilioni 31, tayari asilimia 35.

Mheshimiwa Spika, kuna *standards* za Kimataifa, uki – *break* hiyo ni lazima utaingia kwenye *crisis* ya uchumi. Maslahi haya tunayopigia kelele, walipwe vizuri, wafanywe nini watu hawa hawazidi milioni moja, ni laki tano na sitini *plus*. Sasa tukitaka hawa wapate sana maana yake tusimamishe miradi mikubwa ya maendeleo. Tunazungumzia idadi ya watu chini ya milioni moja, chini ya Watanzania walio sasa karibu milioni 62. Sasa hapa tunazungumza maslahi ya watu hawa tu, ingawa wanafamilia zao, lakini tunazungumzia maslahi ya hawa watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuwe makini tunapotaka kuzungumzia maslahi, tuangalie pia na miradi na mambo mengine ambayo yatabeba uchumi huu ili kujenga uchumi na baadaye tuje tumalize haya yabebe na maslahi ya watumishi. Kwa hiyo hatuwezi kwenda kwenye *perfections a hundred percent,* lakini tumejitahidi na tuko vizuri kama Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona nianze hapa ili tuwekana vizuri, tunaweza tukadai chochote kile tukasema chochote kile, lakini tufahamu kwamba lazima tuendane na uwezo wa uchumi wetu katika kuweka maslahi ya watumishi wetu.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili lililozungumzwa ni nafasi za kazi kugawanywa katika halmashauri ili kuwe na usawa katika kuajiri watumishi wa umma. Sera ya Menejimenti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Toleo la Pili la Mwaka 2008, kifungu cha 4(2) inatamka kuwa ajira zinatakiwa kuwa za ushindani na zifanyike kwa kuzingingatia miundo ya kiutumishi *(Schemes of Services)*.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge hapa wamezungumza kwa hisia kubwa sana kwamba tugawane kwa sababu hatuoni uhalisia, hazigawanywi sawasawa. Hata hivyo, nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, kwamba huko nyuma hatukuwa na Sekretarieti ya Ajira na tatizo lilikuwa kubwa kuliko hili la leo. Ni bora leo tumeweka Sekretarieti ya Utumishi wa Ajira na kuweka ajira zetu ziwe *centralized,* tunaweza tukaona hata hayo mapungufu.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tulikokuwa hata hayo mapungufu kuyaona ilikuwa ni vigumu. Tunafahamu zilikuwepo baadhi ya taasisi ambazo ulikuwa unakuta watu wa ukanda fulani, watu wa maeneo fulani ndiyo wameajiriwa pale, leo kuna hata afadhali unaweza ukasema Hapana, mbona kwangu sijaona, mbona kwangu sijaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo msukumo wa haya yote na tulipofika pamoja na pengine mapungufu ya mfumo ulioko sasa, lakini tumefika hapa kwa sababu wanaomaliza katika vyuo na kutegemea kuajiriwa na Serikali ni wengi kuliko nafasi zilizopo. Nilikuwa naongea na Waziri wa Elimu tunavyo Vyuo vya Ualimu mathani 35 vya Serikali, weka na vya binafsi tuchukulie kila chuo wakamaliza wanafunzi 200 tu katika hivyo vyuo 35, tutakuwa na wahitimu wangapi? Watakuwa karibu 7,000.

Mheshimiwa Spika, hapa hatujaweka na vyuo binafsi, *so in average* tuna wahitimu wa nafasi za Ualimu kwa ngazi tofauti tofauti karibu 15,000 kila mwaka. Ajira za Walimu

zinazotoka mathalani zilizotoka kwa mwaka 2022/2023 ni 13,000, tayari wahitimu wamezidi idadi ya nafasi zilizopo. Kwa hiyo kumbe kuna makosa ambayo tuli–*over plan* na mkumbuke kwa nini Walimu?

Mheshimiwa Spika, Walimu wamekuwa wengi kwa sababu tulikuwa na uhaba wa Walimu wakati tulifungua shule nyingi, shule za kata ambazo zikahitaji Walimu, tukakosa Walimu, ndiyo tukaja na *vodafasta, we had no Teachers*. Tuliposema hivyo vyuo vikafunguka, kila mtu anajua huku ndiyo kwenye mikopo, kwenye nini? Ndiyo sababu tukapeleka wanafunzi wengi na fursa zikafunguka pale, sasa tumewa–*over training* Walimu. Kwa hiyo kuna haja ya kufanya u–*turn* na kupunguza. Sasa hili ni jambo ambalo sekta na yenyewe watatusaidia katika kufanya hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa hili siyo jambo la kiutumishi peke yake, lakini jambo ni kwamba tuna walimu wengi lakini nafasi ni kidogo, kwa hiyo ugomvi huu wote na mivutano hii yote inatokana na sababu hiyo. Niseme tu kwa sababu ya nafasi ndogo tutajitahidi, ni bora tukabaki katika mfumo uliopo tukauboresha kwa kutumia mawazo haya mlioyasema, kuliko tukazichukua hizi nafasi mkasema tugawane. Nilikuwa naangalia kwenye *group* letu la *party caucus* tukigawana tutapata kila mmoja 112, haya nipeni mimi nichukue 112 niende nazo kwenye Jimbo langu la Kibakwe, nikifika nazo tu pale Kibakwe kila mmoja anajua Mbunge ndiyo anaetoa hizi ajira, wanakuja kujaa kwangu.*(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nikishapewa hizo ajira 112 ambazo mmenigawia za Jimbo la Kibakwe, Mfuko wa Jimbo wenyewe mnajua Madiwani tunavyohangaishana nao, kwa hiyo Madiwani na wenyewe watasema tugawane, kama ni 112, unapata 20 haya tugawane kila mmoja kila Diwani anapata Watatu, ikifika kule Diwani nae ataambiwa Mwenyekiti wa Kijiji atasema tugawane, *automatically*

zitakuwa hazitoshi na tutaleta *crisis* na ugomvi zaidi, isipokuwa tunachoweza kufanya ambacho tunafikiria kwenda kufanya ni kutumia mawazo haya ya kuhakikisha kwamba waajiriwa wa nchi hii wanatoka maeneo yote kwa sababu utumishi huu ni utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnakumbuka Waheshimiwa Wabunge, tunayo Majimbo yetu na tumekuwa tukiomba vibali vya Halmashauri kupata ajira na tumekuwa tukipewa zile ajira 15, 16 za wale Watendaji wa Vijiji na nini na nini. Niambieni nani, zimebaki katika Jimbo lake zote? Zikifika kule Mkuu wa Wilaya anataka Ndugu yake awepo, Mkuu wa Wilaya anatoka Kibakwe? Afisa Utumishi hatoki Kibakwe, anataka ndugu yake awemo, *DSO* anataka ndugu yake awemo, Mkurugenzi anataka ndugu yake awemo, Afisa Mipango anataka ndugu yake awemo. Hawa wote hawatakuwa wametoka Nkasi, hawa wote watakuwa wamekuja na vyeo vyao na wao watakuwa ndiyo wanakaa kwenye ile *panel* na ndiyo wenye nguvu, wanazichukua zile zote matokeo yake wa pale Nkasi, wa pale sijui Peramiho hapati.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hilo lenyewe tuko kule sisi limetushinda. Tukisema tuchukue zile ndiyo kabisa! Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wazo ni zuri, acheni tukae tutulie. Suala la Utumishi wa Umma ni suala la usalama wa nchi. Nchi hii imewekwa katika misingi mizuri sana na haya mambo yanayochipuka ni ya mtu mmoja mmoja lakini kuna ukweli kwa maneno haya mnayosema ninyi Viongozi mnaowakilisha watu kwamba kuna upendeleo tunaona kuna harufu, hawezi akawa mtu mzima hapa nikasema haupo haiwezekani! Yako maeneo upendeleo upo na yapo maeneo yako vizuri, lakini lazima turekebishe na kurekebisha kwenyewe hatuwezi kuvunja kitu ambacho kipo kizuri, tukaanzisha ambacho hatukijui hatma yake.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana tutachukua mawazo haya, *will make a system* ambayo hata katika uombaji tu pale tuta–*control*. Hebu waombe wenye *address* inayojulikana kama anatoka Dodoma Mjini au maeneo haya hatuzungumzii makabila sisi tunazungumzia *originality* ya mtu alikosomea na wazazi wake na alikozaliwa, hilo linawezekana kufanyika na zikapatikana katika mtandao na msambazo ambao upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumetengeneza mifumo, bajeti hii ya safari hii ni bajeti ya mifumo. Tunataka kuimarisha nguvu ya mifumo. Kuna mifumo mipya iliyojengwa zaidi ya 15. Mifumo hii itatusaidia sana katika kudhibiti. Nimpongeze sana Mheshimiwa Jenista Mhagama kwa kusimamia na kuanzisha mifumo hii ambayo mingi yake bado hatujaanza kuitekeleza kwa asilimia 100, lakini ipo mifumo mipya.

Mheshimiwa Spika, ipo mifumo ambayo itatusaidia katika kusimamia utendaji kazi wa watumishi, iko mifumo itakayotusaidia katika kuhakikisha mtumishi mmoja mmoja yuko wapi na anafanya nini, iko mifumo ambayo itatusaidia suala la ulipaji wa mishahara na taarifa za kila mtumishi na uki-*press* mimi nilifanyiwa majaribio na nimeweza kuona *just press in real time you get wherever you want,* wapi kuna upungufu wapi kunaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii tunaupungufu wa walimu wa hesabu, masomo ya sayansi 11,336. Ajira zilizotoka za Walimu ni 13,000. Ukitaka hapa ugombane hapa na Waheshimiwa Wabunge useme tunaajiri walimu wa masomo ya sayansi tu, hapa watu wao wana masomo ya *arts,* nini na nini utasikia vurugu, hata huko kwenye maofisi ni vurugu. Wanaanza tuweke kidogo, lakini kimsingi tunao walimu wa masomo ya *arts* wengi wamepitiliza hatuna hata pa kuwaweka. Tulio na shida nao ni hawa wa masomo ya sayansi, *Chemistry*, *Physics, Biology* na Hesabu.

Mheshimiwa Spika, tuchukue basi haya tuamue hapa, tuchukue zote hizi tuseme tunawapa walimu wa hesabu kupunguza *gap,* utasikia tu. Kwa hiyo, nasema Waheshimiwa Wabunge tuachieni tutafakari Serikali hii ni Serikali yenu. Ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na Bunge hili hauishii kwenye kupitisha mafungu tu ya bajeti hii, uendelee hata nje ya hapa na nina wakaribisha na Mheshimiwa Spika nimechukua maoni yako, lazima tulete semina, kwa sababu moja kati ya misingi ya utawala bora ni uwazi. Moja kati ya misingi muhimu ya utawala bora ni uwazi. Hatutaficha chochote tutaleta hata mifumo ambayo bado hatujaimalizia kwa ajili ya majaribio tuje tufanye semina na Waheshimiwa Wabunge waone hali halisi ilivyo ili wakitushauri tushauriane vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo ni mengi lakini muda ni mdogo hata hivyo yamesemwa maeneo mengi sana. Ucheleweshaji wa uwasilishwaji wa michango ya katika Mifuko ya Jamii wastaafu, hili tutaendelea kulisimamia. Tumetengeneza mifumo ambayo itahakikisha ina - *link* na *PSSSF* na mishahara ambapo mfumo huo wenyewe ukiubonyeza tu hivi hakuna mtu anayeweza akafanya chochote hata yule wa *PSSSF* anaweza asifanye chochote mpaka mwajiri atoe mchango wake na muajiriwa naye atoe mchango wake iingie kwa pamoja. Haipokewi tofauti tofauti. Kwa hiyo, hiyo itafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine lililozungumzwa ni watumishi wa umma kukaimu nafasi za uongozi kwa muda mrefu. Hili tatizo linawezekanika ni la kiutendaji tu, ni *very administrative* tutaliwekea utaratibu ambao tutahakikisha kwamba na lenyewe hili linakwisha. Watu wanakaimu muda mrefu na wakati wengine wana sifa. Watu wanakaimishwa wakati hawana sifa na watu wanazulumiwa wenye sifa kuingia. Kwa hiyo, kote kuna matatizo. Mtu anakaimu na sheria inasema kukaimu mwisho ni miezi Sita, lakini mtu anakaimu miaka 10. Sasa huyo ni Kaimu huyo si tayari tu na

wakati huo ukimleta mwingine unaleta ugomvi na *conflicts* kubwa sana ambazo zinapelekea. Kwa hiyo, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba eneo hili tunalifanyia kazi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kanzidata katika kuajili watumishi wapya ili kupunguza gharama za Serikali. *Yes,* haya mawazo yalikuwa ni ya Waheshimiwa Wabunge ya bajeti iliyopita na Mheshimiwa Jenista Mhagama aliyachukua na wamekwenda kutekeleza, kanzidata ipo hawarudii tena kufanya *interview* na sasa tukaongeza mpaka na muda wa kukaa kwenye kanzidata kufika mwaka mmoja, ile *system* inafanya kazi.

Mheshimiwa Spika, mimi niliambiwa na Waheshimiwa Wabunge nisaidie kuna kijana wangu alifanya *interview* na nini na nini, nimeshangaa jana ananishukuru. Ananishukuru nini? Anasema amepata ajira, kumbe wali- *upload* jana, walitoa jana, wametoa. Sikufanya mimi ila nashangaa nashukuriwa na Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi na ninyi kuna watu wanawashukuru lakini hamkufanya chochote. Ni *system* ya Sekretarieti ya Ajira inafanya kazi katika *merits* kwa uwazi na kwa ukweli. Kwa hiyo, hili jambo limefanikiwa ni mawazo yenu. Amini Serikali, muamini kwamba kuna watu wakweli, ingawa kama kuna wazembe ni wachache wanaotupotosha.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine lilikuwa ni usaili unaoendeshwa kufanyika ngazi ya Kanda badala ya Dodoma ikijumuisha matumizi ya TEHAMA. Mfumo upo tayari, tumetengeneza mfumo unaitwa *online aptitude testing system* ambao huu mfumo sasa watafanya usaili hukohuko kwenye Kanda wala hakuna sababu ya kuja Dodoma. Watafanya kwenye Mikoa watafanya kwenye Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ni kuajiri kwa kigezo cha miaka, kwa Jeshi USU, hili tutajaribu kuwasiliana na Wizara ya Kisekta, tuweze kuona changamoto inatokana na nini je, ni lazima kweli kuangalia umri kwa sababu miaka ya 28 mtu akifanya kazi miaka 30 atakuwa na miaka mingapi? Tuangalie tutawasiliana na Wizara ya Kisekta.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu ajira za kujitolea. Ni kweli kulikuwa hakujawekwa utaratibu mahsusi kwa ajili ya ajira za kujitolea. Ziko nchi ambazo ajira za kujitolea *volunteers* ndizo zinazoendesha na zinazosaidia na ku – *supplement gap* ya Watumishi wa Umma. Kwa nini sisi tukiwa tuna watu wengi na tume-*train* sisi wenyewe kwa hela za Serikali, watu wana ujuzi badala ya kumkuta mtu anafundisha na anapenda kufundisha unamkuta anaendesha bodaboda. *This is not right*!

Mheshimiwa Spika, nadhani tukubaliane Waheshimiwa Wabunge na sisi Serikali tunachukua mawazo haya ni lazima tukatengeneze mfumo mahsusi utakao angalia pia hata wanachostahili hicho kidogo, kwa sababu huyu mtu hawezi kujitolea asipate kitu kabisa hataweza kwenda. Anahitaji kufua, anahitaji usafiri. Lazima kuwe kuna utaratibu ambao tuuweke ikibidi hata kutenga bajeti kidogo tutenge tuseme tunahitaji wangapi wa afya, wangapi wa elimu halafu waweze kupata na wafanye kazi huku wakingojea kuajiriwa. Unakuta hawa walioajiriwa pengine hata siyo wazuri sana kuliko hawa wanaojitolea. Inauma wakati mwingine unapokuta haya yanatokea, hili tumelichukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, urejeshaji wa michango ya watumishi walioondolewa kazini wa kubainisha kuwa na vyeti vya kugushi. Mpaka sasa hivi madai 11,896 yenye jumla ya Shilingi Bilioni 35.02 yamelipwa kati ya madai 12,662. Waheshimiwa Viongozi wenzangu, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Serikali hii inaongozwa na Mama huyu ana huruma sana, jambo hili

lilikuwa limekwisha, kukubali kutoa Bilioni 35 ni huruma ya Mheshimiwa Rais. Alisema wapeni fedha zao kwa sababu walifanya kazi lakini jambo lilikuwa limeisha.

Mheshimiwa Spika, katika muda wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia Suluhu, mambo mengi ya kiutumishi yaliyokuwa yanapigiwa kelele yametatuliwa. Kwa upande wa Watumishi na Vyama vyao vya Watumishi wenyewe huko wanaimba tu 'iyena iyena' ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu, haya mengine tunayoyasema huku wala huko hayapo kwa sababu wamefanyiwa mambo ambayo hawakuyatarajia. Kweli kabisa tuwe wakweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ni nyongeza ya mishahara imefanyika, kama ni malimbikizo yamelipwa, hakuna ambacho hakijaguswa niwaambie ukweli Waheshimiwa. Sasa nyingine ni kurudisha posho ya kufundisha *teaching allowance*. *Teaching allowance* hii iliingizwa kwenye mishahara kwa sababu ilikuwa haina *impact* katika mafao. Kwa hiyo, ikaamuliwa na wahusika wenyewe Walimu kwamba hii posho mnayotupa hai - *effect positively* mafao yetu. Kwa hiyo, utaratibu ikaonekana basi kuwasaidia angalau wawe na kitita angalau kizuri iingizwe kule kenye mshahara. Imeingizwa tushasahau sasa tunakuja kudai tena.*(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa mimi niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge wacha tukatafakari, tuwaulize na wenyewe maana hapa kuna walimu mliostaafu, Walimu wenyewe wako kule nje, ninyi mmekuja kuwasemea. Tumewasikia mmewasemea, lakini tukawaulize na wao mnasemaje tunyofoe huku tuwaletee huku au tuiache huku isaidie kwenye mafao? Watasema wao kwa sababu wana vyama vyao.

Mheshimiwa Spika, waraka wa mwaka 2014 kuhusu viwango vya mshahara, posho wa viongozi wa elimu

unaotekelezwa kwa Wakuu wa Shule lakini hautekelezwi kwa Wadhibiti Ubora. Wadhibiti Ubora kulikuwa kuna mkanganyiko wa viwango, mkanganyiko wa viwango ikaonekana huu waraka ukasitishwa na Wizara ya Elimu tutawasiliana na Wizara ya kisekta ambao hawa wadhibiti ubora wako kwao, kwamba baada ya kusitisha wamekuja na *solution* gani na kwenye hotuba yao wanaweza wakaja kuisema vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuhamisha umiliki wa ndege za Wakala wa Serikali *TGFA* kwenda Kampuni ya Ndege ya Tanzania. Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Viongozi wenzangu kulikuwa kuna sababu za msingi sana za kiusalama pia usalama wa rasilimali hizi za Watanzania. Pengine mawazo yale na sababu zile zinaweza zikawa zimepitwa na wakati na pengine wazo hili la kuzifanya ndege hizi zimilikiwe sasa na *ATCL* kwa sababu ni shirika la Kiserikali, *TGFA* ni wakala wa Serikali, *ATCL* ni Wakala wa Serikali. Mimi sioni kama kuna tatizo *just give us time*. Tuje tuangalie zile sababu ambazo siyo rahisi kuzisema, tukaangalie tuweze kufanya hilo kwa sababu limesemwa bajeti iliyopita na limesemwa na bajeti hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhakikisha kwamba vyuo vinatoa kozi ambazo zinaendana na soko la ajira hili nimelisema, Wizara ya Elimu sasa hivi ipo kwenye mchakato wa kubadilisha mitaala na nini, lazima tuangalie pia na *demands* yetu. Waheshimiwa Wabunge haya yataisha tukiwa na Tume ya Mipango. Waheshimiwa Wabunge Tume ya Mipango inakuja waraka umeshatayarishwa mimi nimekwishapitisha nangojea kwenda Baraza la Mawaziri likipitishwa wakati wowote naingia nao pale kwenda kuleta iwepo hapa na ipitishwe ndani ya Bunge hili kama Spika ataruhusu na kutoa nafasi.

Mheshimiwa Spika, tuwe na Tume ya Mipango *that is why are training teachers* bila kujua mahitaji yetu na hata

tukijua mahitaji hatuweki *conditions* za kujua tunahitaji nini na nini, lakini pia hata katika sekta nyingine na ndiyo maana *human capital is a very basic resource* katika nchi, bado inakuwa hatuijui sawa sawa kwamba tunataka nini hatutaki nini, ndiyo maana tunahitaji *reform* kubwa na *reform basically* itafanywa na mifumo ya kidigitali na *artificial intelligence,* lazima tufike hatua hata usaili na nini tuweke maswali pale mtu afanye asahishiwe siyo na binadamu na awe *selected* na *artificial intelligence,* badala ya kufanywa na binadamu kwa sababu huku tunatuhumiana. Kwa hiyo hili wala halina tatizo, tutahakikisha kwamba vyuo vinatoa kozi ambazo kwa kweli zina uhitaji wa watu na vile ambavyo vimehama kwenye malengo yake ya msingi vinarudi katika malengo ya msingi.

Mheshimiwa Spika, eneo la 15 ni Sera, Sheria na Taratibu na Nyaraka za Utumishi wa Umma kupitiwa kwa wakati. Mapitio yanafanyika, tutaendelea kupitia maeneo haya na kuhakikisha kwamba tunaleta mabadiliko ili *reforms* hizi ziendane kwanza tubadilishe sera, tubadilishe sheria na mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge katika muda ambao kama Mheshimiwa Rais ataendelea kuniacha nikabaki katika Wizara hii, ambacho na mimi ninachotaka kuacha kama *legacy* ni kuhakikisha kabisa tunaubadilisha mfumo wa utumishi wa umma, njia pekee tayari msingi umekwishawekwa na Waziri aliyenitangulia kuhusu mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la 16 na la mwisho ni kusimamia na kutoa mafunzo maalum kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi. Mafunzo yanatolewa sana lakini tunaotoa mafunzo tunaelewana? Mafunzo yanatolewa sana, kila bajeti hapo kila mliyopitisha kwenye mafungu yenu kuna mafunzo, kuna kujenga uwezo, kuna kufanya nini, lakini tufike hatua sasa tuwe na *a committed public service, a committed one* na mtu ajue miiko na vitu ambavyo haviruhusiwi katika utumishi

wa umma. Tusichanganye utumishi wa umma. Kama unataka kuwa tajiri nenda kafanye kazi kwenye *private sector*. Kwenye utumishi wa umma hauji kutafuta utajiri unakuja kutoa *service* ni wito. Tusichanganye kabisa *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mawazo mengine ya kufikiria tunaweza tukaufanya utumishi wa umma ukawa kama udalali wa kuuza vitu fulani fulani sokoni, haiwezekani! Lazima utumishi wa umma uwe na miiko na mtu ajiulize niingie au nisiingie? Lazima uwekwe ugumu fulani wa utumishi wa umma. Huwezi ukamfanya kila mtu akawa Sheikh, huwezi ukamfanya kila mtu akawa Mchungaji. Ni lazima kuwe kuna sababu ambayo inakufanya wewe uwe mtumishi wa umma. Sasa hizo ndiyo lazima tufike huko, siyo kila mtu ni mtumishi tu wa umma.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo lazima tulazimishe watu kuyasomea. Leo hii kuna baadhi ya maeneo tumekosa watumishi kabisa, hili siyo jambo la ajabu hata Marekani *best brain* huwa wanazi- *retain* siyo kwamba wao hawana watu ila wanajua *this is the best brain* na hapa kwenye eneo hili ni gumu. Ndiyo maana nendeni Marekani, nendeni wapi, nendeni kokote huko mtakuta Watanzania Wabobezi ndiyo wanaofundisha kwenye Vyuo Vikuu, ndiyo wanaoendeha taasisi muhimu kule, ni kwa sababu watu wana *retain best brain,* kwa sababu duniani kuzidiana akili ni kitu cha kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutasimama na hayo na tuta-*train* watu wetu, wako watu wengine watasoma hata kama hawataki. Tukijua una akili utasomeshwa hiki ili uje ufanye kwa lazima, wamekuwa wakifanya hivyo hata Awamu zilizopita. Mwalimu Nyerere alifanya hivyo, Awamu ya Pili ya Ali Hassan Mwinyi imefanya hivyo, Awamu ya Tatu imefanya hivyo, Awamu ya Nne ya Kikwete imefanya hivyo. Kuna watu lazima walazimishwe kusoma!*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Chamuriho huyu alilazimishwa kusoma, tena hayo masomo aliyoyasomea hayakuwa yake, akaambiwa utasoma hiki unachoambiwa kusoma, leo hii kwenye nchi ukitafuta watu walio na ubobezi katika eneo la usimamizi wa miradi ya kiinjinia huwezi kumuacha Mheshimiwa Chamuriho, lakini *do we have them in the University of Dar es Salaam or other Universities? Will you find other genius?* Bado tunatakiwa kulazimisha watu wetu katika kujenga mfumo mzuri wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na watu ambao wanaweza ku-*deliver* na kusimamia kama nchi ili tuweze kupata maendeleo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nirudie tu kusema nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kusema kwa kuandika na wale ambao hawakusema kwa sababu niliziona hisia zao, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge yote mliyoyasema hapa, yote kabisa tunayachukua kwa uzito mkubwa sana na tuhakikishe kwamba nchi yetu inapata maendeleo na ustawi, kwa sababu rasilimali muhimu ni watu, kuhakikisha wanafanya kazi na uaminifu na uadilifu.

Mheshimiwa Spika, suala la utawala bora hakuna *champion* wa utawala bora kama Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Nimekusikia Mheshimiwa Aida Khenani hayo ni mambo madogo, makubwa yamekwisha tatuliwa, haya madogo tunawaachia watu wa chini huku watayafanya lakini nataka nikuhakikishie Rais wetu hana ubaguzi kwa misingi ya Vyama, Rais wetu hana ubaguzi kwa misingi ya dini, wala kwa misingi ya makabila wala ukanda. Ameamua kujenga nchi moja, ameamua kujenga nchi yenye mshikamano, tuendelee kumuunga mkono na nikuhakikishie jambo hilo tutalishughulikia ili tuweze kuacha kuwa na manung'uniko ya mtu mmoja mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika baada ya maneno haya, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana. Tutaendelea sasa na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ukurasa wa 189.

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, mnaweza kwenda tena kwenye vishkwambi vyenu mkatafuta hapo taarifa hizi ili tuwe tunafuatilia sote kwa pamoja. Hata hivyo, kabla sijaanza kuwahoji mafungu, kuna marekebisho ambayo yameletwa na upande wa Serikali na walishaonana na Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge, na mabadiliko yaliyoletwa na Serikali ni kutokana na mawazo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge ambao wanatuwakilisha sisi sote kwenye Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria.

Kwa hiyo, Serikali ilipochukua mawazo yao, imeenda kuyafanyia kazi na kufanya marekebisho ya fedha kwenye maeneo kadhaa. Kwa hiyo, wakati tukisoma na ile uliyonayo hapo, huenda imeshawekwa hii mpya ama huenda haijawekwa mpya, lakini sisi tunayo hiyo taarifa mpya sasa hapa mbele ambayo Serikali imeileta baada ya kusikilizana na Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria.

Sasa kwa sababu maeneo ya mabadiliko yako mengi kidogo, lakini kwa ujumla wake fedha inayoongezeka, hebu mtu ambaye ana kishkwambi afungue ndiyo nijue kama imeshawekwa hii mpya ama bado.

**WABUNGE:** Imewekwa.

**MWENYEKITI:** Imewekwa, haya. Kiasi kile cha jumla kinasomeka kiasi gani? Ndiyo nitajua kama ndiyo hiyo mpya, ama vipi? Nisomee Mheshimiwa. Nani amesema huku? Mheshimiwa Yahaya. Washa kisemeo.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imewekwa, lakini jumla inakuja kwenye trilioni moja na bilioni moja, ila bado nilikuwa naifuata.

**MWENYEKITI:** Basi sawa. Kama hicho ndicho kinachosomeka, maana yake mpya zimeshawekwa kwa sababu mwanzoni ilikuwa haifiki hii Shilingi trilioni moja. Ahsante sana.

Sasa, Katibu tusomee hiyo sehemu halafu tuendelee.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ukurasa wa 189. Kifungu 1001, kutokana na *addendum* sasa kinasoma Sh. 27,563,399,000.

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kifungu 1001 – *Administration and huma Resources Management*………………...Sh. 27,563,399,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki ndicho chenye mshahara wa Waziri. Hapa ninayo majina ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanataka ufafanuzi, naona majina mengi kabisa hapa.

Tutaanza na Mheshimiwa Constantine John Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba *output* ya vyuo kuanzia *certificate, diploma* na *degree* ni kubwa kuliko uwezo wa Serikali kuajiri; na mfumo ulivyo wa *Ajira portal,* unaruhusu mwombaji kuingiza *credential* yake moja wakati anaomba akitumia namba yake ya *form four;* baadaye hauruhusu kabisa kama mtuishi huyo ameona hapati kazi ya Ualimu, akasome labda *Diploma* au *Degree* nyingine kuingiza hizo *details* kwenye mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri: Ni lini mfumo huo utaweza ku-*accommodate* taarifa za ziada za waomba ajira ambao waliomba kwa cheti cha kwanza, lakini wana sifa nyingine na hawawezi kupata ili waweze kupata ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Mbunge tumelichukua, lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mifumo hii sio Biblia. Mifumo hii mara nyingi hata kwenye simu zetu unaona kuna *upgrading version* kila siku zinafanyika katika mifumo mbalimbali. Kwa hiyo, wazo lake tumelichukua, ni wazo zuri, tutakwenda kulifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Kanyasu naona ameelewa, amekaa. Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri kuhusu Maazimio ya Bunge la Kumi na Mbili, Mkutano wa 10, kuitaka Serikali iweke utaratibu madhubuti na wenye uwazi ambao utaratibu zoezi zima la ajira Serikalini kwa namna ambayo nafasi zitakazojazwa zitaakisi umoja wa kitaifa bila kuathiri vigezo; nilitaka nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa vile haya yalikuwa ni Maazimio ya Bunge na tayari kuna muda kidogo tangu maazimio haya yafanyike, atupe sasa *time frame,* ni lini Serikali itatekeleza hili? Ni lini Wabunge watapata nafasi ya kuutazama huo mfumo na kuu-*assess* kama kweli ni mfumo wa wazi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nani kati yenu? Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Waziri hapa kutaka kujua tunafanyaje? Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu, tulijadili na Kamati jambo hili na sasa hivi tunatarajia kutangaza zile ajira mpya 45,000. Naomba atupe nafasi, katika hizo ajira 45,000 zinazokuja, tutaanza kuufanyia kazi huo mfumo kama ambavyo tulijadili na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anapendekeza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni ajira 21,000 au ni 45,000?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 21,000 ni hizi za mwaka huu wa fedha ambazo zinakwenda

kwisha, 45,000 ni zile ambazo zinakuja baada ya Bunge lako kutupitishia mafungu haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhagama pia naona amekaa. Kwa hiyo, ameelewa.

Mheshimiwa Venant Daudi Protas.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa nataka nipate ufafanuzi wa jumla. Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha hoja yake, ametoa ufafanuzi mzuri juu ya ajira zinazopatikana na amechukua maoni ya Wabunge, na kwamba atajali mgawanyo kutokana na na maeneo yote tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri kasema, hii mifumo siyo Msahafu au Biblia. Tunataka tuelewe, unapokwenda kwenye mfumo pale kuomba ajira, haioneshi huyu mtu anatoka maeneo gani? Haimpi hoja ya kuwa huyu mtu ni wa Igalula au wa Busega? Inamwonesha mtu anapoomba anajaza namba ya *Form Four* na shule aliyosoma, lakini mtu anaweza kuwa anatoka Igalula, kasomea Dar es Salaam, anajaza kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka *commitment* ya Serikali. Kwa kuwa, lengo la Serikali kila upande wa nchi upate wahusika ambao wataingia kwenye Serikali: Je, tunataka tujue, watawajuaje wananchi wa Igalula wameomba kwenye mfumo wakati mfumo wenyewe unakataa kuwatambua hao wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni hivyo, anasema watu wote. Basi watakwenda *manual* kuwajua wananchi gani wako sehemu gani? Kama wanakwenda hivyo hivyo, ndiyo irudi hoja wa Wabunge, sisi tuna majina ya wananchi wetu wote; tuwape 100, chukueni 20, ili tujue wananchi wa kule wametoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka ufafanuzi wa jambo hili, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naona unataka kusimama. Ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo tumeelea katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba, kwanza Serikali inatambua changamoto hiyo iliyopo katika eneo la ajira. Hili nataka nikuhakikishie na wala siyo kwamba, ni la kwako peke yako, ni la Tanzania nzima, na Serikali ina-*appreciate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza kwamba mfumo siyo Msahafu, haya ambayo mnaeleza Waheshimiwa Wabunge ndiyo mambo ambayo tunataka tukajitahidi kuhakikisha kwamba, tunayaweka sawa, ili malalamiko siku nyingine juu ya kwamba kuna upendeleo, sijui wanaangalia watu wa dini fulani, watu wa kabila fulani, tuyaondoe yote. Igalula iwe na watu, Bagamoyo kuwe na watu, Chalinze kuwe na watu, Moshi kuwe na watu, Mara kuwe na watu na maeneo mengineyo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba, hayo ndiyo mabadiliko tunayoenda kufanya. Katika bajeti yetu, yako maeneo ambayo tumeelekeza na Bunge lako likitupitishia, tuna fedha tumezitenga kwa ajili ya kwenda kufanya *review* na kutengeneza mifumo kwa ajili ya kuhakikisha haya mambo yanakaa vizuri, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Protas, naona umesimama.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na ufafanuzi wa Mheshimiwa Naibu Waziri,

naungana naye kwamba mfumo hauwezi kuwatambua. Sasa ndiyo turudi kwenye hoja za Wabunge ya kwamba, kama mtakwenda *manual,* ndiyo twende kwenye hoja, tuhakikishe wananchi wa kila upande wanaingia, kwa sababu mfumo hauwezi kuwatambua kwa maelezo ya Waziri.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante sana. Hoja ni kwamba haturudi kule nyuma, ila tunaboresha hiki kilichopo. Kwa hiyo, maelezo ya Waziri kwamba tunachukua mawazo yako, ni kwamba, hicho ulichosema wale watu wa mfumo waongeze hivyo vi-*box* mle ndani. Ndiyo hoja ya msingi hapa. Kwa hiyo, haturudi tena kule nyuma, aah, hapa hapa tulipo, lakini tunaenda kuuboresha ule mfumo. Ndivyo alivyosema Waziri akijibu hapa, lakini pia ufafanuzi wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nafikiri kwenye hili kwa sababu, Mheshimiwa Waziri wakati akijibu hapa amesema, ile semina niliyosema wataileta, nadhani wakati huo sasa tutaweza pia kupendekeza na vi-*box* na vingine na vingine. Kwa sababu, hizi changamoto tunazozisema ni kwa upande mmoja tu, lakini yako mengine. Pengine mwingine anaweza akaomba Ualimu, Udereva, anaweza akaomba na kazi nyingine. Ule mfumo wote watakapokuja kutueleza tutawapa na hayo mawazo mengine, ili mtu sehemu zote anazoweza yeye kufanya kazi, mfumo uwe naye. Siyo uwe umewekwa tu kwenye Ualimu kumbe na udereva unaweza; na ungeweza kupata Udereva, wewe ungekuwa sawa tu.

Kwa hiyo, hayo yote wataendelea kuongeza hivyo vi-*box,* lakini nyuma kule tusirejee. Maana isije kuwa imetoka picha hiyo. Nadhani picha ni kwamba, maboresho yakafanyike hasa kwenye zile ajira zitakazokuja ili mtakapokuja kutufanyia semina, basi tuwe tunaweza kuwa tunafanya huo ulinganifu.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo jina hapa mbele la Mheshimiwa Halima James Mdee.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya Utumishi wa Umma, Namba 23 ya mwaka 2009, inasisitiza kuwa madai ya watumishi yalipwe mara tu yanapotokea. Sasa taarifa zimekuwa zikionesha kwamba, madai ya watumishi yamekuwa yakikua kwa kiwango kikubwa sana; na majibu ya Waziri yamejikita sana kwenye eneo la mshahara ambao mimi sitataka kulizungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Taarifa za Mkaguzi kwa miaka mbalimbali zimekuwa zikionesha kwa mfano, 1920 ilikuwa Shilingi bilioni 333, mwaka 2021 Shilingi bilioni 429, na sasa hivi ambao bado ndiyo tutaenda kuifanyia kazi ni Shiling bilioni 509. Kwa hiyo, sasa tatizo limekuwa ni kubwa na kutokana na huu ucheleweshwaji unaenda kinyume na kanuni yenyewe; na watu wanaosemwa kwamba ni wacheleweshaji wakubwa sana ni Wizara ya Fedha, na ninashukuru Waziri wa Fedha yuko hapa: Nataka kupata majibu yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, juhudi za Rais wa Awamu ya Sita zimeonekana kwa kupunguza, lakini hizi juhudi haziondoi ukweli kwamba Kanuni ya Utumishi wa Umma ambayo ni Sheria inataka haya masuala yatatuliwe vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba majibu, na nisipopata majibu ya kuridhisha, nitakamata Shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi. Aah, Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikiri kwamba ni kweli anayoyasema kwamba, bado tunayo malimbikizo mbalimbali ya madeni ya wafanyakazi,

lakini hatua ambazo Serikali inafanya na nilieleza wakati najibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa, kwamba, katika moja ya hatua kubwa ambayo Mheshimiwa Rais anafanya ni kuendelea kupunguza vilio vya wafanyakazi. Katika kufanya hivyo, pamoja na mambo mengine yote, kama sitakosea ameshalipa zaidi ya shilingi bilioni 204 katika malimbikizo mbalimbali ya wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoweza kusema ni kwamba, Mheshimiwa Mbunge atuelewe kwamba, Mheshimiwa Rais na Serikali inaendelea kuyaangalia malimbikizo yote, na changamoto zote ambazo zinakabili maeneo hayo ambayo wafanyakazi au watumishi wetu wamekuwa wanayadai. Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nia ya Serikali ni kuendelea kulipa na tutafikia malengo yote hayo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, naona umesimama. Kwa muda wetu pale ninavyouona, Kanuni ya 123 inaanza kufanya kazi sasa.

Katibu.

Kifungu 1001 – *Administration and Human Reosources Management*………………...Sh. 27,563,399,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.......Sh. 558,572,700
Kifungu 1003 – *Government Communication Unit*……………...………………...Sh. 273,879,700
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*……………...…………………....Sh. 274,691,500
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 239,999,500
Kifungu 1006 – *Planning Division*..........................Sh. 584,259,500
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*......…………..Sh. 351,553,500
Kifungu 2001 – *Policy Development Division*....Sh. 2,196,630,600
Kifungu 2002 – *Management Services Division*...Sh. 834,414,500
Kifungu 2003 – *Establishment Division*.................Sh.1,173,940,500
Kifungu 2004 – *Ethic Promotion Division*...............Sh. 586,366,000

Kifungu 2005 – *Human Capital Management Division*……...............………..Sh. 1,348,577,500
Kifungu 2006 – *Performance Contracting*...........Sh. 529,400,000
Kifungu 3001 – *Human Resources Development Division*……………….................Sh. 7,716,269,000
Kifungu 3004 – *Division of Salary and Renumeration*..............................Sh. 821,836,000
Kifungu 4002 – *Management Information System Division*.....................................Sh.12,076,215,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*............................Sh. 1,686,110,360
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts* Unit.........Sh. 157,116,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*..................................................Sh. 117,437,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 1004 – *Information and Communication Technology Unit*............................Sh. 165,362,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*........................................Sh. 0
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 113,848,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*..................................................Sh. 33,205,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*..................................................Sh. 142,637,148

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4001 – *Archive Management Division*....Sh. 480,314,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 4002 – *Records Center Division*.................................Sh. 0

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4003 – *Records Management Division*...Sh. *851,869,492*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 4004 – *Founders of The Nation, Presidential Libraries and Museum Division*.....Sh. 149,912,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Ikulu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..........................Sh. 32,157,384,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..........................Sh. 668,772,770,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 826,331,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning* ..................Sh. 1,018,881,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 625,534,000

Kifungu 1005 – *Information and Communication Technology Unit*............................Sh. 300,787,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*................................................Sh. 754,624,000
Kifungu 2001 – *Cabinet Secretariat*...................Sh. 3,661,435,000
Kifungu 2002 – *Government Communication*....Sh. 380,429,600
Kifungu 2003 – *Good Governance*...................Sh. 1,074,988,000
Kifungu 2004 – *Public Service Appeal*..................Sh. 778,161,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...........................Sh. 2,594,253,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 408,628,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*................................................Sh. 572,720,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*................................................Sh. 289,296,000
Kifungu 1005 – *Procurement and Management Unit*..................................................Sh. 277,044,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*........................Sh. 279,770,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*...........................Sh. 449,096,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*.......................Sh. 395,924,000
Kifungu 2001 – *Public Leaders Ethics Enforcement Division*..........................................Sh. 562,427,000
Kifungu 2002 – *Public Leaders Ethics Promotion Division*..........................................Sh. 550,889,000
Kifungu 2004 – *Zonal Office – Northern Zone*......Sh. 441,769,000
Kifungu 2005 – *Zonal Office – Southern Zone*......Sh. 400,808,000
Kifungu 2006 – *Zonal Office – Central Zone*.........Sh. 563,265,000
Kifungu 2007 – *Zonal Office – Eastern Zone*.........Sh. 573,811,000

Kifungu 2008 – *Zonal Office – Southern Highlands*......................................Sh. 556,836,000
Kifungu 2009 – *Zonal Office – Lake Zon*................Sh. 591,408,000
Kifungu 2010 – *Zonal Office – Western Zone*.......Sh. 419,176,000
Kifungu 2011 – *Zonal Office – Dar-es-Salaam*......Sh. 885,896,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira kwa Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.............................Sh. 3,788,521,475
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 412,542,950
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*...............................................Sh. 600,181,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*.................................................Sh. 296,578,950
Kifungu 1005 – *Legal Service Unit*..........................Sh. 279,643,160
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*..................................................Sh. 321,123,645
Kifungu 1007 – *Management Information Systems Unit*...............................................Sh. 860,865,320
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 274,031,160
Kifungu 2001 – *Recruitment Management Unit*..............................................Sh. 1,797,679,010
Kifungu 2002 – *Quality Control*..........................Sh. 1,508,130,430

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*............................Sh. 3,427,692,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.........Sh. 344,122,000

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*..................................................Sh. 544,238,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.........................Sh. 168,422,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*..................................................Sh. 160,484,000
Kifungu 1006 – *Legal Services Unit*........................Sh. 245,229,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*..................................................Sh. 291,534,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*............................Sh. 178,700,000
Kifungu 1009 – *Guidelines Formulation, Dissemination and Research*................................Sh. 463,770,000
Kifungu 2006 – *Appeals and Complains Department*................................Sh. 1,310,960,000
Kifungu 2007 – *HR Standards and Compliance Department*................................Sh. 1,188,940,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 4001 – *Archive Management Division*....Sh. 450,000,000
Kifungu 4002 – *Records Center Division*................................ Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*.......Sh.181,992,535,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.............................Sh. 3,300,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kiliipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1006 – *Planning Division*........................Sh. 3,487,455,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu 2002 – *Management Services Division*.....................Sh. 0
Kifungu 2004 – *Ethic Promotion Division*.................................Sh. 0
Kifungu 2005 – *Human Capital Management Division*..........................................Sh. 200,000,000
Kifungu 2006 – *Performance Contracting*...........................Sh. 0
Kifungu 3001 – *Human Resources Development Division*...Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 4002 – *Management Information System Division*.......................................Sh. 5,200,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)*

**Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...........................Sh. 1,480,000,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*..................................................Sh. 70,000,000

Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*...............Sh. 0
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*............................Sh. 350,000,000
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*..........................Sh. 50,000,000
Kifungu 2001 – *Public Leaders Ethics Enforcement Division*............................................................Sh. 0
Kifungu 2002 – *Public Leaders Ethics Promotion Division*.....Sh. 0
Kifungu 2011 – *Zonal Office – Dar es Salaam*........................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1007 – *Management Information Systems Unit*..............................................Sh. 3,572,517,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*...........................Sh. 300,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsante sana. Sasa nitawahoji; kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 – Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yalipitishwa na Bunge.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kazi yetu ya kuitazama bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Na hivyo nitangaze kwamba Bunge limepitisha rasmi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na tunawatakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nape uketi, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, pamoja na Mheshimiwa

Naibu Waziri wa Ofisi hii ya Rais, Utumishi na Utawala Bora na Makatibu Wakuu, lakini pia na watendaji wengine ambao mnafanya nao kazi kwa karibu. *(Makofi)*

Tunawapongeza sana kwa bajeti yenu kupitishwa na Bunge, lakini pia tunawapongeza kwa ushirikiano mliyoonesha kwa Kamati yetu ya Bunge ambayo imewapa ushauri na mmekwenda kuufanyia kazi kwa sehemu kubwa sana; kwa hiyo, tunawapongeza sana.

Nitumie nafasi hii kuwatakia kila la heri katika utekelezaji wa haya ambayo mmetuahidi hapa kwamba mtakwenda kuyafanyia kazi. Basi tunaamini kwamba mambo yatakuwa bora zaidi. Lakini pia Mheshimiwa Waziri umeahidi hapo mambo mengi kwamba mmeyachukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge, tunaamini yanakwenda kuboresha utendaji kazi wenu na kuwaweka watumishi wetu katika hali bora zaidi kuliko huko tulikotoka.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie pia fursa hii kuwashukuru sana Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria, kwa kazi nzuri sana waliyoifanya ya kuisimamia ofisi hii na sasa tumeweza kufika sehemu hii nzuri ambayo sote tunafurahi kwa haya matokeo tuliyoyaona. Lakini pia tukiwa na matarajio ya mambo ambayo yatafanyika huko baadaye. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nimeshawatakia heri Serikali, tunaamini kwamba watakwenda kuyatekeleza yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeyapendekeza na wao waliyoyaahidi kwamba wanakwenda kuyatekeleza; tunawatakia kila la heri.

Mheshimiwa Waziri mambo mengi umetolea ufafanuzi hapa, na kwa kawaida yale ambayo hayakutolewa

ufafanuzi yataletwa kwenu kwa maandishi ili mpate picha ya ufafanuzi wa hoja zenu.

Katika yote yaliyozungumzwa hapa Mheshimiwa Waziri, pamoja na mambo mengine, lakini tutatamani katika mwaka ujao wa fedha kama ikiwezekana changamoto ya kuchelewa kwa malipo ya wastaafu iishe. Kwa sababu huwa wanatoa taarifa miezi sita kabla hawajastaafu, maana yake kama kuna changamoto ya kufuatilia michango kwa mwajiri au ya kwake mwenyewe, hiyo ndiyo nafasi ya kurekebisha mambo ili anapoondoka ofisini asianze tena kila wakati kufuatilia malipo yake. Kwa hiyo naamini ile miezi sita iliwekwa mahususi kabisa kwamba inatosheleza kwa mfuko unaohusika kujiandaa kumlipa mafao yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, haya mengine mnayoendelea kuyafanyia kazi muendelee kuyafanyia kazi lakini kwa kweli mstaafu anapotoa taarifa ile ya miezi sita itoshe kabisa. Kama kuna mahali anapaswa kuulizwa barua awe ameshaulizwa, kama kuna mahali anaulizwa sijui alianzia kituo wapi, awe ameshaulizwa. Kwa nini, kwa sababu yeye hahusiki na michango yake kukatwa, ni kazi ya mwajiri.

Kama mwajiri hakuleta huo mfuko sheria zote zimesema yeye ndio akazitafute hizo pesa kwa mwajiri. Haiyumkiniki mwajiriwa ataanza kwenda kumwambia mwajiri peleka pesa yangu, kwa sababu anaogopa na yeye atamuudhi mwajiri. Kwa hiyo, ndiyo maana sheria imeweka kwa sura hiyo.

Kwa hiyo, niwaombe sana, kwenye hili naamini mwaka ujao wa fedha michango ya Wabunge hapa tutakapokuwa tunaizungumzia 2024/2025, *Inshallah,* Mwenyezi Mungu atuweke, basi naamini hili tutakuwa tukiipongeza Serikali kwamba imepiga hatua, hakuna wastaafu ambao wanasubiri sana.

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho; mwongozo uliombwa jana hapa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar kuhusu baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kutumia lugha zisizo na staha Bungeni.

Waheshimiwa Wabunge, jana jioni tarehe 19 Aprili, 2023 katika Kikao cha Kumi cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar alisimama na kuomba mwongozo wa Spika akitumia Kanuni ya 76 ya Kanuni za Kudumu za Bunge ambapo alieleza kuwa kumekuwa na matumizi ya lugha zisizo na staha kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala wa Hoja ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Waheshimiwa Wabunge, nukuu ya maelezo hayo ni kama ifuatavyo; "Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uchangiaji ambao unaendelea ndani ya Bunge sasa hivi, hasa Bunge la jioni ya leo. Kuna lugha ambazo zinatumika siyo za staha, mfano kuwaita watumishi ambao wameaminiwa na Serikali ambao wanaitwa Maafisa Utumishi, kwamba ni "mambumbumbu". Na kuna mchangiaji mwingine amesema "washamba", tuache "ushamba". Hizi lugha nadhani siyo nzuri." Mwisho wa kunukuu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea maombi ya mwongozo huo, Mheshimiwa Mwenyekiti aliahidi kupitia Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* ili kuthibitisha maelezo yaliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge na baadaye kutoa mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, katika mchango wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo wakati akichangia hoja ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, alieleza kuwa, nanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili jambo la ajira ambalo tumekuwa tukilizungumza sana hapa Bungeni na ni mjadala mkubwa hivi sasa. Kwenye eneo la ajira hapa tuna wataalam wabobezi hapa

wakiwemo walimu wetu waliotufundisha vyuo vikuu. Walitufundisha kuajiri kwa kutumia sifa kuondokana ma mambo ya nepotism, tuzingatie *bureaucratic systems* kwa kuajiri kupitia *nepotism*, mambo ya undugu, kufahamiana huyu ni mtoto wa fulani; huu ni ushamba, huu ni utumishi wa kishamba yaani mtu mshamba ambaye hajastaarabika, ataenda kumuangalia ndugu yake badala ya kuzingatia sifa."

Waheshimiwa Wabunge, aidha, katika mchango wa Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane wakati akichangia mjadala wa hoja hiyohiyo, alisema, nanukuu; "Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kuchangia kwenye suala la mafunzo kwa maafisa utumishi. Maafisa utumishi wetu wengi wamekariri *Standing Orders* au zile Kanuni za Utumishi wa Umma. Wengi ni mambumbumbu katika sheria mama, ile…"

Waheshimiwa Mawaziri, naona hapo mnaongea sana na nimesimama. Nimewasikia kwa muda, naona mnajisahau kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, narejea tena kunukuu yale aliyoyasema Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane; "Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kuchangia kwenye suala la mafunzo kwa Maafisa Utumishi. Maafisa Utumishi wetu wengi wamekariri *Standing Orders* au zile Kanuni za Utumishi wa Umma. Wengi ni mambumbumbu katika sheria mama, ile ya Ajira na Mahusiano Kazini."

Waheshimiwa Wabunge, nimepitia Kamusi Kuu ya Kiswahili iliyochapishwa na Baraza Kuu la Kiswahili Tanzania (BAKITA) ili kupata mana fasaha ya maneno yaliyolalamikiwa. Kwa mujibu wa Kamusi hiyo neno mshamba limeelezwa kuwa na maana ya mtu anayetenda jambo baya kinyume na matarajio ya watu wengi. Vilevile neno hilo lina maana ya mpumbavu. *(Makofi)*

Neno mbumbumbu maana yake ni tusi analotukanwa mtu kwa kutojua kile anachoambiwa. Vilevile neno hilo lina maana ya juha, mjinga au mtu asiyejua chochote.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 71(i) mpaka (j) inakataza Mbunge wakati wa mjadala katika Bunge kutumia lugha ya matusi au ishara inayoashiria matusi au kumsema vibaya Mbunge au mtu mwingine. Vilevile Kanuni zinakataza kutumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine.

Pamoja na kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge hao ambao nilishawataja haikuwa na nia ya kuwadunisha watumishi au maafisa utumishi, kwa mujibu wa Kanuni zetu ni wazi kuwa maneno hayo yaliyolalamikiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar ni maneno yasiyoruhusiwa kutumika Bungeni. *(Makofi)*

Kwa hali hiyo, naelekeza maneno hayo yaondolewe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, vilevile nitumie nafasi hii kusisitiza Wabunge wote mnaopata nafasi ya kuzungumza ama kuchangia hoja hapa Bungeni mnapaswa kuzingatia masharti ya Kanuni yetu hiyo ya 71 na kutumia lugha yenye staha kwetu sisi wenyewe Wabunge na kwa watu wengine wote ambao tunakuwa tunawazungumzia katika kuchangia.

Kwa hiyo, huo ndiyo Mwongozo wa Spika kwenye jambo hili lililokuwa limeombwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu tangazo la Idi kwa kawaida huwa linategemea mwandamo wa mwezi, na mimi sina uwezo wa kujua kama mwezi umeshaandama ama vipi kwa sababu sote tuko katika kusubiri. Na katika kusubiri huko basi naahirisha shughuli

za Bunge mpaka siku ya Jumatatu, tarehe 24 Aprili, saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 24 Aprili, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*